# TAARIFA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Uchaguzi House,
Eneo la Uwekezaji Njedengwa,
Kitalu D, Kiwanja Na. 4,
S.L.P. 358,
DODOMA.

© Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2021

ISBN 978 - 9976 - 9957 - 3 - 2

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini kwa maandishi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI**......v
**ORODHA YA CHATI**......vi
**MICHORO**......vii
**ORODHA YA VIAMBATISHO**......viii
**VIFUPISHO VYA MANENO**......ix
**SHUKRANI**......xii
**BARUA YA KUWASILISHA TAARIFA**......xiii
**DIBAJI**......xvi
**MUHTASARI WA TAARIFA**......xvii
**SURA YA KWANZA**......1
**UTANGULIZI**......1
1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania......1
1.2 Mfumo wa Siasa Tanzania......2
1.3 Mfumo wa Uchaguzi Tanzania......3
1.4 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania......4
1.5 Tume ya Taifa ya Uchaguzi......5
**SURA YA PILI**......9
**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**......9
2.1 Maandalizi ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura......9
2.2 Bajeti ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura......9
2.3 Utambuzi wa Maeneo ya Kiutawala na Uhakiki wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura......10
2.4 Maandalizi ya Kanuni na Nyaraka Nyingine Wakati wa Uboreshaji wa Daftari......11
2.5 Vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura......11
2.6 Ratiba ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura......11
2.7 Mifumo ya Uandikishaji wa Wapiga Kura......13
2.8 Uteuzi wa Watendaji wa Zoezi la Uboreshaji wa Daftari......13
2.9 Mafunzo kwa Watendaji wa Uandikishaji......14
2.10 Uandikishaji wa Majaribio wa Wapiga Kura......14
2.11 Mafanikio katika Zoezi la Uandikishaji wa Majaribio......15
2.12 Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Vituoni......15
2.13 Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura......16
2.14 Matokeo ya Uandikishaji wa Wapiga Kura......17
2.15 Mlipuko wa Ugonjwa wa COVID - 19......19

2.16 Uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura....20
**SURA YA TATU....22**
**MAANDALIZI YA UCHAGUZI MKUU....22**
3.1 Bajeti ya Uchaguzi Mkuu....22
3.2 Uhakiki na Utambuzi wa Maeneo ya Kiuchaguzi na Upangaji wa Vituo vya Kupigia kura....22
3.3 Kuandaa Kanuni, Maadili na Nyaraka za Uchaguzi....24
3.4 Vifaa vya Uchaguzi Mkuu....25
3.5 Mifumo ya Menejimenti ya Uchaguzi....27
3.6 Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020....27
3.7 Watendaji wa Uchaguzi....29
3.8 Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi....31
**SURA YA NNE....35**
**UTEUZI WA WAGOMBEA, KAMPENI NA MAADILI YA UCHAGUZI....35**
4.1 Uteuzi wa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais....35
4.2 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais....41
4.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge....41
4.4 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge....42
4.5 Rufaa za Wagombea Ubunge kwa Tume....43
4.6 Wagombea Ubunge Waliochaguliwa bila Kupingwa....44
4.7 Uteuzi wa Wagombea Udiwani....44
4.8 Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Udiwani....45
4.9 Rufaa za Wagombea Udiwani....46
4.10 Wagombea Udiwani Waliochaguliwa Bila Kupingwa....47
4.11 Malalamiko ya Wagombea....47
4.12 Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea....47
4.13 Kampeni za Uchaguzi....47
4.14 Maadili na Gharama za Uchaguzi....48
**SURA YA TANO....51**
**KUPIGA NA KUHESABU KURA....51**
5.1 Risala ya Mwenyekiti wa Tume kwa Wapiga Kura....51
5.2 Siku ya Uchaguzi....51
5.3 Maelekezo ya Kisera Kuhusu Kupiga Kura....52
5.4 Upigaji Kura....53
5.5 Mawakala wa Upigaji Kura....54
5.6 Usalama katika Vituo vya Kupigia Kura....54

5.7 Kuhesabu Kura....54
**SURA YA SITA....57**
**KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI....57**
6.1 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Rais....57
6.2 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge....60
6.3 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani....62
6.4 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum....64
6.5 Kesi za Kupinga Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani....68
**SURA YA SABA....71**
**ELIMU YA MPIGA KURA....71**
7.1 Mkakati wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura....71
7.2 Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020....71
7.3 Mwongozo kwa Vyombo vya Habari vya Umma na Vyama vya Siasa katika kutangaza Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020....72
7.4 Njia zilizotumika katika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura....72
**SURA YA NANE....84**
**USHIRIKISHWAJI WA WADAU WA UCHAGUZI....84**
8.1 Serikali....84
8.2 Vyama vya Siasa....84
8.3 Wapiga Kura....87
8.4 Taasisi na Asasi za Kiraia....88
8.5 Vyombo vya Habari....88
8.6 Taasisi za Dini....89
8.7 Makundi Maalum katika Jamii....89
8.8 Vyombo vya Ulinzi na Usalama....90
8.9 Wazee wa Kimila na Wazee Maarufu....91
8.10 Maoni na Mapendekezo ya Wadau....92
**SURA YA TISA....93**
**WATAZAMAJI WA UCHAGUZI....93**
9.1 Mialiko kwa Watazamaji wa Uchaguzi....93
9.2 Usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi....93
9.3 Mikutano ya Tume na Watazamaji wa Uchaguzi....94
9.4 Kamati ya Watazamaji na Mashirika ya Kimataifa....95
9.5 Taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi....96
**SURA YA KUMI....99**
**TATHMINI YA UCHAGUZI MKUU....99**

10.1 Maeneo ya Tathmini....................................................................................................99
10.2 Walengwa wa Tathmini...............................................................................................99
10.3 Njia Zilizotumika Kufanya Tathmini.........................................................................100
10.4 Matokeo ya Tathmini.................................................................................................100
**SURA YA KUMI NA MOJA..........................................................................................105**
**MAFANIKIO NA CHANGAMOTO................................................................................105**
11.1 Mafanikio Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura........105
11.2 Mafanikio Wakati wa Uchaguzi Mkuu..................................................................105
11.3 Changamoto...............................................................................................................106
**SURA YA KUMI NA MBILI...........................................................................................108**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO...............................................................................108**
12.1 Hitimisho.....................................................................................................................108
12.2 Mapendekezo ..........................................................................................................108

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Orodha ya Vyama vya Siasa Vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka, 2020.....3
Jedwali Na. 2: Matokeo ya Utambuzi wa Maeneo ya Kiutawala.................................................10
Jedwali Na. 3: Matokeo ya Uhakiki wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura...........................10
Jedwali Na. 4: Watendaji wa Uandikishaji wa Daftari Walioteuliwa na Tume............................13
Jedwali Na. 5: Takwimu za Uandikishaji wa Wapiga Kura wa Majaribio..................................15
Jedwali Na. 6: Takwimu za Wapiga Kura kwa Umri..................................................................18
Jedwali Na. 7: Takwimu za Wapiga Kura kwa Jinsi...................................................................19
Jedwali Na. 8: Takwimu za Watu wenye Ulemavu Walioandikishwa.........................................19
Jedwali Na. 9: Majimbo Yaliyobadilishwa Majina......................................................................23
Jedwali Na.10: Majimbo Yaliyobadilishiwa Maeneo ya kiutawala.............................................23
Jedwali Na.11: Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.......................................................28
Jedwali Na.12: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Tanzania Bara................................................30
Jedwali Na.13: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi kwa Tanzania Zanzibar ................................30
Jedwali Na.14: Idadi ya Watendaji wa Vituo.............................................................................31
Jedwali Na.15: Idadi ya Watendaji Waliopatiwa Mafunzo katika Ngazi ya Jimbo na Kata kwa Tanzania Bara .........................................................................................................32
Jedwali Na.16: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Waliopatiwa Mafunzo kwa Tanzania Zanzibar.......32
Jedwali Na.17: Watendaji wa Vituo Waliopatiwa Mafunzo..........................................................33
Jedwali Na.18: Wagombea Walioteuliwa Kugombea Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais........38
Jedwali Na.19: Wagombea ambao Hawakuteuliwa kwa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais.........39
Jedwali Na.20: Wagombea Ubunge Walioteuliwa .......................................................................42
Jedwali Na.21: Rufaa za Wagombea Ubunge .............................................................................43
Jedwali Na.22: Wagombea Udiwani Walioteuliwa .....................................................................45
Jedwali Na.23: Rufaa za Wagombea Udiwani ............................................................................46
Jedwali Na.24: Matokeo ya Kura Alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais...............................59
Jedwali Na.25: Wabunge Waliochaguliwa .................................................................................62
Jedwali Na.26: Kata Ambazo Uchaguzi Uliahirishwa...................................................................63
Jedwali Na.27: Madiwani Waliochaguliwa ..................................................................................63
Jedwali Na.28: Aina za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano..........................................65
Jedwali Na.29: Mgawanyo wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum...........................................67
Jedwali Na.30: Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.....................................................67
Jedwali Na.31: Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum ..............................................68
Jedwali Na.32: Kesi za Kupinga Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani.......................69
Jedwali Na.33: Sampuli ya Watu Walioshiriki katika Zoezi la Tathmini..................................100

# ORODHA YA CHATI

Chati Na. 1: Asilimia ya Viti vya Ubunge kwa kila Chama.............................................61
Chati Na. 2: Asilimia ya Madiwani wa Kuchaguliwa kwa Jinsi......................................64

## MICHORO

Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi........................................................................5
Mchoro Na. 2: Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi....................................................7

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 1: Idadi ya Wapiga Kura Walioandikishwa kwa kila Mkoa...............109
Kiambatisho Na. 2: Orodha ya Wabunge Waliochaguliwa bila Kupingwa....................111
Kiambatisho Na. 3: Risala ya Mwenyekiti....................................................................112
Kiambatisho Na. 4: Orodha ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum..........................120

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AAFP | Alliance for African Farmers Party |
| ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency- Wazalendo |
| ADA-TADEA | African Democratic Alliance-Tanzania Democratic Alliance |
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| AFIS | Automated Fingerprint Identification System |
| AG | Attorney General |
| ASP | Afro-Shirazi Party |
| BVR- Kit | Biometric Voters' Registration-Kit |
| CCK | Chama Cha Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHADEMA | Chama Cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama Cha Ukombozi wa Umma |
| CMS | Candidate Management System |
| COVID-19 | Corona Virus Disease - 2019 |
| CUF | Civic United Front |
| DP | Democratic Party |
| Dkt. | Daktari |
| EISA | Electoral Institute for Sustainable Democracy in Africa |
| EO | Election Officer |
| GIS | Geographical Information System |

| | |
|---|---|
| GN | Government Notice |
| JNICC | Julius Nyerere International Convention Centre |
| MAKINI | Demokrasia MAKINI |
| Mhe. | Mheshimiwa |
| Mst. | Mstaafu |
| Na. | Namba |
| NEC | National Electoral Commission |
| NIDA | National Identification Authority |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform-Mageuzi |
| Ndg. | Ndugu |
| NLD | National League for Democracy |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| OMS | Observers Management System |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PNVRS | Permanent National Voters Register System |
| PVC | Polyvinyl Chloride |
| REC | Regional Election Coordinator |
| REDET | Research and Education for Democracy in Tanzania |
| RMS | Results Management System |
| SAU | Sauti ya Umma |
| TANePS | Tanzania National e-Procurement System |
| TANU | Tanganyika African National Union |

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| ToT | Training of Trainers |
| UDP | United Democratic Party |
| UMD | Union for Multiparty Democracy |
| UPDP | United Peoples' Democratic Party |
| UTP | United Tanganyika Party |
| VIS | Voters Interaction System |
| VRS | Voters Registration System |
| WLMS | Warehouse and Logistic Management System |
| ZEC | Zanzibar Electoral Commission |
| ZPPP | Zanzibar and Pemba People's Party |

# SHUKRANI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanikiwa kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kufanikiwa huko, pamoja na mambo mengine, kumetokana na ushiriki wa wadau wa uchaguzi katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Tume inatumia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote kwa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Wadau hao ni pamoja na wizara, wakala na taasisi mbalimbali za Serikali, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, vyama vya siasa na wagombea, watazamaji wa uchaguzi, viongozi wa dini, vyombo vya habari, makundi maalum katika jamii, asasi za kiraia pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama.

Kwa namna ya pekee, Tume inatoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga na kutoa fedha zilizowezesha kuendesha na kukamilisha shughuli za uchaguzi. Shukrani pia, ziende kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuipatia Tume jengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kuwezesha kupatikana kwa rasilimali watu wakati wa zoezi la uchaguzi. Halikadhalika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaishukuru Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kwa ushirikiano iliouonesha katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

Shukrani pia, ziwaendee watendaji wote wa uchaguzi kuanzia ngazi ya Taifa hadi kituo cha kupigia kura, kwani mafanikio ya uchaguzi mkuu yalitokana na weledi, umakini na umahiri wao katika kutekeleza majukumu waliyopewa.

Mwisho, Tume inatoa shukrani kwa wapiga kura waliojitokeza siku ya uchaguzi na Watanzania wote kwa ujumla kwa kudumisha amani na utulivu katika hatua zote za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**BARUA YA KUWASILISHA TAARIFA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

***Anwani ya Simu "UCHAGUZI".***
***Nambari ya Simu: +255-262962345-8***
***Nambari ya Faksi: +255 262962348***
***Barua Pepe: uchaguzi@nec.go.tz***
***Tovuti: www.nec.go.tz***

*(Barua zote za kiofisi ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi)*

Uchaguzi House,
Eneo la Uwekezaji Njedengwa,
Kitalu D, Kiwanja Na. 4,
S.L.P. 358,
DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja: Tarehe: 20 Julai, 2021

Kumb: Na. CEA.74/75/01/148

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
S. L. P. 1102,
**40400 DODOMA.**

*Mheshimiwa Rais,*

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kukutaarifu kuwa imekamilisha zoezi la kusimamia, kuratibu na kuendesha uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara. Uchaguzi huo ulifanyika siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020 ambayo ilitangazwa kuwa ni siku ya mapumziko.

Kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 74(6) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, majukumu ya Tume ni haya yafuatayo: -

(i) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;

(ii) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge;

(iii) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;

(iv) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa Madiwani;

(v) kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum;

(vi) kutoa elimu ya mpiga kura nchini kote; kuratibu na kusimamia watu na taasisi zote zinazotoa elimu hiyo; na

(vii) kuteua na kuwatangaza Madiwani Wanawake wa Viti Maalum.

*Mheshimiwa Rais,*

Ibara ya 74 ya Katiba imetaja muundo wa Tume na uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wake na kwamba, kila Mjumbe wa Tume atatumikia madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, Katiba inaeleza kuwa, Tume katika utekelezaji bora wa majukumu yake, itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao, na mtendaji mkuu wake ni Mkurugenzi wa Uchaguzi.

*Mheshimiwa Rais,*

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kama sheria inavyoelekeza. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kuandikisha wapiga kura wapya, kuboresha taarifa za wapiga kura hususan waliohama maeneo yao ya kiuchaguzi, kutoa kadi mpya kwa waliopoteza au kadi zao kuharibika na kuondoa wapiga kura waliokosa sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la uboreshaji, idadi ya wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni 29,754,699 ikilinganishwa na wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015. Hili ni ongezeko la wapiga kura 6,593,259 sawa na asilimia 28.47.

Aidha, siku ya kupiga kura jumla ya wapiga kura 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 walijitokeza kupiga kura kati ya wapiga kura 29,754,699 walioandikishwa. Kura halali zilikuwa 14,830,195 sawa na asilimia 98.27 ya kura zote zilizopigwa na kura zilizokataliwa zilikuwa 261,755 sawa na asilimia 1.73 ya kura zote zilizopigwa.

*Mheshimiwa Rais,*
Kwa ujumla, Tume iliendesha uchaguzi mkuu katika hali ya amani na utulivu. Mafanikio hayo yalitokana na maandalizi yaliyofanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Tume pia ilipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi.

*Mheshimiwa Rais,*
Baada ya uchaguzi mkuu kukamilika, Tume imeandaa taarifa inayoelezea namna mchakato wa uchaguzi ulivyofanyika.

Kwa heshima na taadhima, Tume inaomba kuwasilisha kwako Taarifa ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2020.

..............................................

Jaji Rufaa (Mst.) Semistocles S. Kaijage
Mwenyekiti

..............................................

Jaji Rufaa (Mst.) Mbarouk S. Mbarouk
Makamu Mwenyekiti

..............................................

Jaji (Mst.) Mary H. C. S. Longway
Mjumbe

..............................................

Asina A. Omari
Mjumbe

..............................................

Jaji (Mst.) Thomas B. Mihayo
Mjumbe

..............................................

Balozi Omar R. Mapuri
Mjumbe

..............................................

Dkt. Wilson Mahera Charles
Mkurugenzi wa Uchaguzi

## DIBAJI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilisimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020. Baada ya kukamilika kwa mchakato wa uchaguzi, kazi inayofuata ni kuandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taarifa iliyoandaliwa inaelezea namna mchakato wa uchaguzi ulivyoendeshwa na ina jumla ya sura 12 kama ifuatavyo: -

1. Utangulizi
2. Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
3. Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu
4. Uteuzi wa Wagombea, Kampeni na Maadili ya Uchaguzi
5. Kupiga na Kuhesabu Kura
6. Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi
7. Elimu ya Mpiga Kura
8. Ushirikishwaji wa Wadau wa Uchaguzi
9. Watazamaji wa Uchaguzi
10. Tathmini ya Uchaguzi Mkuu
11. Mafanikio na Changamoto
12. Hitimisho na Mapendekezo

Tume imeandaa taarifa hii ikiwa na mambo muhimu ambayo wadau wa uchaguzi watahitaji kwa matumizi mbalimbali katika nyanja za utafiti, rejea, ushauri, taaluma na kwa ajili ya maandalizi ya chaguzi zijazo.

## MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii inahusu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa upande wa Tanzania Bara uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020. Taarifa inaonesha mchakato mzima wa uchaguzi kuanzia uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hadi kukamilika kwa uchaguzi mkuu. Taarifa imegawanyika katika sura kumi na mbili kama ifuatavyo: -

**Sura ya Kwanza** inaelezea kuhusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muundo wake wa kiutawala, mfumo wa siasa na mfumo wa uchaguzi. Vilevile, imeelezea juu ya mzunguko wa uchaguzi, muundo, majukumu, mamlaka na madaraka ya Tume.

**Sura ya Pili** inaelezea namna zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilivyofanyika. Aidha, imebainisha kuwa uboreshaji wa Daftari ulifanyika mara mbili na ulitumia jumla ya Shilingi za Tanzania 154,313,824,607.88. Sura hii, imeonesha matokeo ya uandikishaji ambapo, baada ya zoezi la uboreshaji kukamilika, Daftari lina jumla ya wapiga kura 29,754,699 kutoka wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la wapiga kura 6,593,259. Uboreshaji huo wa Daftari ulifanyika katika vituo 37,814 vya kuandikisha wapiga kura nchi nzima.

**Sura ya Tatu** ni maelezo juu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Pamoja na mambo mengine, imeonesha kuwa Tume ilitumia jumla ya Shilingi za Tanzania 262,493,380,671.00 katika kuendesha uchaguzi mkuu. Fedha hizo zilitengwa na kutolewa na Serikali kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Mambo mengine ambayo yameainishwa katika Sura hii ni uandaaji wa ratiba ya uchaguzi, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo kwa watendaji, uteuzi na mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi. Aidha, Sura hii inaelezea ununuzi na usambazaji wa vifaa vya uchaguzi.

**Sura ya Nne** inahusu uteuzi wa wagombea, kampeni na maadili ya uchaguzi. Tarehe 25 Agosti, 2020 ilikuwa siku ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Katika nafasi ya kiti cha Rais jumla ya wagombea 17 walijitokeza. Kati ya hao, wagombea 15 waliteuliwa kuwania nafasi hiyo.

Kwa nafasi ya Ubunge jumla ya wagombea 1,257 waliteuliwa. Aidha, kwa nafasi ya Udiwani jumla ya wagombea 9,231 waliteuliwa.
Sura hii pia, inaelezea kuanza kwa kampeni na namna zilivyofanyika kwa amani na utulivu. Kampeni zilianza tarehe 26 Agosti, 2020 na kumalizika tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Bara na tarehe 26 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Zanzibar. Pia, inazungumzia usimamizi na utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**Sura ya Tano** inaelezea kuhusu siku ya uchaguzi na utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura vituoni. Upigaji kura ulifanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 siku ya Jumatano kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi 10:00 jioni. Zoezi la kupiga kura lilifanyika katika vituo vya kupigia kura 81,567 nchi nzima ikilinganishwa na vituo 65,105 vya mwaka 2015. Baada ya upigaji kura kukamilika, vituo hivyo vilitumika kuhesabia kura.

**Sura ya Sita** inaelezea kuhusu zoezi la kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara. Sura hii imeeleza kuwa kati ya wapiga kura 29,754,699 walioandikishwa kwenye Daftari, wapiga kura 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 walijitokeza kupiga kura. Aidha, maelezo yametolewa juu ya utaratibu uliotumika kujumlisha kura ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo, ambao uliiwezesha Tume kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais ndani ya saa 48 tangu zoezi la kupiga kura kukamilika. Utaratibu uliotumika kuwapata Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum umeelezwa katika Sura hii. Mwisho, kesi za kupinga matokeo ya uchaguzi wa Ubunge na Udiwani zilizofunguliwa Mahakamani zimeainishwa.

**Sura ya Saba** inahusu elimu ya mpiga kura na namna elimu hiyo ilivyotolewa wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na kipindi cha uchaguzi mkuu. Sura hii imeainisha njia mbalimbali zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura ikiwemo vyombo vya habari, mikutano na wadau, gari la matangazo la Tume, machapisho pamoja na uchaguzi wa mfano (*mock election*) kwa waandishi wa habari. Aidha, imeainisha idadi ya taasisi na asasi zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura, ambapo wakati wa uboreshaji wa Daftari kulikuwa na taasisi na asasi 28 na wakati wa uchaguzi mkuu zilikuwa 252.

**Sura ya Nane** inafafanua juu ya ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi. Wadau hao ni pamoja na Serikali, vyama vya siasa, viongozi wa taasisi za dini, taasisi na asasi za kiraia, vyombo vya habari, wazee wa kimila na wazee maarufu. Vilevile, imewataja wadau wengine wakiwemo makundi maalum katika jamii ambayo ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Sura ya Tisa** inaelezea kuhusu watazamaji wa uchaguzi wa ndani na kimataifa. Imeainisha utaratibu uliotumika kutoa mialiko na kuwasajili watazamaji hao ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji (OMS). Jumla ya taasisi za ndani 97 zenye jumla ya watazamaji 5,297 na taasisi za kimataifa 17 zenye jumla ya watazamaji 196 zilipewa vibali kwa ajili ya kutazama shughuli za uchaguzi. Imeainisha pia, maoni na mapendekezo yaliyotolewa na baadhi ya watazamaji wa uchaguzi waliowasilisha taarifa zao.

**Sura ya Kumi** inatoa tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 iliyofanyika kwa lengo la kupata mrejesho wa namna na jinsi uchaguzi huo ulivyoendeshwa. Imeelezea kuwa tathmini ilifanyika katika mikoa 24 na ilihusisha jumla ya wahojiwa 1,874 miongoni mwao ni watendaji wa uchaguzi, wapiga kura, viongozi wa vyama vya siasa na makundi maalum.

**Sura ya Kumi na Moja** inaainisha mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**Sura ya Kumi na Mbili** inahitimisha na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kuboresha chaguzi zijazo.


## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo katika Latitudi $0^0$ hadi $12^0$ Kusini mwa Ikweta; na Longitudi $25^0$ hadi $45^0$ Mashariki mwa Mstari wa Greenwich. Upande wa Kaskazini Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda; Magharibi inapakana na Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia; upande wa Kusini inapakana na Msumbiji na Malawi na upande wa Mashariki ni Bahari ya Hindi kama inavyoonekana kwenye ramani.

**Ramani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**




Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 945,203 linalojumuisha iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zilizoungana tarehe 26 Aprili, 1964.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na idadi ya watu wapatao milioni 44.9 ambapo Tanzania Zanzibar ilikuwa na idadi ya watu milioni 1.3 na Tanzania Bara ilikuwa na idadi ya watu milioni 43.6.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, makadirio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020 yalikuwa ni milioni 57.6. Tanzania ina makabila zaidi ya 120 na Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa.

Kiutawala, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imegawanyika katika mikoa 31. Tanzania Bara ina mikoa 26, wilaya 139, halmashauri 184, kata 3,956, mitaa 4,263 na vijiji 12,319. Tanzania Zanzibar ina mikoa 5, wilaya 11 na shehia 388.

### 1.2 Mfumo wa Siasa Tanzania

Kwa mujibu wa ibara ya 3(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mfumo wa vyama vingi vya siasa ulirejeshwa mwaka 1992 baada ya kufutwa mwaka 1964 kwa upande wa Tanzania Zanzibar na mwaka 1965 kwa upande wa Tanzania Bara. Tangu kurejeshwa kwa mfumo huo, jumla ya chaguzi sita zimefanyika kila baada ya miaka mitano kuanzia mwaka 1995 hadi 2020.

Tanganyika (Tanzania Bara) ilikuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa kabla ya kupata uhuru mwaka 1961. Vyama vilivyokuwepo ni Tanganyika African National Union (TANU), United Tanganyika Party (UTP) na African National Congress (ANC) ambavyo vilishiriki kwenye chaguzi zilizofanyika wakati huo. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar vyama vya Afro-Shirazi Party (ASP), Zanzibar and Pemba People’s Party (ZPPP), UMMA Party na Zanzibar Nationalist Party (ZNP) vilishiriki kwenye chaguzi kabla ya mwaka 1964.

Mfumo wa vyama vingi vya siasa ulifutwa Zanzibar mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na kwa Tanzania Bara, mwaka mmoja baadae. Baada ya kufutwa kwa mfumo wa vyama vingi, Tanzania Bara ilibaki na chama cha TANU na Tanzania Zanzibar ilibaki na chama cha ASP. Vyama hivyo viliungana mwaka 1977 na kuunda chama kimoja cha siasa ambacho ni Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kwa mujibu wa kifungu cha 8 na 8A vya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imepewa jukumu la kusajili na kusimamia vyama vya siasa nchini. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu vilishiriki uchaguzi. Orodha ya vyama hivyo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1: Orodha ya Vyama vya Siasa Vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka, 2020**

| Na. | Chama cha Siasa |
|---|---|
| 1. | Alliance for African Farmers Party (AAFP) |
| 2. | Alliance for Change and Transparency - Wazalendo (ACT - Wazalendo) |
| 3. | African Democratic Alliance - Tanzania Democratic Alliance (ADA - TADEA) |
| 4. | Alliance for Democratic Change (ADC) |
| 5. | Chama Cha Kijamii (CCK) |
| 6. | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 7. | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) |
| 8. | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) |
| 9. | Civic United Front (CUF) |
| 10. | Demokrasia Makini (MAKINI) |
| 11. | Democratic Party (DP) |
| 12. | National Convention for Construction and Reform - Mageuzi (NCCR -Mageuzi) |
| 13. | National League for Democracy (NLD) |
| 14. | National Reconstruction Alliance (NRA) |
| 15. | Sauti ya Umma (SAU) |
| 16. | Tanzania Labour Party (TLP) |
| 17. | United Democratic Party (UDP) |
| 18. | Union for Multiparty Democracy (UMD) |
| 19. | United Peoples' Democratic Party (UPDP) |

### 1.3 Mfumo wa Uchaguzi Tanzania

Kwa mujibu wa kifungu cha 35 F (8) na 80(1) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tanzania hutumia mfumo wa uchaguzi ambao mgombea anayepata kura nyingi halali kuliko mgombea mwingine yeyote ndiye hutangazwa kuwa mshindi (*first - past – the - post*). Mfumo mwingine unaotumika ni ule wa uwiano wa kura (*proportional representation*) ambao hutumika kupata Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum. Mfumo huo unazingatia masharti ya ibara ya 66 na 78 za Katiba zikisomwa


pamoja na kifungu cha 86A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Ibara ya 66(1) (b) ya Katiba inaelekeza kuwa idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum isipungue asilimia 30 ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuzingatia sharti hilo la kikatiba, mwaka 2010 idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum iliongezwa hadi kufikia asilimia 40.

Idadi ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika mabaraza ya halmashauri, haitakiwi kupungua theluthi moja (1/3) ya madiwani wa kuchaguliwa wa halmashauri husika. Hii inatokana na matakwa ya kifungu cha 35(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, kifungu cha 19(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 pamoja na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

### 1.4 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inasimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Uchaguzi Mkuu hufanyika kila baada ya kipindi cha miaka mitano. Jukumu hilo hutekelezwa kwa mujibu wa ibara ya 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 12 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Tume hufuata mzunguko wa uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu. Awamu hizo ni shughuli kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Shughuli katika awamu hizo zimeoneshwa kwenye Mchoro Na. 1.

**Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi**




## 1.5 Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Tume ilianzishwa tarehe 13 Januari, 1993 kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa mujibu wa ibara ya 74(7) ya Katiba, Tume ni idara huru inayojitegemea na inafanya maamuzi rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao.


### 1.5.1 Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa kuzingatia ibara ya 74(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume inaundwa na Wajumbe saba. Wajumbe hao ni Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ambao wanapaswa kuwa na sifa ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au mtu mwenye sifa ya kuwa Wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka 15. Katika uteuzi wao, Rais atazingatia kuwa endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano.

Mjumbe mwingine atateuliwa kutoka miongoni mwa wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society - TLS). Wajumbe wanne watatakiwa wawe na uzoefu wa kutosha wa kuendesha au kusimamia uchaguzi wa Wabunge au sifa nyingine kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano atakavyoona inafaa kwa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Ibara ya 74(7) ya Katiba ikisomwa pamoja na kifungu cha 4(4) na 6 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Mkurugenzi wa Uchaguzi ndiye Katibu na Mtendaji Mkuu wa Tume. Tume inazo idara sita, ofisi ya Zanzibar na vitengo vitatu vinavyoongozwa na Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo kama inavyoonekana kwenye Mchoro Na. 2.

**Mchoro Na. 2: Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**



### 1.5.2 Dira na Dhima ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inaongozwa na Dira na Dhima ili kufanikisha malengo na matarajio yake.

#### 1.5.2.1 Dira

Kuwa chombo kinachoaminika Afrika katika kusimamia uchaguzi.

#### 1.5.2.2 Dhima

Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa uchaguzi mkuu na chaguzi ndogo kupitia uandikishaji wa wapiga kura, ugawaji wa majimbo na utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha demokrasia.

### 1.5.3 Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 74(6) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, majukumu ya Tume ni haya yafuatayo: -

(i) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;

(ii) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge;

(iii) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;

(iv) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa Madiwani;

(v) kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum;

(vi) kutoa elimu ya mpiga kura nchini kote; kuratibu na kusimamia watu na taasisi zote zinazotoa elimu hiyo; na

(vii) kuteua na kuwatangaza Madiwani Wanawake wa Viti Maalum.

# SURA YA PILI

## UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili, baada ya uchaguzi mkuu mmoja uliomalizika na siku moja kabla ya uteuzi wa wagombea katika uchaguzi mkuu unaofuata. Jukumu hili hutekelezwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Tume iliendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari mara mbili kama ilivyoainishwa kwenye sheria. Uboreshaji huo ulihusisha uandikishaji wa wapiga kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 au zaidi na ambao walitarajiwa kutimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi. Aidha, uboreshaji huo pia ulihusisha wapiga kura walioandikishwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ambao walihitaji kurekebisha taarifa zao ikiwemo waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika na waliohama maeneo yao ya kiuchaguzi. Zoezi hilo pia lilihusisha kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa kwa mujibu wa sheria wakiwemo waliofariki.

### 2.1 Maandalizi ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Maandalizi ya zoezi la uboreshaji wa Daftari yalihusisha uandaaji wa bajeti na uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura. Pia, yalihusisha maandalizi ya kanuni, ununuzi wa vifaa, kuhuisha maelekezo kwa watendaji wa uboreshaji wa Daftari na wadau wa uchaguzi, uteuzi wa watendaji na mafunzo.

### 2.2 Bajeti ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Tume iliandaa bajeti ya jumla ya Shilingi za Tanzania 154,313,824,607.88 kwa ajili ya kuendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kiasi hicho cha fedha kilitengwa na kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Malipo hayo yalifanyika kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 120 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Fedha hizo, pamoja na mambo mengine, zilitumika kununua na kusafirisha vifaa vya uandikishaji na uchapishaji wa nyaraka. Vilevile, zilitumika katika mafunzo na kulipa stahiki za watendaji pamoja na kulipa kodi kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

## 2.3 Utambuzi wa Maeneo ya Kiutawala na Uhakiki wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura

### 2.3.1 Utambuzi wa Maeneo ya Kiutawala

Tume ilifanya utambuzi wa maeneo ya kiutawala katika ngazi ya mkoa, wilaya, halmashauri, jimbo, kata, shehia, mitaa na vijiji. Lengo la utambuzi huo lilikuwa ni kujiridhisha endapo hakuna mabadiliko ambayo yangeweza kuathiri muundo wa kanzidata ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Matokeo ya utambuzi huo yanaoneshwa kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Matokeo ya Utambuzi wa Maeneo ya Kiutawala**

| Na. | Eneo la kiutawala | Mwaka 2015 | Mwaka 2020 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **Tanzania Bara** | | |
| 1. | Mikoa | 25 | 26 |
| 2. | Halmashauri | 178 | 184 |
| 3. | Kata za Tanzania Bara | 3,953 | 3,956 |
| **B.** | **Tanzania Zanzibar** | | |
| 1. | Mikoa | 5 | 5 |
| 2. | Wilaya za Zanzibar | 11 | 11 |
| 3. | Shehia | 386 | 388 |

### 2.3.2 Uhakiki wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura

Baada ya kukamilika kwa zoezi la utambuzi wa maeneo ya kiutawala, Tume ilifanya uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura katika halmashauri na kata zote nchini kabla ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari.

Zoezi la uhakiki wa vituo lililenga kuona kama kuna haja ya kuongeza vituo katika baadhi ya maeneo, kuona kama vituo vilivyopo bado vinakidhi matakwa ya kisheria na kufanya marekebisho mengine kama vile kubadilisha majina ya vituo. Vilevile, uhakiki huo ulilenga kuhakikisha kila mtaa na kijiji kinakuwa na angalau kituo kimoja cha kuandikisha wapiga kura. Mchanganuo wa vituo vya kuandikisha wapiga kura umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Matokeo ya Uhakiki wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| Na. | Sehemu ya Nchi | Mwaka 2015 | Mwaka 2020 |
|---|---|---|---|
| 1. | Tanzania Bara | 36,549 | 37,407 |
| 2. | Tanzania Zanzibar | 380 | 407 |
| **Jumla** | | **36,929** | **37,814** |

## 2.4 Maandalizi ya Kanuni na Nyaraka Nyingine Wakati wa Uboreshaji wa Daftari

Tume hufanya mapitio ya kanuni na nyaraka nyingine za uchaguzi kwa lengo la kuboresha ili kuendana na mahitaji ya wakati husika. Tume ilifanya marekebisho ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2014 na kupata Kanuni za mwaka 2018.

Nyaraka nyingine zilizofanyiwa maboresho ni maelekezo kwa watendaji wa uboreshaji kama vile waratibu wa uandikishaji wa mikoa, maafisa waandikishaji, waandishi wasaidizi, *BVR Kit operators* pamoja na maelekezo kwa vyama vya siasa. Tume pia iliandaa Mwongozo wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura na Mwongozo wa Watazamaji wa Uboreshaji.

## 2.5 Vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Tume ilinunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya zoezi la uboreshaji wa Daftari. Vifaa hivyo vilihusisha vipuri vya *BVR Kits* vikiwemo kamera, betri, printa na wino. Vifaa vingine ni *servers*, vifaa vya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole – AFIS, kompyuta mpakato na kadi za PVC zilizotumika katika zoezi la kuandikisha wapiga kura. Tume pia, ilifanya ununuzi na uchapishaji wa nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na fomu na vitabu vya maelekezo kwa watendaji na wadau wa uboreshaji.

## 2.6 Ratiba ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Tume ilipanga ratiba iliyowezesha kufanyika kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari mara mbili. Uboreshaji huo ulifanyika kati ya tarehe 18 Julai, 2019 na 20 Juni, 2020. Upangaji wa ratiba ya utekelezaji wa zoezi la uboreshaji ulizingatia idadi ya vituo, vifaa na muda wa kukamilisha zoezi la uboreshaji wa Daftari.

Uzinduzi wa zoezi la uboreshaji wa Daftari ulifanyika tarehe 18 Julai, 2019 katika mkoa wa Kilimanjaro. Uzinduzi huo ulifanywa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama vya siasa, wadau na wananchi.







*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Kilimanjaro.*

## 2.7 Mifumo ya Uandikishaji wa Wapiga Kura

Wakati wa utekelezaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume ilitumia mifumo ya TEHAMA. Baadhi ya mifumo hiyo ni Mfumo wa Uandikishaji Wapiga Kura (Voter Registration System - VRS), Mfumo wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (Permanent National Voters Register Sytem - PNVRS), Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole - AFIS na Mfumo wa Uhakiki wa Taarifa za Wapiga Kura (Voters Interaction System -VIS).

## 2.8 Uteuzi wa Watendaji wa Zoezi la Uboreshaji wa Daftari

Tume iliteua jumla ya watendaji 97,041 wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika ngazi mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4. Uteuzi huo ulifanyika kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7A na 8 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 10 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

**Jedwali Na. 4: Watendaji wa Uandikishaji wa Daftari Walioteuliwa na Tume**

| Na. | Watendaji wa Uandikishaji | Tanzania Bara | Tanzania Zanzibar | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Waratibu Uandikishaji Mkoa (REC) | 26 | 2 | 28 |
| 2. | Maafisa Waandikishaji (RO) | 184 | 11 | 195 |
| 3. | Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Jimbo (ARO-Jimbo) | 642 | 150 | 792 |
| 4. | Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata (ARO-Kata) | 3,956 | 0 | 3,956 |
| 5. | Maafisa TEHAMA | 368 | 22 | 390 |
| 6. | Maafisa Uchaguzi | 184 | 0 | 184 |
| 7. | Waandishi Wasaidizi | 37,407 | 407 | 37,814 |
| 8. | BVR Kit Operators | 37,407 | 407 | 37,814 |
| 9. | Waandishi Wasadizi na BVR Kit Operators wa akiba | 15,824 | 44 | 15,868 |
| | **Jumla** | **95,998** | **1,043** | **97,041** |

### 2.9 Mafunzo kwa Watendaji wa Uandikishaji

Tume iliendesha mafunzo kwa watendaji wa uandikishaji kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuratibu na kusimamia zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mafunzo hayo yalitolewa kwa watendaji wa Tume makao makuu ambao waliandaliwa kuwa wakufunzi ili waweze kutoa mafunzo ya uandikishaji kwa watendaji wa ngazi ya mkoa, halmashauri, kata na vituo vya kuandikisha wapiga kura. Watendaji hao walifundishwa kuhusu namna ya kutumia *BVR kits* na Mfumo wa Uandikishaji Wapiga Kura (Voters Registration System-VRS), ujazaji wa fomu mbalimbali, utunzaji wa vifaa vya uandikishaji pamoja na usimamizi wa rasilimali fedha.



*Watendaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari wakiwa kwenye mafunzo kwa vitendo katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dodoma.*

### 2.10 Uandikishaji wa Majaribio wa Wapiga Kura

Kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari, Tume ilifanya uandikishaji wa wapiga kura wa majaribio. Zoezi hilo lililenga kupima ufanisi wa mifumo na vifaa katika mazingira tofauti ikiwemo maeneo yenye miundombinu mibovu ya barabara, vumbi, joto na changamoto za umeme.

Uandikishaji wa majaribio ulifanyika kuanzia tarehe 29 Machi, 2019 hadi tarehe 4 Aprili, 2019 katika Kata ya Kibuta iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Kata ya Kihonda iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Matokeo ya uandikishaji wa majaribio ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Takwimu za Uandikishaji wa Wapiga Kura wa Majaribio**

| Na. | Kata | Wapiga Kura | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wapya | Walioboresha taarifa | Walioondolewa | Jumla |
| 1. | Kihonda | 4,026 | 2,367 | 0 | 6,393 |
| 2. | Kibuta | 1,949 | 789 | 4 | 2,742 |
| Jumla | | 5,975 | 3,156 | 4 | 9,135 |

## 2.11 Mafanikio katika Zoezi la Uandikishaji wa Majaribio


Katika zoezi la uandikishaji wa majaribio, Tume ilifanikiwa kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kubaini kuwa mifumo ya VRS na BVR inaweza kufanya kazi kwa muda mrefu katika mazingira tofauti bila kuwa na changamoto zozote.

## 2.12 Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Vituoni

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulitumia Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Alama za Kibiolojia ujulikanao kama Biometric Voters Registration System - BVR. Mfumo huu ndio uliotumika kuandikisha wapiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Kwa kutumia mfumo huu, alama za vidole, picha na taarifa binafsi za mpiga kura zilichukuliwa na kuhifadhiwa katika kanzidata (*database*) ya Tume. Aidha, wapiga kura walioboresha taarifa zao au kuandikishwa upya walipatiwa kadi ya mpiga kura papohapo kituoni.

Taarifa za wapiga kura zilizohifadhiwa katika kanzidata ya Tume zilichakatwa kwa kutumia Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole - AFIS. Lengo lilikuwa ni kuondoa taarifa za wapiga kura zilizojirudia na hatimaye kuandaa Daftari la Awali la Wapiga Kura.




*Mhe. Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, akiboresha taarifa zake katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Kata ya Kilimani, Dodoma.*

### 2.13 Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura

Tume iliweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ili kutoa fursa kwa wapiga kura kuhakiki taarifa zao. Zoezi hili lilifanyika kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 11A na 22(2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 28(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Tume ilifanya zoezi hilo mara mbili kati ya tarehe 17 Aprili, 2020 na 20 Juni, 2020 ili kuhakikisha wapiga kura wanapata fursa ya kuhakiki taarifa zao. Uwekaji wazi wa Daftari la Awali ulifanyika kwenye vituo vyote 37,814 vilivyotumika katika uandikishaji wa wapiga kura. Uwekaji wazi wa Daftari ulitoa nafasi kwa wapiga kura kusahihisha taarifa zao, kuweka pingamizi kwa wasio na sifa za kuendelea kuwemo katika Daftari na kuondoa waliopoteza sifa wakiwemo waliofariki.

Pamoja na wapiga kura kwenda wenyewe vituoni kuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura, Tume pia iliandaa Mfumo wa Kuhakiki Taarifa za Wapiga Kura (Voters Interaction System - VIS).

Mfumo huu uliruhusu wapiga kura kuhakiki taarifa zao kwa kutumia simu za kiganjani za kawaida au simu janja (*smartphone*) kwa kupiga namba *152*00# au kwa kupitia tovuti ya Tume yaani; *www.nec.go.tz.* Vilevile, wapiga kura walihakiki taarifa zao kwa kupiga simu bila malipo katika kituo cha huduma kwa wateja cha Tume kupitia namba 0800112100.



*Baadhi ya Wapiga Kura wakihakiki taarifa zao wakati wa Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali.*

## 2.14 Matokeo ya Uandikishaji wa Wapiga Kura

Daftari la kudumu la Wapiga Kura linaloandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) linajumuisha pia wapiga kura walioandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 12A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinachoitaka NEC kutumia taarifa za wapiga kura waliondikishwa na ZEC. Idadi ya wapiga kura walioandikishwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ilikuwa 23,161,440. Kati ya hao 22,658,247 waliandikishwa na NEC na 503,193 waliandikishwa na ZEC.

Katika awamu zote mbili za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, jumla ya wapiga kura wapya 6,560,587 waliandikishwa na wapiga kura 3,548,846 waliboresha taarifa zao. Aidha, wapiga kura 30,487 waliondolewa kwenye Daftari kutokana na kukosa sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari kwa mujibu wa sheria. Baada ya zoezi la uboreshaji, Daftari la NEC lilikuwa na jumla ya wapiga kura 29,188,347 na Daftari la ZEC lilikuwa na jumla ya wapiga kura 566,352. Hivyo, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilikuwa na jumla ya wapiga kura 29,754,699 ikilinganishwa na wapiga kura walioandikishwa mwaka 2015 ambao ni 23,161,440 ikiwa ni ongezeko la wapiga kura 6,593,259 ambayo ni sawa na asilimia 28.47.

Idadi ya wapiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika kila mkoa ni kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 1. Pia, mchanganuo wa wapiga kura kwa umri, jinsi na makundi maalum (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 6 na 7.

**Jedwali Na. 6: Takwimu za Wapiga Kura kwa Umri**

| **Wapiga Kura Walioandikishwa na NEC** | | | |
|---|---|---|---|
| **Na.** | **Umri (miaka)** | **Jumla** | **Asilimia** |
| 1. | 18-35 | 15,745,499 | 53.94 |
| 2. | 36-50 | 7,664,343 | 26.26 |
| 3. | 51 na Zaidi | 5,778,505 | 19.80 |
| **Jumla** | | **29,188,347** | **100** |
| **Wapiga Kura Walioandikishwa na ZEC** | | | |
| **Na.** | **Umri (miaka)** | **Jumla** | **Asilimia** |
| 1. | 18-35 | 241,196 | 42.59 |
| 2. | 36-50 | 189,003 | 33.37 |
| 3. | 51 na Zaidi | 136,153 | 24.04 |
| **Jumla** | | **566,352** | **100** |
| **Jumla kuu ya walioandikishwa na NEC na ZEC** | | **29,754,699** | |

**Jedwali Na. 7: Takwimu za Wapiga Kura kwa Jinsi**

| Na. | Wapiga Kura | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Wapiga Kura walioandikishwa na NEC** | | | |
| 1. | Wanaume | 14,496,604 | 49.67 |
| 2. | Wanawake | 14,691,743 | 50.33 |
| Jumla | | 29,188,347 | 100.00 |
| **Wapiga Kura walioandikishwa na ZEC** | | | |
| Na. | Wapiga Kura | Idadi | Asilimia |
| 1. | Wanaume | 272,115 | 48.05 |
| 2. | Wanawake | 294,237 | 51.95 |
| Jumla | | 566,352 | 100.00 |

Katika uboreshaji wa Daftari wa mwaka 2019/2020 idadi ya watu wenye ulemavu walioandikishwa ni 13,211 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Takwimu za Watu wenye Ulemavu Walioandikishwa**

| Na. | Aina ya Ulemavu | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Ulemavu wa Macho | 2,223 |
| 2. | Ulemavu wa Mikono | 4,911 |
| 3. | Ulemavu wa aina nyingine | 6,077 |
| **Jumla** | | **13,211** |

## 2.15 Mlipuko wa Ugonjwa wa COVID-19

Wakati zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura likiendelea, dunia ilikumbwa na janga la ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya Corona. Kwa kutambua uwepo wa ugonjwa huo na kwa kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Tume ilitoa vifaa kinga pamoja na maelekezo ya tahadhari kwa watendaji na wananchi waliofika katika vituo vya kuandikisha wapiga kura ili kuzuia maambukizi na kusambaa kwa virusi hivyo. Watendaji wa uandikishaji walipatiwa vifaa kinga ambavyo ni pamoja na vitakasa mikono, *spirit, gloves, tissue* na barakoa. Vilevile, katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura kulikuwa na huduma ya maji tiririka na sabuni kwa ajili ya wananchi kunawa mikono.

Vifaa vya uboreshaji ambavyo kutokana na matumizi yake vingekuwa na hatari ya kusambaza virusi vya Corona vilisafishwa kwa dawa kabla na baada ya kutumika. Pia, Tume ilitoa maelekezo kwa watendaji na wananchi kuzingatia umbali kati ya mtu mmoja na mwingine (*social distancing*).



*Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikichukua hatua ya kupuliza dawa kwenye mashine za BVR ili kukabiliana na maambukizi ya Virusi vya Corona.*

### 2.16 Uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Tume ilikamilisha uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na orodha ya wapiga kura tarehe 15 Septemba, 2020 kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tume ilitoa nakala moja ya Daftari na nakala mbili za orodha ya wapiga kura kwa kila kituo cha kupigia kura nchi nzima. Daftari na orodha vilihakikiwa na kusambazwa kwenda kwenye vituo vya kupigia kura pamoja na vifaa vingine vya uchaguzi. Aidha, Tume ilitoa nakala tepe ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.




*Dkt. Wilson M. Charles, Mkurugenzi wa Uchaguzi akikabidhi nakala tepe ya Daftari kwa vyama vya siasa.*

# SURA YA TATU

# MAANDALIZI YA UCHAGUZI MKUU

Tume kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, hutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara. Tume ilifanya maandalizi mbalimbali ili kufanikisha jukumu hilo yakiwemo maandalizi ya bajeti ya uendeshaji wa uchaguzi, uhakiki wa maeneo ya uchaguzi, marekebisho ya kanuni, maandalizi ya maadili ya uchaguzi, ratiba ya uchaguzi, maandalizi ya vituo vya kupigia kura, ununuzi na usambazaji wa vifaa vya uchaguzi.

## 3.1 Bajeti ya Uchaguzi Mkuu

Tume baada ya kuandaa makisio ya bajeti ya uchaguzi mkuu kulingana na mahitaji, ilitengewa jumla ya Shilingi za Tanzania 331,858,287,981.00 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Tume iliomba na kupatiwa Shilingi za Tanzania 268,493,380,671.00. Kati ya fedha zilizopokelewa, Tume ilitumia Shilingi za Tanzania 262,493,380,671.00 hadi kukamilika kwa zoezi la uchaguzi mkuu. Shilingi za Tanzania 6,000,000,000.00 zilibaki na kurejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Gharama za uendeshaji wa uchaguzi zilipungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa Kieletroniki - TANePS ambao ulisaidia kuongeza uwazi na ushindani uliopelekea kushuka kwa bei za ununuzi wa vifaa.

## 3.2 Uhakiki na Utambuzi wa Maeneo ya Kiuchaguzi na Upangaji wa Vituo vya Kupigia Kura

Tume ilifanya utambuzi na uhakiki wa maeneo ya kiuchaguzi yakiwemo majimbo na kata. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Tume ilipanga vituo vya kupigia kura vilivyotokana na vituo vya kuandikisha wapiga kura.

### 3.2.1 Mgawanyo wa Majimbo

Tume inayo mamlaka ya kikatiba ya kuchunguza na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika majimbo kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge. Kwa mujibu wa ibara ya 74(6) (c) na 75 za

Katiba, Tume inaweza kutekeleza jukumu hilo mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka 10. Mara ya mwisho, Tume ilichunguza na kugawa majimbo mwaka 2015 ambapo iliongeza majimbo kutoka 232 hadi 264. Kati ya hayo, majimbo 214 yapo Tanzania Bara na 50 Tanzania Zanzibar.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume haikuchunguza mipaka wala kugawa majimbo ya uchaguzi. Idadi ya majimbo yaliyofanya uchaguzi yalikuwa 264 na kati ya hayo, majimbo mawili ya Tanzania Bara na Jimbo moja la Tanzania Zanzibar yalibadilishwa majina kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Majimbo Yaliyobadilishwa Majina**

| Na. | Halmashauri au Wilaya | Jina la Awali | Jina Jipya |
|---|---|---|---|
| 1. | Chamwino | Chilonwa | Chamwino |
| | | Mtera | Mvumi |
| 2. | Mjini Magharibi | Kijitoupele | Pangawe |

Aidha, maeneo ya kiutawala ya majimbo mawili ya Tanzania Bara yalibadilishwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Majimbo Yaliyobadilishiwa Maeneo ya Kiutawala**

| Na. | Jimbo | Eneo la Awali wa Kiutawala | Eneo Jipya la Kiutawala |
|---|---|---|---|
| 1. | Kilombero | Wilaya ya Kilombero | Halmashauri ya Mji Ifakara |
| 2. | Mchinga | Wilaya ya Lindi | Halmashauri ya Manispaa ya Lindi |

### 3.2.2 Kata za Uchaguzi

Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kinaitaka Tume kuzitambua na kuzitumia kata ambazo zimeanzishwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilipokea idadi na majina ya kata 3,956 za Tanzania Bara kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI). Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 12(3) cha Sheria hiyo, Tume ilitangaza kata hizo katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na. 551 la tarehe 17 Julai, 2020.

### 3.2.3 Kupanga na Kuhakiki Vituo vya Kupigia Kura

Tume ilipanga vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia idadi ya wapiga kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika kila kituo. Jumla ya vituo vya kupigia kura 81,567 vilipangwa kwa kuzingatia idadi ya wapiga kura wasiozidi 500 kwa kila kituo. Kati ya hivyo, vituo 80,155 vilitokana na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura walioandikishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na vituo 1,412 vilitokana na Daftari la Wapiga Kura walioandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Aidha, wasimamizi wa uchaguzi walifanya uhakiki wa vituo vya kupigia kura pamoja na ujenzi wa vituo vya muda katika maeneo ya wazi ambayo hayakuwa na majengo ya Umma.

## 3.3 Kuandaa Kanuni, Maadili na Nyaraka za Uchaguzi

Tume iliandaa Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Nyaraka nyingine zilizoandaliwa ni maelekezo kwa watendaji na wadau wa uchaguzi pamoja na maadili ya uchaguzi.

### 3.3.1 Kanuni za Uchaguzi za Mwaka 2020

Kifungu cha 124 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 125 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, vinaipa Tume mamlaka ya kuandaa Kanuni za Uchaguzi. Kwa kuzingatia mamlaka hayo, Tume iliandaa Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Tume ilishirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi hususan vyama vya siasa katika maandalizi ya kanuni hizo.

### 3.3.2 Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020

Kwa mujibu wa kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume kwa kushauriana na Serikali na vyama vya siasa, iliandaa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020. Maadili hayo yalisainiwa tarehe 27 Mei, 2020, na vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu, Serikali na Tume. Baada ya hatua hiyo, maadili ya uchaguzi yalichapishwa kwenye Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na. 722 la tarehe 05 Juni, 2020.

### 3.3.3 Mwongozo wa Watazamaji wa Uchaguzi, 2020

Tume kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 63(4) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Tume iliandaa Mwongozo wa Watazamaji wa Uchaguzi wa Mwaka 2020. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine umeainisha hatua za kutoa mwaliko na kusajili watazamaji wa ndani na kimataifa, haki na wajibu wa watazamaji na maadili ya watazamaji.

### 3.3.4 Maelekezo kwa Watendaji na Wadau wa Uchaguzi ya Mwaka 2020

Tume iliandaa maelekezo ya uchaguzi kwa ajili ya watendaji wa uchaguzi na vyama vya siasa. Maelekezo hayo yalikusudiwa kutoa mwongozo wa jinsi zoezi litakavyofanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi. Pia, yaliwawezesha watendaji wa uchaguzi, vyama vya siasa na mawakala kuelewa taratibu mbalimbali za uchaguzi na yalitumika kwa ajili ya rejea kipindi chote cha uchaguzi. Vilevile, mada zilizoandaliwa kwa ajili ya mafunzo zilizingatia maelekezo husika. Maelekezo hayo ni:-

(i) Maelekezo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, 2020;
(ii) Maelekezo kwa Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura, 2020;
(iii) Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura, 2020;
(iv) Maelekezo kwa Vyama vya Siasa na Wagombea, 2020; na
(v) Maelekezo kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa, 2020.

## 3.4 Vifaa vya Uchaguzi Mkuu

Maandalizi ya vifaa vya uchaguzi yalifanyika kwa kuzingatia idadi ya majimbo, kata, vituo vya kupigia kura, idadi ya wapiga kura, idadi ya watendaji wa uchaguzi na vyama vya siasa.


### 3.4.1 Ununuzi wa Vifaa vya Uchaguzi

Ununuzi wa vifaa vya uchaguzi ulifanyika kwa njia ya zabuni za ushindani na uwazi ili kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilitumia mfumo wa TANePS katika mchakato wa ununuzi wa vifaa na huduma mbalimbali. Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na karatasi za kura, masanduku ya kupigia kura, vituturi, majalada ya nukta nundu, wino usiofutika, shajala, fomu mbalimbali, fulana, kofia na mabango mbalimbali ya uchaguzi. Kwa kuzingatia

Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura ya 410, baadhi ya zabuni zilitolewa moja kwa moja kwenye taasisi za umma zikiwemo Mpigachapa Mkuu wa Serikali, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini, Shirika la Posta na Bohari Kuu ya Madawa (MSD).

### 3.4.2 Kugawa na Kusambaza Vifaa vya Uchaguzi

Tume inao wajibu wa kugawa na kusambaza vifaa vya uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi na kutoa maelekezo ya matumizi, usambazaji na uhifadhi wa vifaa husika. Vifaa hivyo vilipelekwa katika kila halmashauri kwa Tanzania Bara na kila wilaya kwa Tanzania Zanzibar kwa wakati na kwa idadi iliyohitajika na kisha kusambazwa kwenye vituo vya kupigia kura.




*Wajumbe wa Kamati ya Ununuzi, Usambazaji na Lojistiki ya Vifaa inayojumuisha vyama vya siasa wakikagua karatasi za kura, katika maghala ya Tume yaliyopo Dar es Salaam.*

### 3.5 Mifumo ya Menejimenti ya Uchaguzi

Kwa kutumia wataalam wa ndani, Tume ilisanifu na kujenga Mifumo ya Menejimenti ya Uchaguzi (Election Management Systems) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali wakati wa uchaguzi. Mifumo hiyo ni: -

(i) Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea (Candidates Management System - CMS). Mfumo huu ulitumika kusajili, kuhifadhi na kusimamia taarifa za Wagombea wa Uchaguzi Mkuu kwa ngazi ya Rais, Ubunge na Udiwani;

(ii) Mfumo wa Matokeo (Results Management System - RMS). Ni Mfumo uliotumika kuingiza, kuhifadhi na kusimamia taarifa za matokeo ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani;

(iii) Mfumo wa Uhakiki wa Taarifa za Wapiga Kura (Voters Interaction System - VIS). Mfumo huu uliwapa fursa wapiga kura walioandikishwa kuona na kuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari. Pia, mfumo huu ulitumika kuwawezesha wapiga kura kutambua vituo vya kupigia kura kipindi cha uchaguzi;

(iv) Mfumo wa Watazamaji wa Uchaguzi (Observers Management System - OMS). Mfumo huu ulitumika kusajili, kuhifadhi na kusimamia taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi wa Ndani na Nje (Local and International Observers); na

(v) Mfumo wa taarifa za kijiografia (Geographical Information System - GIS). Mfumo huu ulitumika kuandaa taarifa za kijiografia za uchaguzi na kuonesha matokeo katika ramani wakati wa kutangaza matokeo.

### 3.6 Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

Tume ilipanga ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kuzingatia masharti ya uteuzi yaliyomo katika kifungu cha 37(1) (a) cha Sheria ya Taifa Uchaguzi, Sura ya 343. Kwa mujibu wa kifungu tajwa, Tume inatakiwa kupanga siku ya uteuzi kuwa si chini ya siku tano na si zaidi ya siku 25 baada ya kuvunjwa kwa Bunge. Kwa kuzingatia masharti hayo na tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge ambayo ilikuwa tarehe 31 Julai, 2020, Tume iliandaa na kutangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na.11: Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020**

| Na. | Shughuli | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. | Uteuzi wa wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani | Tarehe 25 Agosti, 2020 |
| 2. | Kampeni za uchaguzi | Tarehe 26 Agosti, 2020 hadi 27 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Bara; na Tarehe 26 Agosti, 2020 hadi 26 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Zanzibar |
| 3. | Siku ya kupiga kura | Tarehe 28 Oktoba, 2020 (siku ya Jumatano) |

Ratiba ya uchaguzi ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na. 532 la tarehe 17 Julai, 2020. Ratiba hiyo ilitangazwa pia katika vyombo vya habari ili kuwawezesha wadau wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla kujua ratiba kamili na siku ya uchaguzi.




*Mwenyekiti wa Tume Mhe. Jaji wa Rufaa Mst. Semistocles S. Kaijage (kushoto) na Mkurugenzi wa Uchaguzi Dkt. Wilson M. Charles (kulia) wakati wa kutangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam.*

### 3.7 Watendaji wa Uchaguzi

Tume ina sekretarieti yenye watumishi wa kudumu ambao hutekeleza majukumu ya kila siku ya taasisi. Vilevile, Sheria za uchaguzi zimeipa mamlaka ya kuteua watendaji wa uchaguzi katika kila mkoa, jimbo, kata na vituo. Watendaji hao huteuliwa kwa ajili ya kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi katika maeneo yao.

#### 3.7.1 Watumishi wa Tume

Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, sekretarieti ya Tume ilikuwa na jumla ya watumishi 191 wa kudumu wa kada mbalimbali. Aidha, watumishi 76 walihamishiwa kwa muda kutoka katika Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu ya uchaguzi.

#### 3.7.2 Uteuzi wa Watendaji wa Uchaguzi Ngazi ya Mkoa, Jimbo na Kata

Kwa madhumuni ya kusimamia, kuratibu na kuendesha zoezi la uchaguzi na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7 na 8 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 9 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ilifanya uteuzi wa waratibu wa uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na kata. Aidha, Tume iliwatumia maafisa uchaguzi, maafisa ugavi, wahasibu na maafisa TEHAMA wa halmashauri katika kufanikisha shughuli za uchaguzi. Idadi ya watendaji hao ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Tanzania Bara**

| Na. | Aina ya Watendaji | Eneo | Idadi ya watendaji kwa kila eneo | Jumla ya Maeneo | Jumla ya Watendaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa | Mkoa | 1 | 26 | 26 |
| 2. | Wasimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| 3. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo | Jimbo | 3 | 214 | 642 |
| 4. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata | Kata | 2 | 3,956 | 7,912 |
| 5. | Maafisa Uchaguzi | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| 6. | Maafisa TEHAMA | Halmashauri | 2 | 184 | 368 |
| 7. | Maafisa Ugavi | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| 8. | Wahasibu | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| **Jumla** | | | | | **9,684** |

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, watendaji 113 waliteuliwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 13.

**Jedwali Na. 13: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi kwa Tanzania Zanzibar**

| Na. | Aina ya Watendaji | Eneo | Idadi ya watendaji kwa kila Eneo | Jumla ya maeneo | Jumla ya Watendaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Waratibu wa Uchaguzi | Kisiwa | 1 | 2 | 2 |
| 2. | Wasimamizi wa Uchaguzi | Wilaya | 1 | 11 | 11 |
| 3. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo | Jimbo | 2 | 50 | 100 |
| **Jumla** | | | | | **113** |

### 3.7.3 Watendaji wa Vituo

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 57(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na maelekezo ya Tume, wasimamizi wa uchaguzi waliteua watendaji wa vituo ambao ni wasimamizi wa vituo, wasimamizi wasaidizi wa vituo wawili na makarani waongozaji wapiga kura mmoja kwa kila kituo. Vilevile, siku ya uchaguzi kila kituo cha kupigia kura

kilikuwa na mlinzi mmoja wa kituo. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kulikuwa na jumla ya watendaji wa vituo 407,835 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na. 14: Idadi ya Watendaji wa Vituo**

| Na. | Aina ya Watendaji | Idadi kwa Kila Kituo | Jumla ya Vituo | Jumla ya Watendaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wasimamizi wa Vituo | 1 | 81,567 | 81,567 |
| 2. | Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo | 2 | 81,567 | 163,134 |
| 3. | Makarani Waongozaji Wapiga Kura | 1 | 81,567 | 81,567 |
| 4. | Walinzi wa Vituo | 1 | 81,567 | 81,567 |
| **Jumla** | | | | **407,835** |

### 3.8 Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi

Tume iliratibu na kuendesha mafunzo kwa watendaji mbalimbali wa uchaguzi mara baada ya kuwateua. Jukumu hilo lilitekelezwa kwa mujibu wa kanuni ya 17(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 15(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020. Lengo la mafunzo ya watendaji lilikuwa kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume.

Katika kuhakikisha kuwa mafunzo yanatolewa kwa ufanisi, njia mbalimbali za uwasilishaji wa mada zilitumika. Njia hizo ni pamoja na mafunzo kwa nadharia na vitendo, majadiliano na kuonesha video fupi (*video clips*). Idadi ya watendaji waliopatiwa mafunzo katika ngazi ya mkoa, jimbo na kata ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 15.

**Jedwali Na. 15: Idadi ya Watendaji Waliopatiwa Mafunzo katika Ngazi ya Jimbo na Kata kwa Tanzania Bara**

| Na. | Aina ya Watendaji | Eneo | Idadi kwa kila Eneo | Jumla ya Maeneo | Jumla ya Watendaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa | Mkoa | 1 | 26 | 26 |
| 2. | Wasimamizi wa Uchaguzi wa majimbo | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| 3. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo | Jimbo | 3 | 214 | 642 |
| 4. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata | Kata | 2 | 3,956 | 7,912 |
| 5. | Maafisa Uchaguzi | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| 6. | Maafisa TEHAMA | Halmashauri | 2 | 184 | 368 |
| 7. | Maafisa Ugavi | Halmashauri | 1 | 184 | 184 |
| **Jumla** | | | | | **9,500** |

Watendaji wa vituo waliopatiwa mafunzo kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 16.

**Jedwali Na. 16: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Waliopatiwa Mafunzo kwa Tanzania Zanzibar**

| Na. | Aina ya Watendaji | Eneo | Idadi ya watendaji kwa kila eneo | Jumla ya maeneo | Jumla ya Watendaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Waratibu wa Uchaguzi | Kisiwa | 1 | 2 | 2 |
| 2. | Wasimamizi wa Uchaguzi | Wilaya | 1 | 11 | 11 |
| 3. | Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo | Jimbo | 2 | 50 | 100 |
| **Jumla** | | | | | **113** |

Watendaji wa vituo waliopatiwa mafunzo ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 17.

**Jedwali Na. 17: Watendaji wa Vituo Waliopatiwa Mafunzo**

| Na. | Aina ya Watendaji | Idadi kwa kila eneo | Jumla ya maeneo | Jumla ya watendaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wasimamizi wa Vituo | 1 | 81,567 | 81,567 |
| 2. | Wasimamizi wa Vituo wa Akiba wawili kwa kila Kata | 2 | 3,956 | 7,912 |
| 3. | Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo | 2 | 81,567 | 163,134 |
| 4. | Makarani Waongozaji Wapiga Kura | 1 | 81,567 | 81,567 |
| 5. | Makarani Waongozaji wa Akiba wawili kila Kata | 2 | 3,956 | 7,912 |
| **Jumla** | | | | **342,092** |

### 3.8.1 Mada za Mafunzo

Tume iliandaa mada 12 ambazo zilitumika katika kutoa mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi ngazi ya mkoa, jimbo na kata. Mada hizo ni: -

(i) Wajibu, majukumu na mambo muhimu ya kuzingatiwa na Waratibu wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi;

(ii) Uteuzi wa wagombea;

(iii) Maadili na kampeni za uchaguzi;

(iv) Wajibu na majukumu ya watendaji wa vituo vya kupigia kura na mawakala wa vyama vya siasa;

(v) Taratibu za kupiga kura;

(vi) Taratibu za kuhesabu kura kituoni;

(vii) Taratibu za kujumlisha kura na kutangaza matokeo;

(viii) Fomu za Uchaguzi;

(ix) Mifumo ya uchaguzi;

(x) Mapokezi, uhifadhi na usambazaji wa vifaa vya uchaguzi;

(xi) Mapokezi na matumizi ya fedha za uchaguzi; na

(xii) Wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa katika mchakato wa uchaguzi.

Vilevile, Tume iliandaa mada saba za mafunzo kwa wasimamizi wa vituo, wasimamizi wasaidizi wa vituo na makarani waongozaji wapiga kura kama ifuatavyo: -

(i) Wajibu na majukumu ya wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo;

(ii) Wajibu na majukumu ya makarani waongozaji wapiga kura;

(iii) Taratibu za kupiga kura;

(iv) Fomu zinazotumika wakati wa kupiga kura;

(v) Taratibu za kuhesabu kura kituoni;

(vi) Fomu za uchaguzi; na

(vii) Mambo muhimu ya kuzingatiwa na watendaji wa vituo wakati wa uchaguzi.

# SURA YA NNE

# UTEUZI WA WAGOMBEA, KAMPENI NA MAADILI YA UCHAGUZI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza tarehe 25 Agosti, 2020 kuwa siku ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wagombea waliopendekezwa na vyama vyao vya siasa kugombea kiti cha Rais walitakiwa kujaza na kuwasilisha fomu za uteuzi katika Ofisi za Tume Makao Makuu. Aidha, wagombea Ubunge waliwasilisha fomu za uteuzi katika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo na wagombea Udiwani kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Fomu za uteuzi za wagombea wote ziliwasilishwa siku ya uteuzi kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni.

Kampeni za uchaguzi zilifanyika siku moja baada ya uteuzi hadi siku moja kabla ya upigaji kura kwa upande wa Tanzania Bara na siku mbili Tanzania Zanzibar. Wakati wote wa kampeni wagombea walitakiwa kuzingatia sheria, kanuni za uchaguzi, Maadili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 na ratiba za kampeni.

## 4.1 Uteuzi wa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Fomu za uteuzi wa wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais (Fomu Na. 8A na Fomu Na. 10) zilitolewa katika ofisi za Tume Dodoma kuanzia tarehe 05 hadi 25 Agosti, 2020. Vyama vya siasa 17 kati ya vyama 19 vyenye usajili wa kudumu vilipendekeza na kuwadhamini wagombea katika nafasi hiyo. Vyama hivyo ni AAFP, ACT-Wazalendo, ADA – TADEA, ADC, CCK, CCM, CHADEMA, CHAUMMA, CUF, MAKINI, DP, NCCR-Mageuzi, NLD, NRA, SAU, UMD na UPDP.



AAFP




ACT-Wazalendo



ADA - TADEA



ADC



CCK



CCM




CHADEMA



CHAUMMA



CUF



MAKINI



DP



NCCR - Mageuzi



NLD




NRA



SAU




UMD




UPDP

*Mwenyekiti wa Tume Jaji wa Rufaa Mst. Semistocles S. Kaijage akikabidhi fomu za uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Tume ilitoa fursa kwa wagombea wote waliochukua fomu za uteuzi kuziwasilisha siku tatu kabla ya siku ya uteuzi kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ajili ya kukaguliwa na kuona kama zimekidhi masharti ya kisheria. Wagombea wote waliochukua fomu waliwasilisha fomu zao na zilikaguliwa na Tume kuanzia tarehe 22 hadi 24 Agosti, 2020. Wagombea ambao fomu zao zilikuwa na kasoro walielekezwa na Tume kuzirekebisha.

Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ulifanyika tarehe 25 Agosti, 2020. Wagombea wa vyama 16 kati ya 17 waliochukua fomu walirejeresha fomu za uteuzi kwenye Ofisi za Tume Dodoma kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni kwa ajili ya uteuzi. Mgombea kutoka chama cha NLD hakurejesha fomu ya uteuzi.

Wagombea wa vyama 15 kati ya vyama 16 waliorejesha fomu za uteuzi waliteuliwa na Tume baada ya kukidhi masharti ya uteuzi. Wagombea hao ni kutoka vyama vya CCM, NRA, ADA-TADEA, SAU, MAKINI, NCCR-Mageuzi, CUF, DP, ACT- Wazalendo, ADC, UPDP, CHAUMMA, UMD, AAFP na CHADEMA. Mgombea wa CCK hakukidhi masharti ya uteuzi, hivyo hakuteuliwa.

Kati ya wagombea 15 wa kiti cha Rais walioteuliwa, wanawake walikuwa wawili sawa na asilimia 13 na wanaume 13 sawa na asilimia 87. Aidha, kati ya wagombea 15 wa kiti cha Makamu wa Rais, wanawake walikuwa watano sawa na asilimia 33 na wanaume 10 sawa na asilimia 67. Orodha ya wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais walioteuliwa ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.18.


**Jedwali Na. 18: Wagombea Walioteuliwa Kugombea Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais**

| Na. | Jina la Mgombea | Jinsi | Chama cha Siasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Dkt. Magufuli John Pombe Joseph | Me | CCM |
| | Samia Suluhu Hassan | Ke | |
| 2. | Mahona Leopold Lucas | Me | NRA |
| | Ali Khamis Hassan | Me | |
| 3. | Shibuda John Paul | Me | ADA-TADEA |
| | Hassan Kornely Kijogoo | Me | |
| 4. | Muttamwega Bhatt Mgaywa | Me | SAU |
| | Satia Mussa Bebwa | Ke | |
| 5. | Cesilia Augustino Mmanga | Ke | MAKINI |
| | Tabu Mussa Juma | Me | |
| 6. | Maganja Yeremia Kulwa | Me | NCCR-Mageuzi |
| | Ambar Khamis Haji | Me | |
| 7. | Lipumba Ibrahim Haruna | Me | CUF |
| | Hamida Abdalla Huweishil | Ke | |
| 8 | Philipo John Fungo | Me | DP |
| | Zaina Juma Hamisi | Ke | |
| 9. | Membe Bernard Kamillius | Me | ACT-Wazalendo |
| | Omar Fakih Hamad | Me | |
| 10. | Queen Cuthbert Sendiga | Ke | ADC |
| | Shoka Khamis Juma | Me | |
| 11. | Twalib Ibrahim Kadege | Me | UPDP |
| | Ramadhani Ali Abdallah | Me | |
| 12. | Rungwe Hashim Spunda | Me | CHAUMMA |
| | Mohammed Massoud Rashid | Me | |
| 13. | Mazrui Khalfan Mohammed | Me | UMD |
| | Mashavu Alawi Haji | Ke | |
| 14. | Seif Maalim Seif | Me | AAFP |
| | Rashidi M. Ligania Rai | Me | |
| 15. | Lissu Tundu Antiphas Mughwai | Me | CHADEMA |
| | Mwalimu Salum Mwalimu Juma | Me | |

Orodha ya wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais ambao hawakuteuliwa kutokana na kushindwa kurejesha fomu ya uteuzi au kutokidhi masharti ya kisheria inaoneshwa kwenye Jedwali Na. 19.

**Jedwali Na. 19: Wagombea ambao Hawakuteuliwa kwa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais**

| Na. | Jina la Mgombea | Chama | Sababu ya kutoteuliwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Maisha Mapya Mchunguzi<br>Ussi Nahoda Fumu | NLD | Hakurejesha Fomu ya Uteuzi. |
| 2. | David Daud Mwaijolele<br>Ndugu Ali Said Juma | CCK | Hakukidhi masharti ya kisheria ya uteuzi kwa kutolipa dhamana ya mgombea na kushindwa kutimiza idadi ya wadhamini wa mgombea inayotakiwa. |



CCM




NRA



ADA - TADEA



SAU



MAKINI



NCCR - Mageuzi



CUF



UPDP



ACT-Wazalendo



ADC



DP



CHAUMMA



UMD



AAFP



CHADEMA

*Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikipokea fomu za uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.*

### 4.2 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais

Tume ilibandika fomu za wagombea walioteuliwa kwa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais katika mbao za matangazo za Tume kwa mujibu wa kanuni ya 38 na 39(3) na (4) za Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020. Zoezi hili lilifanyika ili kutoa fursa kwa watu kuzikagua na wale wanaoruhusiwa kuweka pingamizi kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. Fomu hizo zilibandikwa kuanzia saa 10:00 jioni siku ya uteuzi hadi saa 10:00 jioni siku iliyofuatia.

Tume ilipokea pingamizi mbili kutoka kwa mgombea wa CHADEMA Ndg. Lissu Tundu Antiphas Mughwai dhidi ya Dkt. Magufuli John Pombe Joseph wa CCM na Lipumba Ibrahim Haruna wa CUF. Pingamizi hizo ni kama ifuatavyo: -

#### 4.2.1 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea wa CCM

Sababu ya pingamizi iliyotolewa dhidi ya mgombea wa CCM ni kwamba hakuambatisha picha kwenye fomu za uteuzi na hakurejesha fomu kwa mujibu wa masharti yaliyotajwa na sheria. Tume ilipitia fomu za uteuzi wa mgombea pamoja na utetezi wake na kujiridhisha kuwa mgombea aliambatisha picha na alirejesha fomu kwa mujibu wa sheria. Hivyo, katika uamuzi wake Tume ilikataa pingamizi hilo kwa kukosa msingi wa kisheria.

#### 4.2.2 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea wa CUF

Sababu ya pingamizi iliyotolewa dhidi ya mgombea wa CUF ni kwamba hakurejesha fomu kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria. Tume ilipitia fomu za uteuzi wa mgombea pamoja na utetezi wake na kujiridhisha kuwa mgombea alirejesha fomu kwa kuzingatia masharti ya sheria. Hivyo, katika uamuzi wake Tume ilikataa pingamizi hilo kwa kukosa msingi wa kisheria.

### 4.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi walitoa fomu za uteuzi kwa wagombea Ubunge waliopendekezwa na kudhaminiwa na vyama vyao vya siasa kuanzia tarehe 12 hadi 25 Agosti 2020. Tarehe 25 Agosti, 2020 ilikuwa ndio siku ya uteuzi ambapo jumla ya wagombea 1,257 waliteuliwa na wasimamizi wa uchaguzi kugombea Ubunge katika majimbo 264. Kati ya wagombea hao wanaume walikuwa 964 sawa na asilimia 77 na wanawake walikuwa ni 293 sawa na asilimia 23 kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 20.

**Jedwali Na.20: Wagombea Ubunge Walioteuliwa**

| Na. | Chama cha Siasa | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | |
| 1. | AAFP | 17 | 11 | 28 |
| 2. | ACT-Wazalendo | 135 | 21 | 156 |
| 3. | ADA-TADEA | 24 | 13 | 37 |
| 4. | ADC | 33 | 15 | 48 |
| 5. | CCK | 11 | 7 | 18 |
| 6. | CCM | 239 | 25 | 264 |
| 7. | CHADEMA | 153 | 58 | 211 |
| 8. | CHAUMMA | 22 | 6 | 28 |
| 9. | CUF | 116 | 38 | 154 |
| 10. | MAKINI | 33 | 11 | 44 |
| 11. | DP | 16 | 7 | 23 |
| 12. | NRA | 25 | 9 | 34 |
| 13. | NCCR-Mageuzi | 65 | 20 | 85 |
| 14. | NLD | 7 | 2 | 9 |
| 15. | SAU | 13 | 6 | 19 |
| 16. | TLP | 18 | 9 | 27 |
| 17. | UDP | 24 | 9 | 33 |
| 18. | UMD | 4 | 13 | 17 |
| 19. | UPDP | 9 | 13 | 22 |
| **Jumla** | | **964** | **293** | **1,257** |

### 4.4 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Wasimamizi wa uchaguzi walibandika fomu za wagombea walioteuliwa kugombea Ubunge katika mbao za matangazo kwenye ofisi za halmashauri kwa mujibu wa kanuni ya 30 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020. Zoezi hili lilifanyika ili kutoa fursa kwa watu kuzikagua na wale wanaoruhusiwa kuweka pingamizi kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. Fomu hizo zilibandikwa kuanzia saa 10:00 jioni siku ya uteuzi hadi saa 10:00 jioni siku iliyofuatia. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, jumla ya pingamizi 334 za Ubunge zilipokelewa na kufanyiwa uamuzi na wasimamizi wa uchaguzi kwenye maeneo yao. Wale ambao hawakuridhika na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo walitakiwa kukata rufaa kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndani ya saa 24 kwa mujibu wa sheria.

### 4.5 Rufaa za Wagombea Ubunge kwa Tume

Tume ilipokea, ilisikiliza na kutolea uamuzi jumla ya rufaa 165 za wagombea Ubunge. Kati ya hizo, rufaa 98 ziliomba kurejeshwa kwa wagombea na rufaa 67 ziliomba kuenguliwa kwa wagombea walioteuliwa.

Tume ilisikiliza na kutolea uamuzi rufaa hizo ambapo rufaa 67 kati ya rufaa 98 sawa na asilimia 68 zilizoomba wagombea kurejeshwa zilikubaliwa. Wagombea hao walirejeshwa katika orodha ya wagombea. Aidha, rufaa 31 sawa na asilimia 22 ya rufaa zilizoomba wagombea kurejeshwa zilikataliwa.

Kati ya rufaa 67 zilizowasilishwa Tume zikiomba kuondolewa kwa wagombea ambao walikuwa wameteuliwa katika majimbo ni rufaa tatu sawa na asilimia 4.5 zilizokubaliwa. Hivyo, wagombea hao waliondolewa katika orodha ya wagombea Ubunge. Rufaa 64 sawa na asilimia 95.5 zilikataliwa, na wagombea katika rufaa hizo waliendelea kubaki kwenye orodha ya wagombea. Mchanganuo wa rufaa za wagombea Ubunge kwa kila chama ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 21.

**Jedwali Na. 21: Rufaa za Wagombea Ubunge**

| Na. | Chama | Rufaa zilizoomba wagombea walioenguliwa kurejeshwa | | Rufaa zilizoomba wagombea walioteuliwa kuondolewa | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | zilizokubaliwa | zilizokataliwa | zilizokubaliwa | zilizokataliwa | |
| 1. | CHADEMA | 25 | 6 | 0 | 16 | 47 |
| 2. | CCM | 0 | 0 | 3 | 21 | 24 |
| 3. | CUF | 8 | 5 | 0 | 4 | 17 |
| 4. | ACT - WAZALENDO | 20 | 10 | 0 | 10 | 40 |
| 5. | NCCR - MAGEUZI | 6 | 5 | 0 | 4 | 15 |
| 6. | ADA -TADEA | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| 7. | NRA | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 8. | ADC | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| 9. | DP | 2 | 1 | 0 | 1 | 4 |
| 10. | SAU | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| 11. | CHAUMMA | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| 12. | AAFP | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| 13. | MAKINI | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| 14. | CCK | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| 15. | UDP | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **67** | **31** | **3** | **64** | **165** |

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mgombea ambaye hakuridhika na uamuzi wa Tume kuhusu rufaa iliyoamuliwa anayo haki ya kufungua kesi ya kupiga matokeo ya uchaguzi Mahakamani baada ya uchaguzi kukamilika.

### 4.6 Wagombea Ubunge Waliochaguliwa bila Kupingwa

Kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinaweka masharti kuwa, endapo mgombea aliyeteuliwa ni mmoja tu katika uchaguzi wa Ubunge, Tume itamtangaza kwenye Gazeti la Serikali kuwa amechaguliwa. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, wagombea Ubunge 28 walichaguliwa bila kupingwa kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 2.

### 4.7 Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata walitoa fomu za uteuzi kwa wagombea Udiwani waliopendekezwa na kudhaminiwa na vyama vya siasa kuanzia tarehe 12 hadi 25 Agosti 2020. Siku ya uteuzi ilikuwa tarehe 25 Agosti, 2020 na uteuzi ulifanyika katika kata 3,953 Tanzania Bara kati ya kata 3,956 zilizotangazwa na Tume. Kata 3 za Igombemkulu, Kanindo na Milambo zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua hazikufanya uteuzi kutokana changamoto za mipaka ya kiutawala. Jumla ya wagombea Udiwani 9,231 waliteuliwa katika kata hizo. Kati ya hao, 8,563 walikuwa wanaume sawa na asilimia 92.76 na 668 walikuwa wanawake sawa na asilimia 7.24. Mchanganuo wa idadi ya wagombea Udiwani walioteuliwa na vyama vyao vya siasa ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 22.

**Jedwali Na. 22: Wagombea Udiwani Walioteuliwa**

| Na. | Chama cha Siasa | Jinsi | | Idadi ya Wagombea |
|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | |
| 1. | AAFP | 12 | 7 | 19 |
| 2. | ACT-Wazalendo | 856 | 39 | 895 |
| 3. | ADA-TADEA | 15 | 6 | 21 |
| 4. | ADC | 24 | 5 | 29 |
| 5. | CCK | 17 | 16 | 33 |
| 6. | CCM | 3,689 | 264 | 3,953 |
| 7. | CHADEMA | 2,648 | 143 | 2,791 |
| 8. | CHAUMMA | 13 | 2 | 15 |
| 9. | CUF | 822 | 92 | 914 |
| 10. | MAKINI | 23 | 10 | 33 |
| 11. | DP | 22 | 7 | 29 |
| 12. | NRA | 20 | 4 | 24 |
| 13. | NCCR-Mageuzi | 268 | 28 | 296 |
| 14. | NLD | 2 | 1 | 3 |
| 15. | SAU | 20 | 15 | 35 |
| 16. | TLP | 48 | 11 | 59 |
| 17. | UDP | 36 | 3 | 39 |
| 18. | UMD | 10 | 7 | 17 |
| 19. | UPDP | 18 | 8 | 26 |
| **Jumla** | | **8,563** | **668** | **9,231** |

### 4.8 Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata walibandika fomu za wagombea walioteuliwa kugombea Udiwani katika mbao za matangazo kwenye ofisi za kata kwa mujibu wa kanuni ya 27 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020. Zoezi hilo lilifanyika ili kutoa fursa kwa watu kuzikagua na wale wanaoruhusiwa kuweka pingamizi kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. Fomu hizo zilibandikwa kuanzia saa 10:00 jioni siku ya uteuzi hadi saa 10:00 jioni siku iliyofuatia.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, jumla ya pingamizi 1,228 za Udiwani zilipokelewa na kuamuliwa na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Wale ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa walitakiwa kukata rufaa Tume ndani ya saa 24 kwa mujibu wa sheria.

### 4.9 Rufaa za Wagombea Udiwani

Tume ilipokea, ilisikiliza na kutolea uamuzi jumla ya rufaa 451 za wagombea Udiwani. Kati ya hizo, rufaa 389 ziliomba kurejeshwa kwa wagombea na rufaa 62 ziliomba kuondolewa kwa wagombea walioteuliwa.

Tume ilisikiliza na kutolea uamuzi rufaa hizo ambapo rufaa 235 kati ya rufaa 389 sawa na asilimia 60.41 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea zilikubaliwa. Aidha, rufaa 154 kati ya 389 sawa na asilimia 39.59 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea zilikataliwa. Vilevile, rufaa zote 62 ambazo warufani waliomba kuondolewa kwa wagombea zilikataliwa, hivyo wagombea hao waliendelea kubaki kwenye orodha ya wagombea. Rufaa za wagombea udiwani ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 23.

**Jedwali Na.23: Rufaa za Wagombea Udiwani**

| Na. | Chama | Rufaa za kuomba wagombea walioenguliwa warejeshwe | | Rufaa za kuomba wagombea walioteuliwa waondolewe | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Zilizokubaliwa | Zilizokataliwa | Zilizokubaliwa | Zilizokataliwa | |
| 1. | CHADEMA | 146 | 105 | 0 | 23 | 274 |
| 2. | CCM | 0 | 0 | 0 | 21 | 21 |
| 3. | CUF | 39 | 9 | 0 | 3 | 51 |
| 4. | ACT - Wazalendo | 29 | 26 | 0 | 11 | 66 |
| 5. | NCCR - Mageuzi | 11 | 7 | 0 | 4 | 22 |
| 6. | ADC | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 7. | CHAUMMA | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 8. | CCK | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 9. | UDP | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 10. | UMD | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 11. | TLP | 3 | 7 | 0 | 0 | 10 |
| **Jumla** | | **235** | **154** | **0** | **62** | **451** |

Kwa mujibu wa kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mgombea ambaye hakuridhika na uamuzi wa Tume kuhusu rufaa iliyoamuliwa anayo haki ya kufungua kesi ya kupiga matokeo ya uchaguzi Mahakamani baada ya uchaguzi kukamilika.

### 4.10 Wagombea Udiwani Waliochaguliwa Bila Kupingwa

Kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kinaweka masharti kuwa, endapo mgombea Udiwani aliyeteuliwa katika kata ni mmoja tu katika uchaguzi wa Udiwani, Tume itamtangaza kwenye Gazeti la Serikali kuwa amechaguliwa. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, wagombea Udiwani 882 walichaguliwa bila kupingwa kama inavyooneshwa kwenye tovuti ya Tume yaani *www.nec.go.tz*.

### 4.11 Malalamiko ya Wagombea

Tume ilipokea na kufanyia kazi jumla ya malalamiko 61 ya wagombea Ubunge, Udiwani na vyama vya siasa. Malalamiko yaliyowasilishwa yalihusiana na kutoridhika na mchakato wa uteuzi wa wagombea na uamuzi wa Tume kuhusu rufaa. Malalamiko hayo yalichambuliwa na kutolewa uamuzi ambao uliwasilishwa kwa wahusika kwa njia ya barua.

### 4.12 Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea

Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea (Candidates Management System-CMS) ulitumika katika kusajili, kuhifadhi taarifa za wagombea na kuandaa mfano wa karatasi za kura. Wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais walisajiliwa katika Ofisi za Tume Makao Makuu Dodoma na wagombea Ubunge na Udiwani walisajiliwa katika halmashauri husika.

### 4.13 Kampeni za Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 51(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, wagombea, mawakala pamoja na vyama vya siasa waliendesha kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyotangazwa. Kampeni zilianza tarehe 26 Agosti, 2020 hadi 27 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar kampeni zilimalizika tarehe 26 Oktoba, 2020 ili kupisha zoezi la upigaji wa kura ya mapema (*early voting*) ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar. Kampeni hizo zilifanyika kwa njia ya mikutano ya hadhara, nyumba kwa nyumba, mabango, matangazo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kwa kiwango kikubwa kampeni ziliendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni, maadili na taratibu zilizowekwa. Aidha, kamati za maadili zilishughulikia malalamiko yaliyojitokeza wakati wa kampeni.

### 4.13.1 Uratibu wa Kampeni za Uchaguzi wa Rais na Makamu wa Rais

Tume iliunda Kamati ya Uratibu wa Kampeni za wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais. Kila chama cha siasa kilichokuwa na mgombea katika uchaguzi wa Rais kilikuwa na mjumbe kwenye kamati hiyo.

Vyama vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi wa Rais viliwasilisha mapendekezo ya ratiba ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ajili ya kuratibiwa. Baada ya kupokea ratiba hizo, Mkurugenzi wa Uchaguzi tarehe 21 Agosti, 2020 aliitisha kikao na vyama hivyo na kukubaliana ratiba ya kampeni za wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais kwa nchi nzima. Nakala ya ratiba ya kampeni iliyopangwa ilipelekwa kwa Mkuu wa Mkoa na Inspekta Jenerali wa Polisi kwa ajili ya kutoa ulinzi katika mikutano ya wagombea na kwa vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi wa Rais. Nakala nyingine za ratiba zilipelekwa kwa waratibu wa uchaguzi wa mikoa na wasimamizi wa uchaguzi.

### 4.13.2 Uratibu wa Kampeni za Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani

Vyama vya siasa vilivyokuwa na wagombea Ubunge viliwasilisha mapendekezo ya ratiba za kampeni ya uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi. Aidha, wagombea Udiwani waliwasilisha mapendekezo ya ratiba za kampeni kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata waliunda kamati za uratibu wa kampeni ambazo zilikutana na kukubaliana kuhusu ratiba za kampeni kwenye maeneo yao.

Nakala za ratiba zilisambazwa kwa vyama vya siasa vilivyokuwa na wagombea Ubunge na Udiwani. Pia, zilipelekwa kwa Wakuu wa Wilaya na Makamanda wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kuratibu ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

## 4.14 Maadili na Gharama za Uchaguzi

Vyama vya siasa na wagombea walitakiwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278.

### 4.14.1 Maadili ya Uchaguzi, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na Serikali na vyama vya siasa iliandaa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020. Lengo la Maadili

ni kuweka usawa katika ushindani baina ya vyama vya siasa wakati wote wa kampeni za uchaguzi. Ili kusimamia utekelezaji wa maadili hayo ziliundwa kamati za maadili ya uchaguzi ngazi ya Kata, Jimbo, Taifa na Rufaa kama ifuatavyo: -

#### 4.14.1.1 Kamati ya Maadili ya Rufaa

Tume iliunda Kamati ya Maadili ya Rufaa. Mwenyekiti wa Tume ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa kamati hiyo. Wajumbe wa kamati hiyo walikuwa ni Mwenyekiti wa Tume, Makamu Mwenyekiti wa Tume, mjumbe mmoja kutoka katika kila chama cha siasa kilichoshiriki uchaguzi wa Rais na mjumbe mmoja kutoka Serikalini ambaye alikuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Katibu wa Kamati hiyo alikuwa mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Wakati wa uchaguzi Kamati ya rufaa ilipokea na kuamua rufaa moja.

#### 4.14.1.2 Kamati ya Maadili ya Kitaifa

Tume iliunda Kamati ya Maadili ya Kitaifa. Mjumbe mmoja wa Tume ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati. Wajumbe wengine wa kamati hiyo walikuwa ni mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kilichoshiriki uchaguzi wa Rais na mwakilishi wa Serikali aliyeteuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Katibu na Katibu Msaidizi wa Kamati hii walitoka katika Sekretarieti ya Tume. Wakati wa kampeni za uchaguzi kamati hii ilipokea na kuamua jumla ya malalamiko 12 ya ukiukwaji wa maadili na rufaa saba dhidi ya uamuzi wa kamati za maadili ngazi ya jimbo kama inavyooneshwa kwenye tovuti ya Tume yaani *www.nec.go.tz*.

#### 4.14.1.3 Kamati za Maadili Ngazi ya Jimbo

Wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo 264 waliunda Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Jimbo baada ya kupata maelekezo kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mwenyekiti wa kamati ya maadili ya uchaguzi ngazi ya jimbo alikuwa msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika. Wajumbe wengine walitoka katika kila chama cha siasa kilichokuwa na mgombea katika jimbo husika na mwakilishi mmoja kutoka Serikalini ambaye aliteuliwa na Katibu Tawala wa Wilaya husika. Aidha, msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo alikuwa katibu wa kamati hiyo.

#### 4.14.1.4 Kamati za Maadili Ngazi ya Kata

Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata waliunda Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Kata 3,953 baada ya kupata maelekezo kutoka Tume. Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Kata alikuwa msimamizi msaidizi wa uchaguzi wa kata husika. Wajumbe wengine walitoka katika kila chama cha siasa kilichokuwa na mgombea katika kata husika na mwakilishi mmoja kutoka Serikalini ambaye aliteuliwa na Katibu Tawala wa Wilaya husika. Aidha, mtumishi kutoka katika ofisi ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi alikuwa katibu wa kamati hiyo.

### 4.14.2 Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278

Sheria ya Gharama za Uchaguzi, pamoja na mambo mengine, imelenga kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika shughuli za uchaguzi. Utekelezaji wa Sheria hii husimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa. Sheria inahitaji uwepo wa uwazi wa vyanzo vya mapato, matumizi, michango pamoja na kuweka ukomo wa fedha zinazotumika katika uchaguzi, lengo likiwa ni kudhibiti vitendo vya rushwa ndani ya vyama vya siasa na uchaguzi kwa ujumla. Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza kumwekea pingamizi mgombea yeyote au chama cha siasa kilichokiuka Sheria ya Gharama za Uchaguzi kama ambavyo imeelezwa katika kifungu cha 20 cha Sheria hiyo. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume haikupokea pingamizi lolote kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

# SURA YA TANO

# KUPIGA NA KUHESABU KURA

Upigaji kura ni moja ya hatua muhimu katika mchakato wa uchaguzi. Tume ilifanya maandalizi yote muhimu katika kuhakikisha zoezi la upigaji kura linafanyika kwa mujibu wa sheria. Vifaa na watendaji wa vituo waliandaliwa wa kutosha kwa ajili ya kufanikisha zoezi hili.

## 5.1 Risala ya Mwenyekiti wa Tume kwa Wapiga Kura

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi siku moja kabla ya siku ya uchaguzi alisoma risala kupitia vyombo vya habari. Katika risala yake alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wanaowataka katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Pia, aliwakumbusha na kuwasisitiza wananchi kuhusu utaratibu wa kupiga kura husaf usan, muda wa kufungua na kufunga vituo vya kupigia kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi. Aidha, risala hiyo ilieleza mambo yanayopaswa na yasiyopaswa kufanywa na mpiga kura siku ya uchaguzi. Nakala ya risala ipo katika Kiambatisho Na. 3.

## 5.2 Siku ya Uchaguzi

Tume ilitangaza tarehe 28 Oktoba, 2020 kuwa siku ya uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara. Kwa kuwa tarehe hiyo ilikuwa ni siku ya kazi, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliitangaza kuwa siku ya mapumziko. Uchaguzi ulihusisha wapiga kura 29,754,699 na ulifanyika katika vituo vya kupigia kura 81,567.

Zoezi la kupiga kura lilianza saa 1:00 asubuhi na kukamilika saa 10:00 jioni. Vifaa vya uchaguzi katika kila kituo cha kupigia kura vilipelekwa mapema kwa idadi iliyohitajika, hali iliyowezesha upigaji kura kuanza kama ilivyopangwa. Aidha, kulikuwa na mabango katika kila kituo cha kupigia kura na katika njia za kuelekea vituoni kulikuwa na mabango mshale yaliyowasaidia wapiga kura kutambua kwa urahisi vilipo vituo vya kupigia kura.

### 5.3 Maelekezo ya Kisera Kuhusu Kupiga Kura

Tume ilitoa Maelekezo ya Kisera kwa mujibu wa kifungu cha 126 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Lengo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa kila raia mwenye sifa ya kupiga kura anapata fursa ya kutumia haki yake ya kikatiba. Maelekezo ya Kisera yalikuwa kama ifuatavyo: -

(i) Kwa mpiga kura asiye na picha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini ana kadi ya kupigia kura yenye taarifa binafsi sawa na taarifa zilizomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; aruhusiwe kupiga kura.

(ii) Kwa mpiga kura ambaye ana kadi yenye namba ya mpiga kura inayotofautiana na namba ya mpiga kura iliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ilihali taarifa nyingine zote ikiwemo picha ni sawa katika kadi na Daftari; aruhusiwe kupiga kura.

(iii) Mpiga kura ambaye ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini amepoteza kadi yake ama kadi yake imeharibika na taarifa zake zipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; aruhusiwe kupiga kura kwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:-

    (a) Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
    (b) Leseni ya udereva; au
    (c) Pasi ya kusafiria.

    Majina yaliyomo katika vitambulisho hivyo yafanane na majina yaliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

(iv) Kwa mpiga kura ambaye ana kadi ya kupigia kura lakini taarifa zake hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; asiruhusiwe kupiga kura;

(v) Katika Jimbo la Misungwi kulikuwa na mabadiliko ya jina la Kata ya Isesa ambayo sasa inaitwa Buhunda na baadhi ya vijiji vya kata hiyo kuhamishiwa kata ya jirani ya Ilujamate. Wapiga kura katika kata hizo mbili watapiga kura kama ifuatavyo: -

    (a) Wapiga kura wa vijiji vya Isesa na Mbalama watapiga kura katika Kata ya Ilujamate badala ya Kata ya Buhunda kupitia vituo walivyojiandikishia.

(b) Wapiga kura wa Kijiji cha Mwagimagi watapiga kura katika Kata ya Buhunda badala ya Kata ya Ilujamate kwenye vituo walivyojiandikishia.

(c) Kituo cha Shule ya Msingi Gukwa kilichokuwa katika kijiji cha Nyang'homango Kata ya Ilujamate kilihamishiwa katika Kijiji kipya cha Gukwa kilichopo katika Kata ya Buhunda. Hivyo, wapiga kura wa kituo hicho watapiga kura katika Kata ya Buhunda badala ya Kata ya Ilujamate.

### 5.4 Upigaji Kura

Vituo vya kupigia kura viliandaliwa katika namna ambayo iliwezesha zoezi la kupiga kura kufanyika kwa uwazi na wapiga kura kuchukua muda mfupi katika kupiga kura. Vyama vya siasa viliweka mawakala katika kila kituo kwa lengo la kushuhudia na kufuatilia hatua zote za upigaji kura kituoni.

Wapiga kura walijipanga katika mistari miwili yaani mstari wa wanawake na mstari wa wanaume ili kupunguza msongamano. Wakati wa kupiga kura kipaumbele kilitolewa kwa watu wenye ulemavu, wagonjwa, wazee, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga waliokuja nao vituoni.

Kwa watu wenye ulemavu wa macho (wasioona), Tume ili andaa majalada yenye maandishi ya nukta nundu ili kuwawezesha kupiga kura wenyewe. Wale ambao hawakuwa na uwezo wa kutumia majalada hayo, waliruhusiwa kwenda na watu wa kuwasaidia. Aidha, wapiga kura wasiojua kusoma na wasioweza kupiga kura wao wenyewe waliruhusiwa kwenda vituoni na watu wanaowaamini kwa ajili ya kuwasaidia kupiga kura.

### 5.5 Mawakala wa Upigaji Kura

Vyama vya siasa viliteua na kuwasilisha kwa wasimamizi wa uchaguzi orodha na utambulisho wa mawakala tarehe 21 Oktoba, 2020. Utambulisho wa mawakala ulizingatia kanuni za uchaguzi ambazo zinataka vyama vya siasa kuwasilisha barua ya utambulisho iliyoambatishwa na picha ya wakala, kama wakala hakuwa na picha aliruhusiwa kuambatisha nakala ya mojawapo ya vitambulisho ambavyo ni leseni ya udereva, kitambulisho cha taifa, pasi ya kusafiria au kadi ya mpiga kura. Mawakala waliotimiza masharti kwa mujibu wa sheria waliapishwa kuanzia tarehe 21 hadi 23 Oktoba, 2020. Msimamizi wa uchaguzi baada ya kuwaapisha mawakala aliandaa orodha na utambulisho wa mawakala ambayo aliwakabidhi wasimamizi wa vituo wakati wa kugawa vifaa. Orodha ya mawakala ilibandikwa katika vituo vya kupigia kura siku ya kupiga kura. Wasimamizi wa vituo waliwaruhusu mawakala waliopangwa na kutambulishwa katika vituo vya kupigia kura kuingia vituoni.

Mawakala walikuwa na wajibu wa kulinda maslahi ya wagombea na vyama vyao vya siasa katika vituo vya kupigia kura kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 57 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 58 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Mawakala hao waliruhusiwa kushuhudia mchakato wa upigaji kura na walipewa fursa ya kueleza kuhusu kuridhika au kutoridhika kwao na mwenendo wa upigaji kura kwa kujaza Fomu Na.14.

### 5.6 Usalama katika Vituo vya Kupigia Kura


Tume iliweka utaratibu uliohakikisha vituo vyote vya kupigia kura vinakuwa na ulinzi. Katika kutekeleza jukumu hilo, wasimamizi wa uchaguzi walishirikiana na Makamanda wa Polisi wa Wilaya kupata walinzi kwa ajili ya kulinda vituo vya kupigia kura. Siku ya kupiga kura kila kituo kilikuwa na mlinzi mmoja.

### 5.7 Kuhesabu Kura

Mara baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura, vituo vya kupigia kura vilitumika kwa ajili ya zoezi la kuhesabu kura. Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura walihesabu kura huku wakishuhudiwa na watu wanaoruhusiwa kisheria kuwepo wakati wa kuhesabu kura ikiwemo mawakala wa vyama vya siasa.

Kabla ya kuanza kuhesabu kura masanduku ya kura yalikaguliwa ili kuthibitisha kuwa lakiri hazijafunguliwa. Hatua hiyo ilifuatiwa na wasimamizi wa vituo kufungua sanduku moja baada ya lingine na kuhesabu kura zote zilizomo ndani ya sanduku, kura alizopata kila mgombea na kura zilizokataliwa au kuharibika. Utaratibu wa kuhesabu kura ulizingatia misingi ya uwazi na mawakala walijaza Fomu Na. 16 kuonesha kuridhika au kutoridhika katika kila hatua ya kuhesabu kura.

Wasimamizi wa vituo baada ya kuhesabu kura walijaza fomu za matokeo, Fomu Na. 21A kwa matokeo ya kiti cha Rais, Fomu Na. 21B kwa matokeo ya Ubunge na Fomu Na. 21C kwa matokeo ya Udiwani ambazo zilisainiwa na mawakala. Aidha, Wasimamizi wa vituo walibandika nakala za matokeo hayo nje ya kituo cha kupigia kura na nakala nyingine waliwapatia mawakala. Baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu kura vituoni fomu za matokeo na vifaa vilipelekwa kwa wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata kwa ajili ya majumuisho ya kura.




*Mpangilio wa kituo cha kupigia kura.*

# SURA YA SITA

# KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI

Zoezi la kujumlisha kura lilifanyika katika vituo vya kujumlishia kura vilivyoandaliwa katika kila jimbo na kata, mara baada ya masanduku ya kura na fomu za matokeo ya uchaguzi kutoka katika vituo vya kupigia kura kupokelewa. Kabla ya kuanza zoezi la kujumlisha kura, wasimamizi wa uchaguzi waliwapa taarifa ya muda na mahali zoezi la kujumlisha kura lilipofanyika wagombea na vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi.
Zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani lilifanyika kwa uwazi mbele ya watu wanaoruhusiwa kuwepo wakati wa kujumlisha kura, wakiwemo wagombea na mawakala wa vyama vya siasa.

## 6.1 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Rais

Wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo walianza zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Rais kwa kutangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo cha kupigia kura. Matokeo hayo yaliingizwa katika mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS) ambao uliwezesha kupatikana kwa jumla ya kura zote zilizopigwa na idadi ya kura alizopata kila mgombea wa kiti cha Rais katika jimbo husika. Baada ya kupatikana kwa idadi hiyo, wasimamizi wa uchaguzi walijaza matokeo hayo katika Fomu Na. 24A mbele ya mawakala. Wasimamizi wa uchaguzi pamoja na mawakala walisaini fomu hizo.

Nakala za fomu za matokeo ya uchaguzi wa Rais katika jimbo zilibandikwa katika mbao za matangazo nje ya vituo vya kujumlishia kura na nakala nyingine walipatiwa mawakala wa vyama vya siasa. Wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo walituma nakala ya fomu za matokeo Tume makao makuu kwa ajili ya kutangazwa na kujumuishwa na matokeo ya majimbo mengine.

Zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Rais lilifanywa na Tume katika kituo cha kujumlishia na kutangazia matokeo kilichokuwa Dar es Salaam katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (Julius Nyerere International Convention Center – JNICC).




*Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wakitangaza matokeo ya Uchaguzi wa Rais katika kituo cha kutangazia matokeo katika ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam.*

Matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais (*partial presidential election results*) kutoka katika majimbo yalianza kupokelewa kuanzia alfajiri ya tarehe 29 Oktoba, 2020 na yalihakikiwa na kutangazwa kadri yalivyokuwa yakipokelewa kutoka majimboni. Matokeo rasmi ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa tarehe 30 Oktoba, 2020 ndani ya saa 48 tangu kukamilika kwa zoezi la kupiga kura.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, idadi ya wapiga kura walioandikishwa ilikuwa 29,754,699, waliopiga kura katika uchaguzi wa Rais walikuwa 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 ya walioandikishwa. Kura halali zilikuwa 14,830,195 sawa na asilimia 98.27 ya waliopiga kura na kura zilizokataliwa zilikuwa 261,755. Wapiga kura ambao hawakujitokeza kupiga Kura walikuwa 14,662,749 sawa na asilimia 49.28 ya walioandikishwa. Matokeo ya kura alizopata kila mgombea wa kiti cha Rais yaliyotangazwa na Tume yameoneshwa katika Jedwali Na. 24.

**Jedwali Na.24: Matokeo ya Kura Alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais**

| Na. | Chama cha Siasa | Jina la Mgombea | Idadi ya Kura halali | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | Dkt. MAGUFULI John Pombe Joseph | 12,516,252 | 84.40 |
| 2. | NRA | MAHONA Leopold Lucas | 80,787 | 0.54 |
| 3. | ADA-TADEA | SHIBUDA John Paul | 33,086 | 0.22 |
| 4. | SAU | MUTTAMWEGA Bhatt Mgaywa | 14,922 | 0.10 |
| 5. | MAKINI | CECILIA Augustino Mmanga | 14,556 | 0.10 |
| 6. | NCCR - Mageuzi | MAGANJA Yeremia Kulwa | 19,969 | 0.13 |
| 7. | CUF | LIPUMBA Ibrahim Haruna | 72,885 | 0.49 |
| 8. | DP | PHILIPO John Fumbo | 8,283 | 0.06 |
| 9. | ACT-Wazalendo | MEMBE Bernard Kamillius | 81,129 | 0.55 |
| 10. | ADC | QUEEN Cuthbert Sendiga | 7,627 | 0.05 |
| 11. | UPDP | TWALIB Ibrahim Kadege | 6,194 | 0.04 |
| 12. | CHAUMMA | RUNGWE Hashim Spunda | 32,878 | 0.22 |
| 13. | UMD | MAZRUI Khalfani Mohamed | 3,721 | 0.03 |
| 14. | AAFP | SEIF Maalim Seif | 4,635 | 0.03 |
| 15. | CHADEMA | LISSU Tundu Antiphas Mughwai | 1,933,271 | 13.04 |
| **Jumla** | | | **14,830,195** | **100.00** |

Tume kwa mamlaka iliyonayo chini ya ibara ya 41(6) na 47(2) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 35F (8) na 35H vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ilimtangaza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi kuwa mshindi wa kiti cha Rais na aliyekuwa Mgombea mwenza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa mshindi wa kiti cha Makamu wa Rais kwa kupata kura 12,516,252 ambazo ni sawa na asilimia 84.40 ya kura zote halali zilizopigwa. Tume iliwakabidhi mshindi wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais hati ya kuchaguliwa tarehe 01 Novemba, 2020 katika ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyopo Njedengwa Jijini Dodoma.




*Hafla ya kukabidhi cheti cha ushindi kwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais.*


### 6.2 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge

Wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo walianza zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Wabunge kwa kutangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo cha kupigia kura. Matokeo hayo yaliingizwa katika Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS) ambao uliwezesha kupatikana kwa jumla ya kura zote zilizopigwa na idadi ya kura alizopata kila mgombea Ubunge katika jimbo husika. Baada ya kupatikana kwa idadi hiyo ya kura, wasimamizi wa uchaguzi walijaza matokeo hayo katika Fomu Na. 24B mbele ya mawakala.

Wasimamizi wa uchaguzi waliwatangaza washindi wa Ubunge katika majimbo husika na kubandika nakala za fomu za matokeo katika mbao za matangazo nje ya vituo vya kujumlishia kura. Mawakala na wagombea waliokuwepo wakati wa kujumlisha kura walipatiwa nakala za fomu za matokeo.

Matokeo ya jumla ya uchaguzi wa Wabunge yalionesha kwamba kati ya majimbo 264 chama cha ACT-Wazalendo kilishinda katika majimbo manne sawa na asilimia 1.51, CCM majimbo 256 sawa na asilimia 96.97, CHADEMA jimbo moja sawa na asilimia 0.38, CUF majimbo matatu sawa na asilimia 1.14. Orodha ya Wabunge walioshinda Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inapatikana kwenye tovuti ya Tume *www.nec.go.tz*. Asilimia ya matokeo hayo ni kama inavyooneshwa kwenye Chati Na.1.

**Chati Na. 1: Asilimia ya Viti vya Ubunge kwa kila Chama**



Mchanganuo wa matokeo hayo kwa jinsi unaonesha kuwa kati ya Wabunge 264 wa kuchaguliwa, 26 ni wanawake sawa na asilimia 9.85 na 238 ni wanaume sawa na asilimia 90.15. Idadi ya Wabunge waliochaguliwa kwa mchanganuo wa vyama vyao na jinsi umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 25.

**Jedwali Na. 25: Wabunge Waliochaguliwa**

| Na. | Jina la Chama | Jinsi | | Idadi ya Wabunge | Asilimia ya Viti vya Ubunge |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | | |
| 1. | ACT-Wazalendo | 4 | 0 | 4 | 1.51 |
| 2. | CCM | 233 | 23 | 256 | 96.97 |
| 3. | CHADEMA | 0 | 1 | 1 | 0.38 |
| 4. | CUF | 1 | 2 | 3 | 1.14 |
| **Jumla** | | **238** | **26** | **264** | **100.00** |
| **Asilimia kwa Jinsi** | | **90.15** | **9.85** | | |

### 6.3 Utaratibu wa Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani

Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata walianza zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Madiwani kwa kutangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo cha kupigia kura. Hesabu ya kura za Udiwani kutoka vituo vyote ndani ya kata zilijumlishwa ili kupata jumla ya kura zote zilizopigwa na idadi ya kura alizopata kila mgombea. Baada ya kupatikana kwa idadi hiyo ya kura, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata walijaza matokeo hayo katika Fomu Na. 24C mbele ya mawakala.

Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi waliwatangaza washindi wa nafasi za Udiwani katika kata husika na kubandika nakala za fomu za matokeo katika mbao za matangazo nje ya vituo vya kujumlishia kura. Mawakala na wagombea waliokuwepo wakati wa kujumlisha kura walipatiwa nakala za fomu za matokeo.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliahirisha uchaguzi katika kata 4 kati ya kata 3,953 zilizofanya uteuzi wa wagombea kutokana na vifo vya wagombea, kukosekana kwa karatasi za kura na vurugu siku ya uchaguzi. Kata ambazo uchaguzi uliahirishwa ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na. 26. Kata hizo zilifanya uchaguzi baadae.

**Jedwali Na. 26: Kata ambazo Uchaguzi Uliahirishwa**

| Na. | Halmashauri | Jimbo | Kata | Sababu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mji Kahama | Kahama Mjini | Nyahanga | Kifo cha Mgombea |
| 2. | Manispaa ya Iringa | Iringa Mjini | Igumbilo | Kifo cha Mgombea |
| 3. | Wilaya ya Moshi | Moshi Vijijini | Kibosho Kati | Kukosekana kwa Karatasi za Kura |
| 4. | Wilaya ya Tandahimba | Tandahimba | Miuta | Kuwepo kwa vurugu siku ya Uchaguzi |


Matokeo ya jumla ya uchaguzi wa Madiwani yalionesha kwamba kati ya kata 3,953 zilizo shiriki katika uchaguzi wa Madiwani, Chama cha ACT-Wazalendo kilipata Madiwani 22 sawa na asilimia 0.56, CCM Madiwani 3,820 sawa na asilimia 96.63, CHADEMA Madiwani 85 sawa na asilimia 2.15, CUF Madiwani 20 sawa na asilimia 0.51, DP Diwani mmoja sawa na asilimia 0.02 na NCCR-Mageuzi Madiwani watano sawa na asilimia 0.13 kama inavyoonekana katika Jedwali Na.27.

**Jedwali Na. 27: Madiwani Waliochaguliwa**

| Na. | Jina la Chama | Jinsi | | Idadi ya Madiwani | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | | |
| 1. | ACT-Wazalendo | 22 | 0 | 22 | 0.56 |
| 2. | CCM | 3,562 | 258 | 3,820 | 96.63 |
| 3. | CHADEMA | 85 | 0 | 85 | 2.15 |
| 4. | CUF | 18 | 2 | 20 | 0.51 |
| 5. | DP | 1 | 0 | 1 | 0.02 |
| 6. | NCCR-Mageuzi | 5 | 0 | 5 | 0.13 |
| **Jumla** | | **3,693** | **260** | **3,953** | **100** |

Idadi ya Madiwani Wanawake wa kuchaguliwa ni 260 kati ya madiwani 3,953 sawa na asilimia 6.58 na Madiwani Wanaume 3,693 sawa na asilimia 93.42. Idadi ya viti vya Udiwani kwa jinsi kwa asilimia ni kama inavyooneshwa kwenye Chati Na.2.

**Chati Na.2: Asilimia ya Madiwani wa Kuchaguliwa kwa Jinsi**




## 6.4 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum

Tume, kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ina jukumu la kuteua na kutangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Kwa mujibu ibara ya 66(1)(b) ya Katiba, idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum inatakiwa isipungue asilimia 30 ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Mwaka 2010 idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum iliongezwa kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 40 ya Wabunge wote.

Kwa upande wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika mabaraza ya halmashauri, idadi yao inatakiwa isipungue theluthi moja (1/3) ya madiwani wa kuchaguliwa katika kata zilizopo kwenye halmashauri husika. Masharti haya yameainishwa chini ya kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kifungu cha 35(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, pamoja na kifungu cha 19 (1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

### 6.4.1 Uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum

Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum, inapatikana kwa kuzingatia jumla ya Wabunge wa aina zote kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Idadi na aina za Wabunge zinazotumika kukokotoa idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 28.

**Jedwali Na. 28: Aina za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano**

| Na. | Aina ya Wabunge | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Wabunge wa kuchaguliwa majimboni | 264 |
| 2. | Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi | 5 |
| 3. | Wabunge wa kuteuliwa na Rais | 10 |
| 4. | Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1 |
| 5. | Spika, iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge | 1 |
| | **Jumla** | **281** |

Kanuni ya kupata idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ni kama ifuatavyo: -

*Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum*

*= Idadi ya Wabunge wote x 40%*
*= 281x 40/100*
*= 112.4 ≈113*

Kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ilikuwa 113 na iligawanywa kwa vyama vilivyopata asilimia tano (5%) au zaidi ya kura zote halali za Ubunge kama ilivyoainishwa katika ibara ya 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi mkuu na kupata angalau asilimia tano (5%) ya kura zote halali za Wabunge vilipendekeza kwa Tume majina ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kura halali za Wabunge zilikuwa ni 14,014,362 kwa madhumuni ya ukokotoaji wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Jinsi ya kupata asilimia tano (5%) ya kura zote halali za Ubunge ni kama ifuatavyo: -

*Asilimia tano (5%) = idadi ya kura zote halali za ubunge x 5/100*

*= 14,014,362 x 5/100*
*= 700,718*

Kila chama cha siasa kilichoshiriki uchaguzi wa Ubunge na kupata angalau asilimia tano (5%) ya kura halali za Ubunge kilistahili kupata Viti Maalum. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 asilimia tano ya kura halali za Ubunge ilikuwa 700,718.

Kwa mujibu wa ibara ya 78(2) (a) ya Katiba, endapo Mbunge atachaguliwa bila kupingwa, kura za Mgombea wa kiti cha Rais wa chama husika zitahesabiwa kuwa ni kura halali za Mbunge aliyechaguliwa bila kupingwa katika jimbo husika.

Baada ya kukokotoa asilimia ya kura ambazo kila chama kilipata katika uchaguzi wa Wabunge, vyama viwili tu ndivyo vilivyopata angalau asilimia tano (5%) ya kura zote halali za Ubunge. Vyama hivyo ni CCM kilichopata kura 10,945,322 sawa na asilimia 78.1 na CHADEMA kilichopata kura 2,204,493 sawa na asilimia 15.7. Vyama hivyo ndivyo vilistahili kupata mgawanyo wa viti maalum 113 vya Ubunge kwa kuzingatia uwiano wa kura halali ambazo kila chama kilipata. Kanuni iliyotumika kugawa viti hivyo ni kama ifuatavyo: -

$$\text{Idadi ya viti maalum kwa chama} = \frac{\text{Kura zote halali za ubunge kwa chama husika X jumla ya viti maalum}}{\text{Jumla ya kura halali za ubunge kwa vyama vilivyopata angalau asilimia tano}}$$

Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa vyama vilivyokidhi masharti ya Ibara 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 29 na orodha ya Wabunge hao imeoneshwa kwenye Kiambatisho Na.4.

**Jedwali Na. 29: Mgawanyo wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya Kura Halali | Idadi ya Viti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | 10,945,322 | 94 | 83.2 |
| 2. | CHADEMA | 2,204,493 | 19 | 16.8 |
| **Jumla** | | **13,149,815** | **113** | **100** |

Baada ya uchaguzi mkuu kukamilika na kufanyika kwa uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum na Wabunge wengine wanaoteuliwa na mamlaka zingine, Bunge la Jamhuri ya Muungano litakuwa na idadi ya Wabunge 393. Kati ya hao, Wabunge wanawake ni 146 sawa na asilimia 37.2 na Wabunge wanaume ni 247 sawa na asilimia 62.8. Mchanganuo wa wabunge ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 30.

**Jedwali Na. 30: Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano**

| Na. | Aina ya Wabunge | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | |
| 1. | Wabunge wa kuchaguliwa majimboni | 238 | 26 | 264 |
| 2. | Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi | 3 | 2 | 5 |
| 3. | Wabunge wa kuteuliwa na Rais | 5 | 5 | 10 |
| 4. | Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1 | 0 | 1 |
| 5. | Wabunge Wanawake wa Viti Maalum | - | 113 | 113 |
| **Jumla** | | **247** | **146** | **393** |
| **Asilimia** | | **62.8** | **37.2** | **100** |

### 6.4.2 Uteuzi wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum

Tume ilikokotoa idadi ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum ambayo ni theluthi moja (1/3) ya madiwani wa kuchaguliwa katika halmashauri na Wabunge wa majimbo kwenye halmashauri husika kama ifuatavyo:-

$$\textit{Jumla ya viti maalum katika halmashauri} = \frac{\textit{Idadi ya kata katika halmashauri} + \textit{Idadi ya Wabunge wa majimbo ndani ya halmashauri}}{3}$$

Tume iligawanya viti maalum kwa kila halmashauri kwa kuzingatia idadi ya kata katika halmashauri husika. Viti maalum vilivyopatikana kwa kila halmashauri viligawanywa kwa vyama vilivyoshinda uchaguzi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Kanuni inayotumika kupata idadi ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa kila chama katika halmashauri ni: -

*Idadi ya Madiwani Wanawake Viti Maalum kwa chama =*

$$\frac{\textit{Idadi ya kata ambazo chama kimeshinda + Idadi ya Wabunge wa majimbo wa chama husika ndani ya halmashauri}}{3}$$

Tume baada ya kufanya ukokotoaji kwa mujibu wa Sheria, jumla ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum ni 1,374 kwa halmashauri zote. Mgawanyo wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa kila chama kilichokidhi masharti ya kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 31.

**Jedwali Na. 31: Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya Viti | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | ACT- Wazalendo | 5 | 0.36 |
| 2. | CCM | 1,339 | 97.45 |
| 3. | CHADEMA | 25 | 1.82 |
| 4. | CUF | 4 | 0.30 |
| 5. | NCCR-Mageuzi | 1 | 0.07 |
| **Jumla** | | **1,374** | **100.00** |

### 6.5 Kesi za Kupinga Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani

Sheria za uchaguzi zinatoa haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa Ubunge na Udiwani kwa kufungua kesi Mahakamani baada ya matokeo hayo kutangazwa. Kifungu cha 111 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 110 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 vinataja watu ambao wanaruhusiwa kupinga matokeo ya uchaguzi Mahakamani kuwa ni: -

(i) mtu ambaye alipiga kura au alikuwa ana haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaolalamikiwa;

(ii) mtu ambaye alikuwa na haki ya kuteuliwa kuwa mgombea au kuchaguliwa katika

uchaguzi huo;

(iii) mtu ambaye alikuwa mgombea katika uchaguzi huo; au

(iv) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, jumla ya kesi 15 za kupinga matokeo ya uchaguzi wa Wabunge na Madiwani zilifunguliwa. Kati ya hizo, kesi nne zilifunguliwa kupinga matokeo ya Ubunge na kesi 11 za kupinga matokeo ya Udiwani. Orodha ya kesi zilizofunguliwa inaoneshwa kwenye Jedwali Na. 32.

**Jedwali Na. 32: Kesi za Kupinga Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani**

| Na. | Kesi | Mahakama | Jimbo/Kata |
|---|---|---|---|
| | **Kesi za Ubunge** | | |
| 1. | Mbarak Daud Mbarak (ACT -Wazalendo) vs AG na wenzake, Kesi Na. 67/2020 | Mahakama Kuu ya Zanzibar | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 2. | Halima Ibrahim Mohamed (ACT -Wazalendo) vs AG na wenzake, Kesi Na. 68/2020 | Mahakama Kuu ya Zanzibar | Jimbo la Malindi |
| 3. | Faki Haji Makame (ACT -Wazalendo) vs AG na wenzake, Kesi Na. 69/2020 | Mahakama Kuu ya Zanzibar | Jimbo la Bububu |
| 4. | Boniface Anyisile Mwabukusi (NCCR-Mageuzi) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama Kuu Mbeya | Jimbo la Busokelo |
| | **Kesi za Udiwani** | | |
| 1. | Swabiru Musa Basenga (CCM) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Kigoma | Kata ya Itebura |
| 2. | Bonaventure N. Kinyuko (CCM) vs AG na wenzake, Kesi Na. 69/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Kasulu | Kata ya Bunyegera |
| 3. | Japhari Rashid Kitanda (CUF) vs AG na wenzake, Kesi Na. 69/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Tunduru | Kata ya Misechela |
| 4. | Andrea Chizuwa Ngoligo (ACT-Wazalendo) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma | Kata ya Chahwa |
| 5. | Tito Isack Matonya (CHADEMA) vs AG na wenzake, Kesi Na. 2/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma | Kata ya Majeleko |

| Na. | Kesi | Mahakama | Jimbo/Kata |
|---|---|---|---|
| 6. | Sebastian Antony Mbilingwa (CHADEMA) vs AG na wenzake, Kesi Na. 3/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma | Kata ya Mbabala |
| 7. | Geofrey Richard Chipungu (CHADEMA) vs AG na wenzake, Kesi Na. 4/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma | Kata ya Nzuguni |
| 8. | Mamba Meshack Zacharia (CCM) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma | Kata ya Bukura |
| 9. | Philipo Mhagama (ACT -Wazalendo) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Ruvuma | Kata ya Lilambo |
| 10. | Nyanguli Mtesigwa Philemon (CCM) vs AG na wenzake, Kesi Na. 2/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma | Kata ya Kibera |
| 11. | Emmanuel Gembe (CCM) vs AG na wenzake, Kesi Na. 1/2020 | Mahakama ya Hakimu Mkazi Tabora | Kata ya Imalamakoye |

Kwa mujibu wa kifungu cha 113 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 112 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume itaitisha na kuendesha upya uchaguzi katika jimbo au kata ambayo Mahakama itatengua matokeo ya uchaguzi unaolalamikiwa.

# SURA YA SABA

# ELIMU YA MPIGA KURA

Kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi au asasi zinazotoa elimu hiyo. Elimu ya mpiga kura hutolewa kwa wananchi wote kwa lengo la kuwawezesha kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za mchakato wa uchaguzi kuanzia hatua ya uboreshaji wa Daftari hadi upigaji kura wenyewe. Elimu hiyo hulenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba katika kujitokeza kujiandikisha kuwa wapiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka.

## 7.1 Mkakati wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura

Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliandaa Mkakati wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura katika kuhakikisha kuwa taarifa na elimu ya mpiga kura vinawafikia wananchi wengi zaidi. Mkakati huo ulihusisha maandalizi ya miongozo ya kutolea elimu ya mpiga kura na usimamizi wa vyombo vya habari vya umma. Halikadhalika, uliainisha njia za kuwezesha kutoa elimu ya mpiga kura katika kipindi cha mchakato wa uchaguzi mkuu.

Njia zilizoainishwa katika mkakati huo ni pamoja na kutumia vyombo vya habari, tovuti ya Tume, mitandao ya kijamii, ushirikishaji wa asasi za kiraia, kutumia gari la elimu ya mpiga kura la Tume, ushiriki katika matamasha na maonesho mbalimbali ya kitaifa, elimu ya mpiga kura katika shule za sekondari, mikutano ya wadau, elimu ya mpiga kura kwenye vyombo vya usafiri, sanaa na machapisho.

## 7.2 Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020

Tume iliandaa Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020 ambao uliwawezesha wadau wa uchaguzi kutoa elimu yenye ujumbe unaofanana kwa nchi nzima. Hii ilisaidia wananchi kuelewa mchakato wa uchaguzi. Wadau waliohusika kutoa elimu ya mpiga kura ni pamoja na taasisi na asasi za kiraia zilizopewa vibali vya kutoa elimu hiyo.

### 7.3 Mwongozo kwa Vyombo vya Habari vya Umma na Vyama vya Siasa katika Kutangaza Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

Tume kwa kushauriana na vyombo vya habari vya umma, wagombea na vyama vya siasa iliandaa Mwongozo kwa Vyombo vya Habari vya Umma kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Mwongozo huo, ulilenga kutoa fursa sawa kwa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa vyama vyote vya siasa kueleza ilani, sera za vyama vyao na kutangaza habari za mikutano ya kampeni kwa kutumia vyombo vya habari vya umma.

Tume iliunda Kamati ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya kuratibu matumizi ya vyombo vya habari vya umma wakati wa kampeni za uchaguzi. Kamati hiyo ilijumuisha wajumbe kutoka Tume, vyama vya siasa, vyombo vya habari vya umma na asasi za kiraia.

### 7.4 Njia Zilizotumika katika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Mkakati wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura uliainisha njia mbalimbali zilizotumika katika kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Njia hizo ni pamoja na: -

#### 7.4.1 Redio, Runinga na Magazeti

Wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu Tume ilishiriki kutoa elimu ya mpiga kura kupitia vipindi vya mazungumzo (*talk shows*), mahojiano (*interviews*) mubashara na yale ya kurekodi katika redio na runinga za kitaifa na za kijamii zinazopatikana katika wilaya na mikoa husika.


Wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari, jumla ya vipindi 221 viliendeshwa kupitia runinga, redio za kitaifa na kijamii. Pia, jumla ya vipindi 308 viliendeshwa wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu. Sambamba na hilo, makala na mashairi yanayohusu mchakato wa uchaguzi yaliandaliwa na kuchapishwa katika magazeti mbalimbali.




*Mkurugenzi wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura, Bi. Giveness Aswile (kushoto) akitoa elimu ya mpiga kura kupitia kipindi cha redio kilichorushwa mubashara kupitia redio Access FM Mbeya.*

### 7.4.2 Mitandao ya Kijamii

Tume kwa kutumia mitandao ya kijamii ya *Facebook, Instagram* na *Twitter* ilitoa taarifa muhimu kuhusiana na zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu, ili kuwafikia wapiga kura wanaotumia mitandao hiyo. Aidha, *NEC Online TV* kupitia *YouTube* na tovuti zilitumika kwa madhumuni hayo. Vilevile, Tume ilitumia mitandao hiyo kupata mrejesho kutoka kwa wapiga kura na wananchi kwa jumla katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Mitandao hiyo ilibeba taarifa muhimu, *infographics*, picha mnato na video zenye kuelezea umuhimu wa wananchi na wapiga kura kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kujitokeza siku ya kupiga kura.



*Mitandao ya kijamii ya Tume.*

### 7.4.3 Mikutano ya Wadau

Tume imeweka utaratibu wa kukutana na wadau wa uchaguzi kabla ya kuanza kwa mazoezi makubwa kama vile uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari, Tume ilifanya mikutano tisa na wadau wa uchaguzi ngazi ya Taifa kuanzia tarehe 13 hadi 20 Juni, 2019. Pia, wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu Tume ilifanya jumla ya mikutano saba na wadau. Wadau walioshiriki katika mikutano hiyo ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wawakilishi wa watu wenye ulemavu, wawakilishi wa vijana, wawakilishi wa wanawake, taasisi na asasi za kiraia na wahariri wa vyombo vya habari.

Tume ilifanya jumla ya mikutano 27 ya wadau wa uchaguzi katika ngazi ya mkoa wakati wa uboreshaji wa Daftari na mikutano 28 wakati wa uchaguzi mkuu. Lengo la mikutano hiyo lilikuwa ni kutoa taarifa kuhusu kuanza kwa mazoezi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uchaguzi mkuu. Pia lengo lingine la mikutano hiyo lilikuwa kupokea maoni ya wadau na kuwahamasisha kushiriki katika michakato hiyo.



*Picha ya juu, Mhe. Jaji Rufaa (Mst.) Semistocles S. Kaijage, Mwenyekiti wa Tume akiongea na wadau wa uchaguzi na picha za chini, Dkt. Wilson M. Charles, Mkurugenzi wa Uchaguzi akikabidhi vyama vya siasa nakala ya orodha ya wapiga kura.*

Tume ilialikwa na kushiriki kwenye mikutano na makongamano yaliyoandaliwa na wadau na kutumia fursa hiyo kutoa elimu ya mpiga kura kuhusu uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Makongamano ambayo Tume ilishiriki ni pamoja na kongamano la viongozi wa dini lililoandaliwa na Jukwaa la Kikristo Tanzania, Mahakama ya Tanzania, Centre for International Policy - Africa na Foundation for Civil Society.

Tume ilizifikia jamii za wawindaji na waokota matunda katika Kijiji cha Mongo wa Mono Bonde la Yaeda Chini kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ambacho ni makao makuu ya jamii ya Wahadzabe. Lengo lilikuwa ni kuielimisha na kuihamasisha jamii hiyo iweze kushiriki katika uchaguzi. Tume ilitumia njia ya kukutana nao ana kwa ana kutokana na ugumu wa kuifikia jamii hiyo kutokana na mfumo wao wa maisha.



*Afisa wa Tume Bi. Dorothea Mbogo akitoa elimu ya mpiga kura kwa jamii ya Wahadzabe katika kijiji cha Mongo wa Mono Bonde la Yaeda Chini kilichopo Wilaya ya Mbulu, Manyara.*

### 7.4.4 Maonesho Mbalimbali

Tume ilishiriki katika maadhimisho na maonesho mbalimbali wakati wa uboreshaji wa Daftari na wakati wa uchaguzi mkuu kwa lengo la kukutana na wadau wake ana kwa ana na kuwapa taarifa muhimu za mazoezi hayo. Maadhimisho na maonesho ambayo Tume ilishiriki ni haya yafuatayo: -

(i) Maonesho ya siku ya wakulima (Nane Nane) yaliyofanyika mkoani Simiyu kuanzia tarehe 31 Julai hadi 07 Agosti, 2019;

(ii) Maadhimisho ya wiki ya vijana na kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mkoani Simiyu tarehe 07 hadi 14 Oktoba, 2019.

(iii) Wiki ya Sheria iliyofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 31 Januari hadi 6 Februari, 2020; na

(iv) Maonesho ya siku ya wakulima (Nane Nane) yaliyofanyika katika mikoa ya Simiyu, Morogoro na Dodoma kuanzia tarehe 31 Julai hadi 8 Agosti, 2020.

Ushiriki katika maonesho na maadhimisho ulitoa fursa kwa Tume kuwaelimisha wadau wake kuhusiana na majukumu yake, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia masuala ya uchaguzi. Wadau hao walielimishwa namna vifaa vya uboreshaji wa Daftari kama vile *BVR Kits* na vifaa vya uchaguzi mathalani vituturi na masanduku ya kura yanavyotumika.



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya (wa pili kushoto) akizungumza na Afisa wa Tume Bi. Johari Mutani (kulia) alipotembelea banda la Tume kwenye maonesho ya Wakulima Nane Nane Dodoma, Agosti, 2020.*

### 7.4.5 Vyombo vya Usafiri na Vituo vya Mabasi

Tume ilitoa elimu ya mpiga kura katika magari ya abiria na iliandaa vibandiko (*stickers*) ambavyo vilibandikwa katika daladala zinazofanya safari katika baadhi ya miji na majiji nchini.




*Mojawapo ya gari la abiria likiwa na kibandiko chenye kauli mbiu ya zoezi la uboreshaji wa Daftari na taarifa muhimu ya nani anaweza kujiandikisha, lini na wapi.*

### 7.4.6 Gari la Elimu ya Mpiga Kura

Tume ilitoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia gari lake la elimu ya mpiga kura wakati wa uboreshaji wa Daftari katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Tume ilikodi magari ya matangazo kwa ajili ya kazi hiyo. Magari hayo yalipita katika maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu ambapo magulio na minada, masoko, vituo vya mabasi na shule mbalimbali za sekondari zilifikiwa. Wananchi walielimishwa kuhusu masuala ya uchaguzi na walipata fursa ya kutoa maoni na kuuliza maswali. Vilevile, magari hayo yalitumika kusambaza machapisho yenye kuelimisha kuhusu mchakato wa uchaguzi.









*Utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa kutumia gari la elimu ya mpiga kura.*

### 7.4.7 Njia za Asili

Katika kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kuhusiana na uboreshaji wa Daftari na mchakato wa uchaguzi, Tume ilitumia njia za asili zinazotumiwa na jamii husika ili kufikisha ujumbe kwa wananchi. Njia hizo ni pamoja na: -

(i) Kupiga Mbiu ya Mgambo ambayo ilihusisha kutoa matangazo mitaani, na kwenye maeneo yenye mikusanyiko. Aina hii ya mawasiliano ilitumika katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

(ii) Ngoma ambayo hupigwa alfajiri wakati watu wakijiandaa kwa ajili ya kwenda kwenye shughuli za kilimo ilitumika kutoa matangazo katika mikoa ya nyanda za juu kusini na kanda ya pwani.

(iii) Upatu ambao hutumiwa na masheha wa maeneo husika katika kutoa matangazo. Matangazo hayo yalitolewa wakati wa jioni au usiku, kwa lengo la kuwahimiza wapiga kura kujitokeza wakati wa uboreshaji wa Daftari na siku ya kupiga kura. Njia hii ilitumika zaidi Tanzania Zanzibar.

(iv) Njia ya kupiga *mhembe* (baragumu) katika mikoa ya kanda ya ziwa ilitumika wakati wa kutoa matangazo nyakati za alfajiri na jioni.

### 7.4.8 Elimu kwa Njia ya Sanaa

Tume ilitumia njia ya sanaa kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Baadhi ya kazi za sanaa zilizotumika ni michezo ya kuigiza iliyoandaliwa na Tume kwa kushirikiana na Research and Education for Democracy in Tanzania - REDET. Michezo hiyo ililenga kuonesha namna mchakato wa uboreshaji na ule wa uchaguzi unavyofanyika na jinsi wadau mbalimbali wanavyoshirikishwa.

Vilevile, ziliandaliwa *jingles* zenye ujumbe maalum wa kuhamasisha makundi maalum katika jamii, kama vile watu wenye ulemavu, wanawake na vijana kushiriki katika mchakato wa uboreshaji wa Daftari na ule wa uchaguzi mkuu. *Jingles* na michezo ya kuigiza iliyoandaliwa ilirushwa kupitia vipindi mbalimbali, kwa muda tofauti katika vituo vya runinga ambavyo ni Clouds Tv, TBC1 na Channel Ten. Tume pia, iliandaa matamasha ya muziki kwa lengo la kuburudisha na kupata nafasi ya kutoa elimu na hamasa ya uchaguzi.



*Mmojawapo wa wasanii wa kizazi kipya akiburudisha na kuhamasisha wananchi wakati wa Tamasha la Daftari, Dar es Salaam.*

Tume iliratibu utunzi na uandaaji wa nyimbo maalum zenye ujumbe mahsusi kuhusiana na zoezi la uboreshaji wa Daftari. Nyimbo hizo zilitungwa na kuimbwa na baadhi ya wasanii maarufu wa muziki wa kizazi kipya nchini kwa madhumuni ya kuelimisha na kuhamasisha wapiga kura.

### 7.4.9 Taasisi na Asasi za Kiraia

Tume ilitoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia 28 kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya asasi zilizopewa vibali, asasi 24 zilitoka Tanzania Bara na asasi nne zilitoka Tanzania Zanzibar.

Kwa upande wa uchaguzi mkuu, jumla ya asasi 252 zilipewa vibali kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura. Kati ya hizo, asasi 245 zilitoka Tanzania Bara na asasi saba Tanzania Zanzibar. Hata hivyo, asasi 107 tu ndizo zilizofanikiwa kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo mbalimbali nchini. Njia walizotumia kutoa elimu hiyo ni vipindi vya redio, runinga, mikusanyiko ya watu, semina na mitandao ya kijamii. Taasisi na asasi hizo zilitoa elimu hiyo kwa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura.

#### 7.4.10 Machapisho

Tume wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu iliandaa machapisho mbalimbali yakiwemo mabango taarifa, mabango mchakato kituoni na mabango ya uhamasishaji. Machapisho hayo yalisambazwa katika halmashauri na wilaya zote nchini kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura.

Vilevile, *billboards* zenye kuelimisha kuhusu utaratibu wa kupiga kura ziliandaliwa na kuwekwa katika njia kuu za majiji na miji nchini. Pia, *banners* zilizobeba kauli mbiu ya uchaguzi mkuu ziliandaliwa na kutumika katika mikutano ya Tume na wadau wake. Tume iliandaa na kugawa *tyre covers* zenye ujumbe unaoonesha tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na kauli mbiu isemayo **"KURA YAKO SAUTI YAKO NENDA UKAPIGE KURA"**.

#### 7.4.11 Kituo cha Huduma kwa Wateja

Tume ilifungua kituo cha huduma kwa wapiga kura (*call centre*) wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uchaguzi mkuu. Wapiga kura waliwezeshwa kupiga simu bila malipo kupitia namba 0800112100 na kupatiwa ufafanuzi kuhusiana na masuala mbalimbali ya uchaguzi.

#### 7.4.12 Uchaguzi wa Mfano *(Mock Election)*

Tume ilifanya zoezi la uchaguzi wa mfano tarehe 20 na 21 Oktoba, 2020 kwa waandishi wa habari. Zoezi hilo lilihusisha kuigiza mchakato wa upigaji kura katika kituo cha kupigia kura hadi kutangaza matokeo. Lengo lilikuwa ni kuwajengea waandishi wa habari uelewa kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi kituoni hadi kutangaza matokeo.

Waandishi wa habari 200 kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari walishiriki. Baada ya kufundishwa kwa nadharia, waandishi hao waliweza kufanya zoezi la uchaguzi wa mfano. Zoezi hilo liliwawezesha waandishi wa habari kufahamu mchakato wa uchaguzi kwa vitendo, hivyo kuwafanya kuwa mabalozi wazuri wa uchaguzi.




*Waandishi wa habari wakishiriki katika zoezi la uchaguzi wa mfano (mock election) tarehe 20 na 21 Oktoba, 2020 Dar es Salaam.*

## SURA YA NANE

## USHIRIKISHWAJI WA WADAU WA UCHAGUZI

Tume iliwashirikisha wadau mbalimbali nchi nzima kabla na wakati wa mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Ushirikishwaji huo ulihusisha kuwapa wadau taarifa mbalimbali na kupokea maoni na mapendekezo kwa kukutana nao katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Lengo la kuwashirikisha wadau lilikuwa ni kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za uchaguzi na kufanya mchakato wa uchaguzi kuwa jumuishi na shirikishi.

Wadau walioshirikishwa nchi nzima ni pamoja na Serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia, vyombo vya habari, taasisi na viongozi wa dini, makundi maalum katika jamii, vyombo vya ulinzi na usalama, wapiga kura, watazamaji wa uchaguzi na viongozi wa kimila.

### 8.1 Serikali

Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kifungu cha 120 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake iliyopewa kikatiba na kisheria kwa kuipatia rasilimali na nyenzo muhimu za kuendeshea mchakato wa uchaguzi. Aidha, Tume ilishirikisha Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kupeana taarifa mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Wizara na taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### 8.2 Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa ni moja ya wadau wakuu wa uchaguzi kwa kuwa husimamisha wagombea katika nafasi mbalimbali za uongozi. Tume inaamini mafanikio iliyoyapata katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, pamoja na mambo mengine, yalitokana na ushirikishaji

wa vyama vya siasa katika hatua zote muhimu. Maeneo ambayo Tume ilivishirikisha vyama vya siasa ni kama ifuatavyo: -

### 8.2.1 Maandalizi ya Kanuni

Tume ilikutana na viongozi wa vyama vya siasa na kupokea maoni yao juu ya Rasimu ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari zilizoandaliwa. Pia, Tume ilikutana na viongozi hao na kupokea maoni yao kuhusu kanuni za Uchaguzi Mkuu. Katika mikutano hiyo, Tume ilipokea maoni na mapendekezo kuhusiana na marekebisho ya kanuni na kuyafanyia kazi. Aidha, baada ya marekebisho hayo kukamilika vyama vya siasa vilipewa nakala za kanuni hizo kwa ajili ya rejea.

### 8.2.2 Uandaaji wa Maadili ya Uchaguzi

Kwa kushauriana na vyama vya siasa na Serikali, Tume iliandaa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020. Maadili hayo yaliridhiwa na kusainiwa na vyama vyote 19 vya siasa vyenye usajili wa kudumu, Serikali na Tume mnamo tarehe 27 Mei, 2020. Tume ilivipatia vyama vya siasa na wagombea nakala za Maadili hayo kwa ajili ya rejea.



*Tume ya Taifa ya Uchaguzi, mwakilishi wa Serikali na wawakilishi wa vyama vya siasa katika picha ya pamoja baada ya kusaini Maadili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020.*


MWENYEKITI - NEC


KATIBU MKUU OWM - SERIKALI



NAIBU KATIBU MKUU - ADA-TADEA


NAIBU KATIBU MKUU - CHAUMMA


KATIBU WA ITIKADI NA UENEZI - CCM


KATIBU MKUU - UDP


KATIBU MKUU - CHADEMA


-MWENYEKITI - UPDP


KATIBU MKUU - NCCR - Mageuzi


KATIBU MKUU - MAKINI


KATIBU MKUU - ACT - Wazalendo


KATIBU MKUU - TLP


MKURUGENZI - CUF


KATIBU MKUU- NRA


KATIBU MKUU - UMD


KATIBU MKUU - NLD


KATIBU MKUU - AAFP


NAIBU KATIBU MKUU - ADC


KATIBU MKUU- SAU


KATIBU MKUU - DP


MWENYEKITI - CCK

*Mwenyekiti wa Tume, Mwakilishi wa Serikali na wawakilishi wa vyama vya siasa wakati wa kusaini Maadili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 katika ukumbi wa JNICC tarehe 27 Mei, 2020.*

### 8.2.3 Mawakala wa Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa viliweka mawakala katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura, kupigia kura, kuhesabu kura na kujumlisha matokeo. Mawakala hao walipewa nafasi ya kujiridhisha katika kila hatua iliyokuwa ikifikiwa katika michakato husika na kutakiwa kujaza fomu maalum kuelezea kuridhika au kutokuridhika na mwenendo wa zoezi husika. Vyama vya siasa pia, vilielezwa juu ya haki ya kuwasilisha malalamiko katika mamlaka za kisheria ikiwa havikuridhishwa na namna mchakato wa uchaguzi ulivyoendeshwa.

### 8.2.4 Mifumo ya Menejimenti ya Uchaguzi

Vyama vya siasa vilipitishwa kwenye mifumo ya menejimenti ya uchaguzi kuona namna inavyofanya kazi kabla ya kuanza kutumika. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Uandikishaji wa Wapiga Kura (VRS), Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea (CMS), Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS) na Mfumo wa Uhakiki wa Taarifa za Wapiga Kura (VIS).

### 8.2.5 Kamati za Uchaguzi

Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliunda kamati mbalimbali za uchaguzi ambazo ziliwashirikisha wadau wa uchaguzi vikiwemo vyama vya siasa. Lengo la kamati hizo lilikuwa kuongeza uwazi na kupata maoni na ushauri wa wadau katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi.

Kamati hizo ni Kamati ya Mahusiano ya Serikali na Vyama vya Siasa, Kamati ya Ununuzi, Usambazaji na Lojistiki ya Vifaa, Kamati ya Watazamaji wa Uchaguzi na Mashirika ya Kimataifa, Kamati ya Uratibu wa Kampeni za Uchaguzi, Kamati ya Habari na Mawasiliano ya Umma, Kamati za Maadili ya Uchaguzi na Kamati ya Elimu ya Mpiga Kura na Asasi za Kiraia.

## 8.3 Wapiga Kura

Tume iliwashirikisha wapiga kura na wananchi kwa ujumla kwa kuwapatia taarifa muhimu kuhusiana na mchakato wa uchaguzi kupitia vyombo vya habari, mikutano, mitandao ya kijamii, machapisho na tovuti ya Tume. Hii ilifanyika ili kuwawezesha wapiga kura kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi hadi upigaji kura.

### 8.4 Taasisi na Asasi za Kiraia

Taasisi na asasi za kiraia zilishirikishwa kwa kupatiwa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura na utazamaji wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Eneo lingine la ushirikishwaji ni katika Kamati ya Habari na Mawasiliano na Kamati ya Elimu ya Mpiga Kura na Asasi za Kiraia. Vilevile, Tume ilifanya mikutano na wadau hao kwa lengo la kuzipatia miongozo ya utoaji wa elimu ya mpiga kura na taarifa mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

### 8.5 Vyombo vya Habari

Tume ilitoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia vyombo vya habari vya Umma na binafsi ili kuvishirikisha na kuvipa jukumu la kufikisha taarifa mbalimbali kwa wananchi wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Aidha, Tume ilikutana na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki katika mchakato wa uchaguzi mkuu. Vyombo vya habari pia, vilishirikishwa katika Kamati ya Elimu ya Mpiga kura na Asasi za Kiraia na Kamati ya Habari na Mawasiliano.




*Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (waliokaa) wakiwa kwenye picha na wahariri wa vyombo vya habari kwenye mkutano wa Tume na wahariri hao uliofanyika tarehe 19 Juni, 2020 Dar es Salaam.*

## 8.6 Taasisi za Dini

Taasisi za dini ni miongoni mwa wadau muhimu katika mchakato wa uchaguzi na zilikuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha amani na utulivu wakati wote. Tume katika kulitambua hilo iliwashirikisha kupitia mikutano mbalimbali iliyofanyika kabla ya zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu. Kupitia mikutano hiyo, Tume iliwapa taarifa muhimu za mwenendo wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Pamoja na hayo, Tume iliwasihi viongozi wa dini kuwahamasisha waumini wao kushiriki kwa amani na utulivu katika mchakato wa uchaguzi.




*Mkutano kati ya Tume na viongozi wa taasisi za dini uliofanyika tarehe 15 Agosti, 2020 Dar es Salaam.*

## 8.7 Makundi Maalum katika Jamii

Tume inatambua uwepo wa makundi maalum na mahitaji yao katika jamii ili kuweza kushiriki vyema katika mchakato wa uchaguzi. Makundi hayo ni watu wenye ulemavu, wanawake na vijana. Tume iliwashirikisha kwa kukutana nao ili kufahamu mahitaji yao wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu.

Aidha, wawakilishi wa watu wenye ulemavu wa kuona, walishiriki katika kuandaa rasimu ya majalada ya nukta nundu na kufanya uhakiki wakati wa uchapishaji wa majalada hayo. Tume ilikutana na wawakilishi hao tarehe 01 hadi 04 Septemba, 2020 kwa ajili hiyo. Pia, walishiriki kutoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu wa kutokuona ili kuwawezesha

kuyatumia majalada hayo ili waweze kupiga kura bila usaidizi.

Vilevile, kituturi kilitengenezwa kwa namna ambayo kiliweza kugeuzwa ili kuwawezesha wapiga kura wenye ulemavu wa viungo kupiga kura kwa urahisi. Eneo lingine ambalo Tume iliweka msisitizo wakati wa zoezi la uandikishaji na kupiga kura ni kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu, wagonjwa, wajawazito, wazee na wanawake wenye watoto wachanga waliokuja nao vituoni.




*Mikutano kati ya Tume na wawakilishi wa makundi maalum katika jamii iliyofanyika Dar es Salaam.*

## 8.8 Vyombo vya Ulinzi na Usalama

Tume inatambua jukumu la kisheria la vyombo vya ulinzi na usalama katika kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu katika shughuli za uchaguzi. Tume iliwashirikisha wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wakiwemo Inspekta Jenerali wa Polisi, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kuwakutanisha na Msajili wa Vyama vya Siasa, mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na wawakilishi wa vyama vya siasa tarehe 19 Agosti, 2020. Katika mkutano huo, wadau walijadili namna bora ya kuhakikisha uchaguzi mkuu unafanyika katika hali ya amani na utulivu.





*Mkutano wa Tume, vyombo vya ulinzi na usalama, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi tarehe 19 Agosti, 2020.*

### 8.9 Wazee wa Kimila na Wazee Maarufu

Wazee wa kimila na wazee maarufu ni kundi ambalo Tume ililipa umuhimu wa kipekee kutokana na heshima na ushawishi walionao katika jamii. Tume ilikutana na wazee hawa na kuwaeleza kuhusu zoezi la uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu na umuhimu wa jamii husika kushiriki katika mazoezi hayo. Lengo la Tume lilikuwa ni kuhakikisha kuwa wanashiriki katika kutoa elimu ya mpiga kura na kuwahamasisha wananchi katika jamii zao kushiriki katika uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu kwa amani na utulivu.



*Viongozi wa Tume wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa kimila katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Iringa.*

**8.10 Maoni na Mapendekezo ya Wadau**

Katika mikutano mbalimbali ya wadau iliyofanyika nchi nzima wakati wa uboreshaji wa Daftari na uchaguzi mkuu walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo: -

(i) sheria za uchaguzi kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili;

(ii) uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu usimamiwe na mamlaka moja;

(iii) elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia ziwe endelevu;

(iv) Serikali iwezeshe asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura;

(v) wapiga kura waruhusiwe kupiga kura ya Rais katika kituo chochote;

(vi) *diaspora* waruhusiwe kupiga kura;

(vii) wagombea ubunge na udiwani wanaochaguliwa bila kupingwa wapigiwe kura;

(viii) ushiriki wa wanawake na vijana kwenye mchakato wa uchaguzi uboreshwe;

(ix) kuboresha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum kwenye mchakato wote wa uchaguzi ikiwemo kampeni;

(x) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uwe endelevu; na

(xi) kuunganisha mifumo ya utambulisho wa watu ili kurahisisha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

## SURA YA TISA

## WATAZAMAJI WA UCHAGUZI

Watazamaji wa uchaguzi ni wadau muhimu katika mchakato wa uchaguzi ambao hushiriki katika kutazama uchaguzi na kutoa maoni kuhusiana na mchakato wa uchaguzi. Kwa mujibu wa kanuni ya 18 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 16 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, Tume ilitoa mwaliko na usajili kwa taasisi na asasi za ndani na kimataifa kwa ajili ya kutazama shughuli za uchaguzi.

### 9.1 Mialiko kwa Watazamaji wa Uchaguzi

Tume ilitoa mialiko kwa taasisi na asasi za ndani kupitia matangazo katika vyombo vya habari, tovuti ya Tume na mitandao ya kijamii. Mialiko pia ilitolewa kwa Tume za Uchaguzi rafiki, mashirika ya kikanda na taasisi za kimataifa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kutazama uchaguzi.

### 9.2 Usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi

Tume iliandaa kituo cha kusajili Watazamaji ambacho kilikuwa katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam. Usajili huo ulifanyika kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji wa Uchaguzi (Observer Management System – OMS). Pamoja na kusajili, mfumo huo ulitumika kutoa vitambulisho vya watazamaji wa uchaguzi. Taasisi za ndani 97 zenye jumla ya watazamaji 5,297 zilisajiliwa, na kwa upande wa Taasisi za Kimataifa, taasisi 17 zilisajiliwa ambazo zilikuwa na jumla ya watazamaji 196. Orodha ya taasisi na asasi zilizopewa vibali vya utazamaji imeoneshwa kwenye tovuti ya Tume yaani *www.nec.go.tz.*

### 9.3 Mikutano ya Tume na Watazamaji wa Uchaguzi

Tume ilifanya mikutano na watazamaji wa uchaguzi kabla na wakati wa uchaguzi ili kuwafahamisha kuhusu maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Aidha, Tume iliwapatia watazamaji wa uchaguzi, pamoja na vitu vingine, sheria za uchaguzi na kanuni zake, vitabu vya mwongozo kwa watazamaji, orodha na ramani za majimbo, orodha ya vituo vya kupigia kura na orodha ya vyama vya siasa. Pia, walipatiwa maelekezo mbalimbali ya uchaguzi na Jarida la Maandalizi kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza shughuli zao.






*Mkutano wa Tume na watazamaji wa uchaguzi, Dar es Salaam.*





*Mkutano wa Tume na watazamaji wa uchaguzi, Dar es Salaam.*

### 9.4 Kamati ya Watazamaji na Mashirika ya Kimataifa

Katika kufanikisha uratibu wa watazamaji wa uchaguzi, Tume iliunda kamati ya kuratibu utazamaji wa uchaguzi ambapo wajumbe wa kamati waliteuliwa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Idara ya Uhamiaji, Vyama vyote vya siasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kamati hiyo ilikuwa na jukumu la kujadili na kushauri masuala mbalimbali yanayohusu mwenendo wa watazamaji.

### 9.5 Taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi

Kwa kuzingatia kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, watazamaji wa uchaguzi wanatakiwa, katika kipindi kisichozidi miezi miwili tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi kuwasilisha taarifa zao Tume.

Jumla ya taasisi na asasi 18 kati ya taasisi na asasi 117 zilizopewa vibali vya kutazama uchaguzi mkuu zilitekeleza takwa hilo la kisheria. Kati ya taasisi na asasi 18 zilizowasilisha taarifa za utazamaji wa uchaguzi, 13 ni za ndani ya nchi wakati 5 ni taasisi za kimataifa. Maoni na mapendekezo mbalimbali yalitolewa katika taarifa za watazamaji zilizowasilishwa.

#### 9.5.1 Maoni ya Watazamaji

Watazamaji wa uchaguzi ambao waliwasilisha taarifa zao za utazamaji waliridhishwa na kutoa pongezi katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo: -

(i) matokeo ya uchaguzi wa Rais kutangazwa ndani ya saa 48 tangu kukamilika kwa zoezi la upigaji kura;

(ii) vituo vya kupigia kura kuwa na vifaa vya kutosha;

(iii) Serikali kugharamia shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa asilimia 100;

(iv) idadi kubwa ya vituo vya kupigia kura ambavyo vilikuwa rahisi kufikika na rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum;

(v) wapiga kura kutumia muda mfupi katika vituo vya kupigia kura;

(vi) kutumika kwa majalada ya nukta nundu katika vituo vya kupigia kura yaliyowawezesha watu wenye ulemavu wa kuona kupiga kura kwa urahisi;

(vii) kujitokeza kwa idadi kubwa ya wagombea wanawake katika nafasi mbalimbali za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ikilinganishwa na miaka mingine;

(viii) kutolewa kwa muda wa kutosha kwa wagombea kufanya kampeni;

(ix) mazingira ya amani na utulivu siku ya kupiga kura;

(x) vituo vingi vya kupigia kura kuwa na mawakala wa vyama vya siasa;

(xi) vituo vingi kufunguliwa na kufungwa kwa wakati;

(xii) mchakato wa uchaguzi kushirikisha makundi yote ya jamii kama vile vijana, wazee na wanawake; na

(xiii) watendaji wa vituo kutoa kipaumbele kwa makundi ya wazee, walemavu na wanawake wenye watoto wachanga waliokwenda nao vituoni.

### 9.5.2 Mapendekezo ya Watazamaji

Kimsingi, baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na watazamaji wa uchaguzi ni kama ifuatavyo: -

(i) elimu ya mpiga kura iendelee kutolewa kwa vyama vya siasa, mawakala na watendaji wa vituo;

(ii) ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalum katika uchaguzi uboreshwe;

(iii) juhudi zifanyike kuboresha mazingira ya kufanya siasa;

(iv) utaratibu wa kuwatambulisha mawakala wa vyama vya siasa upitiwe upya; na

(v) sheria za uchaguzi zifanyiwe marekebisho katika maeneo yafuatayo: -


 (a) matokeo ya uchaguzi wa Rais yaruhusiwe kupingwa mahakamani;

 (b) wagombea wa Ubunge na Udiwani wanaopita bila kupingwa wapigiwe kura kama ilivyo kwa mgombea wa nafasi ya kiti cha Rais;

 (c) utaratibu unaotumika kuwateua Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ufanyiwe marekebisho; na

 (d) mawakala wa vyama vya siasa wapewe vitambulisho mapema kabla ya siku ya uchaguzi.







*Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika picha za pamoja na baadhi ya Watazamaji wa Uchaguzi.*

# SURA YA KUMI

# TATHMINI YA UCHAGUZI MKUU

Tume ilifanya Tathmini baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, ikiwa ni mojawapo ya hatua muhimu katika mzunguko wa uchaguzi. Lengo la tathmini lilikuwa ni kupata mrejesho wa namna zoezi la uchaguzi lilivyotekelezwa. Pia, kujua mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Tume katika mchakato wa uchaguzi.

## 10.1 Maeneo ya Tathmini

Zoezi la tathmini lilifanyika katika mikoa 24, kati ya hiyo mikoa 22 ilikuwa ya Tanzania Bara na mikoa miwili ilikuwa ya Tanzania Zanzibar. Katika mikoa hiyo, majimbo 44 yalihusika kwa Tanzania Bara na majimbo manne kwa Tanzania Zanzibar. Tathmini hii ilifanyika kuanzia Novemba hadi Disemba 2020 na iliangazia mchakato wa uchaguzi kuanzia hatua ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, uteuzi wa wagombea, upigaji kura hadi kujumlisha na kutangaza matokeo.

## 10.2 Walengwa wa Tathmini

Walengwa wa tathmini hii waligawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza lilihusisha wapiga kura, makundi maalum katika jamii na viongozi wa vyama vya siasa. Walengwa katika kundi hili walihojiwa kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) upatikanaji wa kadi ya Mpiga kura;

(ii) uhakiki wa taarifa wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la awali;

(iii) njia zilizotumika kuhakiki taarifa za wapiga kura;

(iv) sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume;

(v) kufikika kwa vituo vya kupigia kura;

(vi) mawakala wa vyama vya siasa kuapishwa na kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao; na

(vii) mwitikio wa wapiga kura.

Kundi la pili lilihusisha watendaji wa uchaguzi katika ngazi ya vituo, kata na majimbo.

Walengwa katika kundi hili walihojiwa kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) ufanisi wa mashine za BVR katika kuandikisha wapiga kura; na

(ii) sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume.

Sampuli ya watu walioshiriki katika zoezi la tathmini imeoneshwa kwenye Jedwali Na. 33.

**Jedwali Na. 33: Sampuli ya Watu Walioshiriki katika Zoezi la Tathmini**

| Na. | Wahusika | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | |
| 1. | Wapiga Kura | 244 | 201 | 445 |
| 2. | Viongozi wa Vyama vya Siasa | 238 | 69 | 307 |
| 3. | Makundi Maalum katika jamii | 57 | 111 | 168 |
| 4. | Watendaji wa Uchaguzi Ngazi ya Halmashauri, Kata na Vituo | 637 | 317 | 954 |
| **Jumla** | | **1,176** | **698** | **1,874** |

## 10.3 Njia Zilizotumika Kufanya Tathmini

Tume ilitumia njia mbalimbali katika kukusanya taarifa. Njia hizo ni pamoja na mahojiano ya ana kwa ana, madodoso, majadiliano na makundi mbalimbali na mikutano. Njia nyingine zilikuwa ni kufanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kama vile taarifa zilizotolewa na watazamaji wa uchaguzi, taasisi na asasi za kiraia zilizotoa elimu ya mpiga kura.

## 10.4 Matokeo ya Tathmini

Matokeo ya tathmini katika baadhi ya maeneo ni haya yafuatayo: -

### 10.4.1 Ufanisi wa Mashine za BVR

Wahojiwa 1,706 walitoa maoni kuhusu ufanisi wa mashine za BVR katika kuandikisha wapiga kura. Kati ya hao, 954 walikuwa watendaji wa uboreshaji, 752 wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa. Watendaji 942 kati ya 954 waliohojiwa ikiwa ni sawa na asilimia 98.7 walieleza kuwa mashine hizo zilifanya kazi ipasavyo na watendaji 12 sawa na asilimia 1.3 walisema kuna wakati mashine za BVR zilishindwa kufanya kazi ipasavyo. Wahojiwa 467 kati ya wahojiwa 752 ambao ni wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa sawa na asilimia 62.1 walieleza kuwa mashine hizo zilifanya kazi ipasavyo na wahojiwa 285 sawa na asilimia 37.9 walisema kuna wakati mashine za BVR zilishindwa

kufanya kazi ipasavyo.

Matokeo haya yanaonesha kuwa mashine za BVR kwa kiwango kikubwa zilifanya kazi kwa ufanisi wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

### 10.4.2 Upatikanaji wa Kadi ya Mpiga Kura

Wahojiwa 752 ambao ni wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu upatikanaji wa kadi ya mpiga kura. Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 640 kati ya 752 ya waliohojiwa sawa na asilimia 85.1 walisema upatikanaji wa kadi ya mpiga kura ulikuwa rahisi na 112 sawa na asilimia 14.9 walisema upatikanaji wa kadi ya mpiga kura haukuwa rahisi. Kwa kuzingatia maoni haya, inaonesha kuwa kwa kiwango kikubwa, mchakato wa upatikanaji wa kadi za mpiga kura ulikuwa rahisi.

### 10.4.3 Uhakiki wa Taarifa Wakati wa Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali

Wahojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu kuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali. Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 601 kati ya 752 ya walioulizwa swali hili, sawa na asilimia 79.9 walisema walihakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali na 151 sawa na asilimia 20.1 walisema hawakuhakiki taarifa zao. Matokeo haya yanaonesha kuwa, idadi kubwa ya waliohojiwa walihakiki taarifa zao.

### 10.4.4 Njia Zilizotumika Kuhakiki Taarifa za Wapiga Kura

Wahojiwa ambao walihakiki taarifa zao, waliulizwa pia njia ambazo walitumia kuhakiki taarifa zao. Viongozi wa vyama vya siasa na wapiga kura 548 kati ya 601 ya waliohakiki taarifa zao sawa na asilimia 91.2 walisema walitumia njia ya kwenda vituoni, ambapo wahojiwa 31 sawa na asilimia 5.1 walitumia njia ya simu za mkononi na wahojiwa 22 sawa na asilimia 3.7 walitumia tovuti ya Tume kuhakiki taarifa zao. Matokeo haya yanaonesha kuwa, wapiga kura wengi walipendelea kutumia njia ya kwenda kituoni moja kwa moja kuhakiki taarifa zao. Aidha, matokeo haya pia, yanaonesha kuwepo kwa njia za kielektroniki kulitoa njia mbadala kwa wapiga kura kuhakiki taarifa zao.

### 10.4.5 Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume

Kati ya viongozi wa vyama vya siasa na watendaji wa uchaguzi 1,261 waliohojiwa, wahojiwa 1,241 sawa na asilimia 98.4 walisema kuwa sheria, kanuni, maadili na vitabu

vya maelekezo kwa wadau wa uchaguzi vilisaidia katika kuendesha uchaguzi. Aidha, wahojiwa 20 sawa na asilimia 1.6 walisema kuwa sheria, kanuni, maadili na vitabu vya maelekezo havikusaidia katika kuendesha uchaguzi. Matokeo haya yanaonesha kuwa sheria, kanuni na maelekezo kwa wadau wa uchaguzi yalisaidia katika kuendesha uchaguzi.

### 10.4.6 Kufikika kwa Vituo vya Kupigia Kura

Wahojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu urahisi wa kufika au vinginevyo kwenye vituo vya kupigia kura. Wahojiwa 654 kati ya 752 sawa na asilimia 86.9 walisema vituo vya kupigia kura vilifikika kwa urahisi. Wakati wahojiwa 98 sawa na asilimia 13.1 walisema vituo vya kupigia kura havikufikika kwa urahisi. Matokeo haya yanaonesha kuwa vituo vya kupigia kura katika maeneo mengi nchini vilifikika kwa urahisi.

### 10.4.7 Kuapishwa kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa

Viongozi wa vyama vya siasa 307 walihojiwa kuhusu zoezi la kuapisha mawakala na utaratibu uliotumika kuwaruhusu kuingia vituoni siku ya uchaguzi. Wahojiwa 257 kati ya 307 ambao ni sawa na asilimia 83.7 walisema mawakala waliapishwa na kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati. Wakati wahojiwa 38 sawa na asilimia 12.3 walisema mawakala hawakuapishwa wala kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati. Aidha, wahojiwa 12 sawa na asilimia 4.0 walisema hawajui lolote kuhusiana na suala hili. Matokeo haya yanaonesha kuwa kwa kiasi kikubwa mawakala wa vyama vya siasa waliokidhi matakwa ya kisheria na kikanuni walipata fursa ya kutekeleza majukumu yao.

### 10.4.8 Mwitikio wa Wapiga Kura

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kati ya wapiga kura 29,754,699 walioandikishwa katika Daftari, wapiga kura 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 walijitokeza kupiga kura. Katika tathmini ya mwitikio wa wapiga kura, jumla ya mikutano na mijadala 24 ilifanyika. Washiriki wa mikutano hiyo walitoka kwenye makundi ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake.

#### 10.4.8.1 Sababu za Mwitikio wa Wapiga Kura kuwa Mdogo

Washiriki waliulizwa kuhusu mwitikio mdogo wa wapiga kura kwa baadhi ya maeneo siku ya kupiga kura. Baadhi ya sababu zilizobainishwa ni pamoja na zifuatazo: -

(i) baadhi ya wapiga kura kuwa maeneo tofauti na vilipo vituo walivyojiandikishia kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kazi, kilimo, safari na masomo;

(ii) elimu ya mpiga kura iliyotolewa kutofika katika maeneo yote, hasa maeneo ya vijijini;

(iii) kukosekana kwa elimu ya uraia ya kutosha;

(iv) umbali wa vituo vya kupigia kura kwa baadhi ya maeneo;

(v) baadhi ya wagombea kushindwa kutekeleza ahadi wanazotoa wakati wa kampeni;

(vi) wagombea kuchaguliwa bila kupingwa katika baadhi ya maeneo;

(vii) baadhi ya wapiga kura kupoteza kadi za kupigia kura;

(viii) hofu ya usalama wakati wa kupiga kura kwa baadhi ya maeneo;

(ix) baadhi ya wapiga kura kuwa na imani kuwa mgombea wa chama fulani atashinda;

(x) wapiga kura kujikita zaidi katika shughuli nyingine za uzalishaji siku ya kupiga kura;

(xi) baadhi ya vyama kuwashawishi wapiga kura wasiende kupiga kura;

(xii) baadhi ya vyama kukosa sera bora za kuwavutia wapiga kura;

(xiii) hali ya hewa katika baadhi ya maeneo hususan maeneo yenye mvua kipindi cha mwezi Oktoba;

(xiv) baadhi ya wananchi kujiandikisha kupiga kura kwa lengo la kupata kadi ya mpiga kura ili waitumie kwa shughuli zingine;

(xv) baadhi ya wapiga kura kutohakiki majina yao kwenye Daftari hivyo kushindwa kufahamu vituo watakavyopigia kura vilipo;

(xvi) baadhi ya vyama kushindwa kufanya kampeni za kutosha katika maeneo yote; na

(xvii) baadhi ya vyama kununua kadi za wapiga kura ili wapiga kura washindwe kwenda kupiga kura.

#### 10.4.8.2 Mapendekezo ya Kuboresha Mwitikio wa Wapiga Kura

Washiriki wa zoezi la tathmini kutoka katika makundi ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake walipendekeza mambo yafuatayo ili kuboresha mwitikio wa

wapiga kura katika chaguzi zijazo. Baadhi ya mambo yaliyopendekezwa ni yafuatayo: -

(i) elimu ya mpiga kura iwe endelevu na itolewe kwa muda mrefu zaidi kwa maeneo yote nchini hasa vijijini;

(ii) asasi za kiraia na taasisi nyingine zinazohusika na utoaji wa elimu ya mpiga kura ziruhusiwe kutoa elimu endelevu;

(iii) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uwe endelevu;

(iv) watendaji wa Tume waendelee kusimamia uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya kazi zao bila upendeleo; na

(v) Tume ianzishe utaratibu wa kupiga kura kwa njia ya mtandao (*electronic voting*).

## SURA YA KUMI NA MOJA

## MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

Katika kusimamia, kuratibu na kuendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kulikuwa na mafanikio yafuatayo: -

### 11.1 Mafanikio Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

(i) kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kufikisha idadi ya wapiga kura 29,754,699 ikilinganishwa na wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015;

(ii) kufanikiwa kusanifu, kujenga na kutumia mifumo minane ya menejimenti ya uchaguzi kwa ushirikiano na wataalam wengine wa ndani ya nchi;

(iii) kuongeza idadi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura kutoka 36,929 vya mwaka 2015 hadi kufikia 37,814 kwa mwaka 2020, hivyo kuwezesha vituo kufikika kwa urahisi;

(iv) kufanikiwa kufanya zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura licha ya changamoto ya uwepo wa ugonjwa wa COVID -19;

(v) kukusanya takwimu za watu wenye mahitaji maalum wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari; na

(vi) kuwawezesha wapiga kura kuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kutumia Mfumo wa Uhakiki wa Taarifa za Wapiga Kura (Voters Interaction System - VIS).

### 11.2 Mafanikio Wakati wa Uchaguzi Mkuu

(i) uchaguzi mkuu kufanyika na kukamilika katika hali ya amani na utulivu;

(ii) kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais ndani ya saa 48 baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura;

(iii) kufanikiwa kufanya uchaguzi licha ya changamoto ya uwepo wa ugonjwa wa COVID -19;

(iv) matumizi ya mifumo ya TEHAMA iliyosanifiwa na kujengwa na wataalam wa ndani ya nchi katika usajili wa wagombea, usajili wa watazamaji, uhakiki wa taarifa za wapiga kura na vituo, kujumlisha na kutangaza matokeo;

(v) kuongeza vituo vya kupigia kura kutoka 65,105 vya mwaka 2015 hadi kufikia 81,567 kwa mwaka 2020, hivyo kusogeza vituo karibu zaidi na wapiga kura na kuepusha msongamano wa wapiga kura vituoni;

(vi) kuruhusu matumizi ya vitambulisho mbadala kwa wapiga kura waliopoteza kadi za mpiga kura. Vitambulisho hivyo ni leseni ya udereva, pasi ya kusafiria na kitambulisho cha Taifa (NIDA);

(vii) kuwepo kwa majalada ya nukta nundu (*tactile ballot folders*) yaliyoandaliwa kwa kuwashirikisha watu wenye ulemavu wa kutoona kwa ajili ya kupiga kura;

(viii) kuongeza wigo wa ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi hadi ngazi ya mikoa;

(ix) kufanikiwa kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo mengi ya nchi na kuandaa uchaguzi wa mfano (*mock election*) kwa waandishi wa habari; na

(x) kukamilika kwa ujenzi wa ofisi za Tume Jijini Dodoma na ukarabati wa ofisi ya Tume Zanzibar ambapo shughuli za uchaguzi zilifanyikia.

### 11.3 Changamoto

Wakati wa kusimamia na kuratibu shughuli za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uchaguzi mkuu, Tume ilipata changamoto zifuatazo: -

#### 11.3.1 Changamoto Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

(i) kuwepo kwa idadi kubwa ya wananchi waliopoteza kadi za kupigia kura au kadi zao kuharibika;

(ii) baadhi ya asasi na taasisi zilizopewa vibali vya elimu ya mpiga kura kushindwa kutekeleza jukumu hilo;

(iii) wapiga kura kushindwa kukumbuka kwa usahihi taarifa zao binafsi wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura walipokwenda vituoni kwa ajili ya kurekebisha taarifa zao, hivyo kutumia muda mrefu katika kutafuta majina;

(iv) uwepo wa mvua nyingi zilizoharibu miundombinu ya barabara, hivyo kuathiri usafirishaji na usambazaji wa vifaa vya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika baadhi ya maeneo; na

(v) mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili.

### 11.3.2 Changamoto Wakati wa Zoezi la Uchaguzi Mkuu

(i) mwitikio mdogo wa wapiga kura katika baadhi ya maeneo;

(ii) baadhi ya asasi na taasisi zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura kushindwa kutoa elimu hiyo;

(iii) baadhi ya wananchi kushindwa kuhakiki taarifa zao hivyo kushindwa kutambua vituo vyao vya kupigia kura;

(iv) madai ya baadhi ya mawakala wa vyama vya siasa kuzuiliwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura;

(v) madai ya baadhi ya wagombea kuwa hawakupata majibu ya rufaa zao, wakati hakuna kumbukumbu za rufaa hizo kupokelewa wala kusajiliwa na Tume; na

(vi) baadhi ya majengo yanayotumiwa kwa ajili ya vituo vya kupigia kura kukosa miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum.

# SURA YA KUMI NA MBILI

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 12.1 Hitimisho

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa mafanikio. Mafanikio hayo yalitokana na hali ya amani na utulivu iliyokuwepo nchini na utekelezaji wa mipango iliyojiwekea. Mipango hiyo ilitekelezwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Katika maandalizi ya uchaguzi mkuu, Tume ilihakiki vituo vya kuandikisha wapiga kura na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Baada ya kukamilisha zoezi la uboreshaji wa Daftari, Tume iliandaa vituo vya kupigia kura. Vilevile, Tume ilifanya ununuzi na usambazaji wa vifaa vya uchaguzi, uteuzi wa watendaji wa uchaguzi na mafunzo, uteuzi wa wagombea, kushughulikia rufaa za wagombea, uratibu wa kampeni za uchaguzi, utoaji wa elimu ya mpiga kura, kusimamia zoezi la kupiga na kuhesabu kura, kujumlisha na hatimae kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Kwa ujumla, zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 liliendeshwa na kuratibiwa kwa mafanikio. Aidha, maoni na mapendekezo mbalimbali ya watazamaji waliowasilisha taarifa zao yanabainisha kuwa uchaguzi huo ulikuwa huru, wa haki na wa kuaminika.

## 12.2 Mapendekezo

Ili kuboresha uendeshaji wa uchaguzi, Tume inapendekeza yafuatayo: -

(i) itungwe sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo itaiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;

(ii) kuwe na watendaji wa Tume hadi ngazi ya halmashauri;

(iii) mamlaka husika ziangalie uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo;

(iv) sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili; na

(v) Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha kifedha asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: Idadi ya Wapiga Kura Walioandikishwa kwa kila Mkoa**

| **Wapiga Kura Walioandikishwa na NEC** | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Mkoa** | **Walioandikishwa** |
| 1. | Arusha | 1,255,584 |
| 2. | Dar es Salaam | 3,427,917 |
| 3. | Dodoma | 1,327,829 |
| 4. | Geita | 1,212,146 |
| 5. | Iringa | 625,681 |
| 6. | Kagera | 1,412,008 |
| 7. | Kaskazini Pemba | 26,663 |
| 8. | Kaskazini Unguja | 21,926 |
| 9. | Katavi | 452,948 |
| 10. | Kigoma | 1,043,281 |
| 11. | Kilimanjaro | 1,009,726 |
| 12. | Kusini Pemba | 18,980 |
| 13. | Kusini Unguja | 13,666 |
| 14. | Lindi | 645,644 |
| 15. | Manyara | 883,431 |
| 16. | Mara | 1,115,777 |
| 17. | Mbeya | 1,137,084 |
| 18. | Mjini Magharibi | 47,605 |
| 19. | Morogoro | 1,612,952 |
| 20. | Mtwara | 930,841 |
| 21. | Mwanza | 1,845,816 |
| 22. | Njombe | 452,982 |
| 23. | Pwani | 992,067 |
| 24. | Rukwa | 638,979 |
| 25. | Ruvuma | 904,078 |
| 26. | Shinyanga | 995,918 |
| 27. | Simiyu | 900,759 |
| 28. | Singida | 848,456 |
| 29. | Songwe | 619,703 |
| 30. | Tabora | 1,463,665 |
| 31. | Tanga | 1,304,235 |
| **Jumla** | | **29,188,347** |

| Wapiga Kura Walioandikishwa na ZEC | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Mkoa** | **Walioandikishwa** |
| 1. | Kaskazini Pemba | 64,114 |
| 2. | Kaskazini Unguja | 101,539 |
| 3. | Kusini Pemba | 77,978 |
| 4. | Kusini Unguja | 80,330 |
| 5. | Mjini Magharibi | 242,391 |
| **Jumla** | | **566,352** |
| **Jumla kuu** | | **29,754,699** |

**Kiambatisho Na. 2: Orodha ya Wabunge Waliochaguliwa bila Kupingwa**

| Na | Halmashauri | Jimbo | Jina la Mgombea | Chama |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wilaya ya Kongwa | Kongwa | JOB Yustino Ndugai | CCM |
| 2. | Wilaya ya Bumbuli | Bumbuli | JANUARY Yusuf Makamba | CCM |
| 3. | Wilaya ya Pangani | Pangani | JUMAA Hamidu Aweso | CCM |
| 4. | Wilaya ya Gairo | Gairo | SHABIBY Ahmed Mabkhut | CCM |
| 5. | Wilaya ya Mlimba | Mlimba | KUNAMBI Emmanuel Godwin | CCM |
| 6. | Wilaya ya Kilosa | Kilosa | KABUDI Palamagamba John | CCM |
| 7. | Wilaya ya Morogoro | Morogoro Kusini | KALOGERIS Innocent Edward | CCM |
| 8. | Wilaya ya Morogoro | Morogoro Kusini Mashariki | TALETALE Hamisi Shabani | CCM |
| 9. | Wilaya ya Mvomero | Mvomero | ZEELAND Jonas Van | CCM |
| 10. | Wilaya ya Chalinze | Chalinze | KIKWETE Ridhiwani Jakaya | CCM |
| 11. | Wilaya ya Mtama | Mtama | NAPE Moses Nnauye | CCM |
| 12. | Wilaya ya Ruangwa | Ruangwa | MAJALIWA Kassim Majaliwa | CCM |
| 13. | Wilaya ya Madaba | Madaba | JOSEPH Kizito Mhagama | CCM |
| 14. | Mji wa Mafinga | Mafinga Mjini | CHUMI Cosato David | CCM |
| 15. | Wilaya ya Songwe | Songwe | MULUGO Philipo Augustino | CCM |
| 16. | Wilaya ya Ileje | Ileje | Mhandisi. MSONGWE Godfrey Kasekenya | CCM |
| 17. | Wilaya ya Kaliua | Ulyankulu | REHEMA Juma Migilla | CCM |
| 18. | Wilaya ya Nzega | Nzega Vijijini | DKT. KIGWANGALLA Hamisi Andrea | CCM |
| 19. | Wilaya ya Kalambo | Kalambo | JOSEPHAT Sinkamba Kandege | CCM |
| 20. | Wilaya ya Msalala | Msalala | IDDI Kassim Iddi | CCM |
| 21. | Wilaya ya Ushetu | Ushetu | KWANDIKWA Elias John | CCM |
| 22. | Wilaya ya Misungwi | Misungwi | MNYETI Alexander Pastory | CCM |
| 23. | Wilaya ya Butiama | Butiama | SAGINI Jumanne Abdallah | CCM |
| 24. | Mji wa Babati | Babati Mjini | GEKUL Pauline Philipo | CCM |
| 25. | Wilaya ya Babati | Babati Vijijini | SILLO Daniel Baran | CCM |
| 26. | Wilaya ya Ludewa | Ludewa | KAMONGA Joseph Zacharius | CCM |
| 27. | Wilaya ya Njombe | Lupembe | SWALLE Edwin Enosy | CCM |
| 28. | Wilaya ya Mlele | Katavi | ISACK Aloyce Kamwelwe | CCM |

**Kiambatisho Na. 3: Risala ya Mwenyekiti**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## RISALA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KUHUSU UPIGAJI KURA UTAKAOFANYIKA JUMATANO TAREHE 28 OKTOBA, 2020

**Ndugu wananchi**

Kama mnavyofahamu, kesho tarehe 28 Oktoba, 2020, ni siku ya kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa mujibu wa ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndicho chombo chenye mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Tume tayari imekamilisha maandalizi yote muhimu ya uchaguzi, vikiwemo vifaa. Hadi kufikia leo, vifaa vimefikishwa kwenye maeneo husika na sasa zoezi la kusambazwa vifaa hivyo kwenye vituo vya kupigia kura linaendelea. Mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi kwa maana ya wasimamizi wa vituo, wasimamizi wasaidizi na makarani waongozaji wapiga kura yalikamilika tarehe 26 Oktoba, 2020.

**Ndugu wananchi**

Nitumie nafasi hii kuvipongeza vyama vya siasa na wagombea waliojitokeza kuchukua fomu na kuteuliwa kuwa wagombea katika nafasi mbalimbali.

Nitumie nafasi hii pia kuwapongeza wananchi wote, kwa utulivu mliouonesha wakati wote wa kipindi cha kampeni. Ingawa kulikuwa na kasoro ndogondogo katika kampeni hizo, kamati za maadili katika kila ngazi husika zilishughulikia malalamiko kwa mujibu wa sheria. Aidha, juhudi zilifanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kukemea ukiukwaji wa maadili uliofanywa na baadhi ya wagombea ili kuwezesha kampeni kufanyika kwa usalama na amani.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi mkuu iliyotangazwa na Tume, leo saa 12.00 jioni ndio mwisho wa kampeni za uchaguzi kwa Tanzania Bara, kampeni ambazo zilianza tangu tarehe 26 Agosti, 2020, ikiwa ni siku moja baada ya zoezi la uteuzi wa wagombea kufanyika. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kampeni hizo zilikamilika jana ili kupisha kura ya mapema ambayo imefanyika leo.

**Ndugu wananchi**

Katika uchaguzi mkuu utakaofanyika kesho jumla ya wapiga kura 29,754,699 wanatarajiwa kushiriki. Kati ya hao, wapiga kura 29,188,347 wameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) na wapiga kura 566, 352 wameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Katika uchaguzi huu, Tume itatumia jumla ya vituo vya kupigia kura 81,567 vikiwemo vituo 80,155 vinavyotokana na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la NEC na vituo 1,412 vinavyotokana na Daftari la Wapiga Kura la ZEC.

Katika uchaguzi huu, vyama vya siasa 15 vimesimamisha wagombea katika nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais. Aidha, vyama vyote 19 vyenye usajili wa kudumu vinashiriki uchaguzi huu kwa kusimamisha wagombea katika nafasi mbalimbali za uongozi. Kwa mujibu wa takwimu, kuna jumla ya wagombea 1,257 katika nafasi ya Ubunge na kuna jumla ya wagombea 9,231 katika nafasi ya Udiwani.

Kutokana na kuwepo kwa wagombea ubunge 28 waliochaguliwa bila kupingwa kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, uchaguzi katika nafasi hiyo utafanyika katika majimbo 236 badala ya majimbo 264. Vivyo hivyo, katika nafasi ya udiwani, uchaguzi utafanyika katika kata 3,071 badala ya 3,953 kutokana na kuwepo kwa Madiwani 882 waliochaguliwa bila kupingwa kwa mujibu wa kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Tume imechambua takwimu kwa kuangalia pia uwiano wa kijinsia katika nafasi zote za uongozi zinazogombewa. Wagombea wanawake katika nafasi ya kiti cha Rais ni wawili kati ya 15, sawa na asilimia 13. Kwa nafasi ya kiti cha Makamu wa Rais, wanawake ni watano kati ya 15, sawa na asilimia 33.

Wagombea wanawake kwa nafasi ya ubunge walioteuliwa ni 293, sawa na asilimia 23. Kwa upande wa madiwani, wanawake walioteuliwa ni 668, sawa na asilimia 7.2 ya wagombea wote.

**Ndugu wananchi**

Kwa niaba ya Tume, napenda kutoa rai kwa wananchi wenye sifa za kupiga kura kwa maana ya wale wote mliojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuzingatia kifungu cha 10 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kikisomwa pamoja na kifungu cha 15 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, kujitokeza kwa wingi kuchagua viongozi mnaowataka. Kila mpiga kura akumbuke kuwa kupiga kura ni haki ya kikatiba kwa mujibu wa ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kwamba kura ni sauti yake inayomuwezesha kumuweka kiongozi madarakani.

**Ndugu wananchi**

Tume kupitia vikao vyake ilifanya uamuzi juu ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza kuhusu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na mabadiliko ya mipaka ya kiutawala na kutoa maelekezo ya kisera. Lengo ni kuhakikisha kila mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura anapata nafasi ya kufanya hivyo. Kwa kuzingatia kifungu cha 3, 13(2) na 61(3) (a) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, vikisomwa pamoja na kifungu cha 4 na 62 (a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume pamoja na mambo mengine imetoa maelekezo yafuatayo ya kisera katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020:-

i. Kuruhusu matumizi ya kitambulisho mbadala kwa wapiga kura ambao kadi zao zimeharibika au zimepotea.Vitambulisho ambavyo vimeruhusiwa kutumika kama utambulisho wa mpiga kura ni kitambulisho cha Taifa (NIDA), leseni ya udereva na pasi ya kusafiria (*passport*). Mpiga kura anaruhusiwa kutumia kimojawapo kati ya vitambulisho hivyo ili mradi majina yake yaliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kituoni yafanane na yale yaliyopo katika kitambulisho mbadala alichowasilisha.

ii. Kutoa ruhusa ya kupiga kura kwa mtu ambaye picha yake haipo au haionekani katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kituoni, lakini mtu huyo anayo kadi ya mpiga kura yenye taarifa zake binafsi zilizo sawa na taarifa zilizomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la kituo.

iii. Kuruhusu kupiga kura kwa yule ambaye namba yake ya kadi ya mpiga kura inatofautiana na ile iliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hili litafanyika iwapo tu taarifa nyingine zote za mpiga kura zikiwemo picha na taarifa binafsi zinafanana na zile zilizopo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

iv. Kutowaruhusu kupiga kura wale ambao wana kadi za kupigia kura lakini taarifa zao hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**Ndugu wananchi**

Tume inatumia fursa hii pia kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea, mawakala na wafuasi wao kuhakikisha wanafuata Sheria, kanuni, taratibu na maelekezo ya Tume wakati wote wa zoezi la upigaji kura, kuhesabu, kujumlisha na kutangaza matokeo. Wakati wote wa zoezi la kupiga kura na kuhesabu kura, mawakala wa vyama vya siasa wanatakiwa kuwepo kwenye vituo husika.

Wajibu wa mawakala hao ni kulinda maslahi ya vyama vyao na wagombea. Hata hivyo, hawatakiwi kuingilia masuala ya utendaji ambayo yamekasimiwa kwa mujibu wa sheria kwa wasimamizi wa vituo. Iwapo wataridhishwa au kutoridhishwa na namna uchaguzi unavyoendeshwa vituoni watapaswa kujaza maelezo yao katika fomu maalum ambazo watapatiwa na wasimamizi wa vituo. Ifahamike kuwa, kutokuwepo kwa wakala hakutazuia zoezi la uchaguzi kuendelea kituoni.

Ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi haukuishia kwa mawakala wa vyama vya siasa pekee. Tume imeruhusu watazamaji wa uchaguzi wa ndani na kimataifa zaidi ya 5,000 ambapo kesho watapita katika vituo mbalimbali vya kupigia kura. Natoa wito kwa wananchi na watendaji wa uchaguzi kuwapa ushirikiano wa kutosha.

Kundi lingine litakalopata nafasi ya kushuhudia zoezi la upigaji kura ni waandishi wa habari zaidi ya 1,500 ambao waliomba na kupewa vitambulisho maalum na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Niwakumbushe waandishi wa habari kuwa wanaruhusiwa kuingia ndani ya vituo lakini hawaruhusiwi kupiga picha wala kuhoji watendaji wa uchaguzi ndani ya kituo.

**Ndugu wananchi**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha na kuwasisitizia wananchi na wapiga kura wote, kuhusu mambo yafuatayo:-

i. Vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na vitafungwa saa 10:00 jioni. Hata hivyo, mpiga kura yeyote atakayekuwepo kituoni wakati wa kufunga kituo ataruhusiwa kupiga kura. Aidha, ifikapo saa 10:00 jioni mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mpiga kura wa mwisho kwenye mstari ili kuhakikisha kwamba mpiga kura anayepiga kura ni yule aliyefika ndani ya muda uliobainishwa. Zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura wote watakapomalizika.

ii. Hairuhusiwi kuvaa sare za chama cha siasa kwenye vituo vya kupigia kura au kuendesha kampeni siku ya uchaguzi.

iii. Iwapo Mpiga kura atafika kituoni na kushindwa kutambua kituo chake cha kupigia kura, atasaidiwa na karani mwongozaji wapiga kura kwa kutafuta jina lake kwenye orodha na kumwelekeza kituo cha kupigia kura kilipo. Hii inajitokeza pale ambapo kuna kuwa na wapiga kura wengi walioandikishwa katika kituo husika na hivyo kulazimika kuwagawa wapiga kura kwa idadi isiyozidi 500 katika kila kituo.

iv. Mpiga kura afikapo kituoni anapaswa kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wanaonyonyesha ambao wamekwenda vituoni na watoto.

v. Wapiga kura wenye ulemavu wa kutoona lakini wana ufahamu wa kusoma maandishi ya nukta nundu, watapewa fursa ya kutumia kifaa cha *Tactile Ballot Folder* ili kupiga kura. Wale wasioweza kukitumia kifaa hicho, wataruhusiwa kwenda vituoni na watu waliowachagua wenyewe ili kuwasaidia kupiga kura.

Mtu mmoja anaweza kumsadia mpiga kura mmoja tu labda kama wapo wapiga kura zaidi ya mmoja kutoka katika kaya moja.

Kwa mujibu wa kanuni ya 57 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 ikisomwa pamoja na kanuni ya 50 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, upigaji kura ni wa

siri, hivyo kila mtu apige kura yake kwa siri na mtu asishawishiwe na mtu yeyote kueleza nani amempigia kura. **KURA YAKO NI SIRI YAKO.**

vi. Mara baada ya kupiga kura, wapiga kura wanatakiwa kuondoka vituoni. Kwa kuwa vyama vya siasa vitakuwa vimeweka mawakala wao vituoni, hao watalinda maslahi ya vyama husika na wagombea wao.

vii. Kwa kuzingatia kifungu cha 61(3) (a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kifungu 62(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mpiga kura atapiga kura kwenye kituo chake alichojiandikisha au alichopangiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hivi karibuni kumekuwepo na upotoshaji kuwa mpiga kura anaweza kupiga kura ya Urais katika kituo kingine mbali ya pale alipojiandikisha. Jambo hili si la kweli, kwani ili mtu aweze kupiga kura kumchagua Rais, Mbunge au Diwani ni lazima awemo kwenye Daftari la Wapiga Kura la kituo alichojiandikisha.

**Ndugu wananchi**

Nitumie nafasi hii kuelezea utaratibu wa kutangaza matokeo. Kwanza, ifahamike kuwa ibara ya 41(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 81 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha 82 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, imetoa mamlaka ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi.

Baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika, vituo hivyo hugeuka kuwa vituo vya kuhesabu kura. Kwa maana hiyo, kura zitahesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Matokeo yatajazwa kwenye fomu maalum ambazo zitatiwa saini na msimamizi wa kituo pamoja na mawakala. Wakala anaweza kupewa nakala ya fomu ya matokeo na nakala nyingine itabandikwa mahali pa wazi nje ya kituo.

Msimamizi wa kituo atapeleka nakala halisi ya fomu ya matokeo na vifaa vya uchaguzi vilivyotumika kwenye zoezi la upigaji kura pamoja na matokeo ya kiti cha Rais na Mbunge kwa msimamizi wa uchaguzi. Matokeo ya uchaguzi wa madiwani yatapelekwa kwa msimamizi msaidizi wa uchaguzi. Mawakala wa vyama wataruhusiwa kusindikiza msafara wa kupeleka matokeo hayo.

Matokeo yote yakishapokelewa katika ngazi husika yatajumlishwa mbele ya mawakala na wote wanaoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya kujumlishia matokeo kwa mujibu wa kifungu cha 72 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kifungu cha 73(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali ya Mitaa, Sura ya 292.

Kama ilivyokuwa wakati wa kuhesabu kura, baada ya ujumlishaji kukamilika, matokeo yatatiwa saini na msimamizi wa uchaguzi na mawakala watakaokuwepo. Mawakala wanaweza kupewa nakala ya matokeo na nakala moja itabandikwa mahali pa wazi nje ya kituo cha ujumlishaji.

Matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yatatangazwa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Matokeo ya uchaguzi wa Wabunge yatatangazwa na wasimamizi wa uchaguzi na katika hatua hiyo msimamizi wa uchaguzi atataja idadi ya kura alizopata kila mgombea wa kiti cha Rais katika jimbo lake.

Matokeo ya uchaguzi wa Rais yakiwa katika fomu maalum yatatumwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume itayahakiki na kuyatangaza matokeo ya kila jimbo kwa kutaja idadi ya kura ambazo mgombea amepata katika jimbo husika. Katika kipindi hicho matokeo yatatangazwa kwa kadri yatakavyopokelewa kutoka majimboni. Baada ya kupokea matokeo kutoka majimbo yote, Tume itayajumlisha na hatimaye kutangaza mshindi.

Ifahamike kuwa mawakala wa vyama vya siasa watakuwepo kushuhudia zoezi la kutangaza matokeo ya kila jimbo kuanzia kujumlisha matokeo na hatimaye kumtangaza mshindi.

Kwa kumalizia, Tume inavitakia kila heri vyama vya siasa na wagombea wao, inawasihi kuweka uzalendo mbele kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Sote tuna wajibu wa kuhakikisha amani ya nchi inaendelea kuwepo na hatimaye kuwa na uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika.

Hili litawezekana iwapo kila mdau atatimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Kwa mara nyingine natoa rai kwa wapiga kura wote nchini kujitokeza kwa wingi kesho katika vituo vya kupigia kura ili kuwachagua viongozi mnaowataka.

**KUMBUKA KURA YAKO SAUTI YAKO, NENDA UKAPIGE KURA!**

**Jaji R (Mst) Semistocles S. Kaijage.**
**Mwenyekiti**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**Kiambatisho Na. 4: Orodha ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum**

| Na. | Jina Kamili | Chama |
|---|---|---|
| 1 | Najma Murtaza Giga | CCM |
| 2 | Neema Kichiki Lugangira | CCM |
| 3 | Sylvia Francis Sigula | CCM |
| 4 | Dkt. Ritta Enespher Kabati | CCM |
| 5 | Dkt. Paulina Daniel Nahato | CCM |
| 6 | Stella Ikupa Alex | CCM |
| 7 | Asya Sharif Omar | CCM |
| 8 | Neema Gerald Mwandabila | CCM |
| 9 | Khadija Shaban Taya | CCM |
| 10 | Tecla Mohamed Ungele | CCM |
| 11 | Lucy John Sabu | CCM |
| 12 | Bernadeta Kasabago Mushashu | CCM |
| 13 | Mariam Madalu Nyoka | CCM |
| 14 | Josephine Johson Genzabuke | CCM |
| 15 | Dkt. Alice Karungi Kaijage | CCM |
| 16 | Janeth Maurice Massaburi | CCM |
| 17 | Esther Edwin Malleko | CCM |
| 18 | Rose Cyprian Tweve | CCM |
| 19 | Fatma Hassan Toufiq | CCM |
| 20 | Munira Mustafa Khatib | CCM |
| 21 | Saada Mansour Hussein | CCM |
| 22 | Irene Alex Ndyamkama | CCM |
| 23 | Hawa Mchafu Chakoma | CCM |
| 24 | Juliana Didas Masaburi | CCM |
| 25 | Martha Jachi Umbulla | CCM |
| 26 | Shally Josepha Raymond | CCM |
| 27 | Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi | CCM |
| 28 | Maimuna Ahmad Pathan | CCM |
| 29 | Mwanaidi Ali Khamis | CCM |
| 30 | Jacqueline Kainja Andrew | CCM |
| 31 | Norah Waziri Mzeru | CCM |
| 32 | Bupe Nelson Mwakangata | CCM |
| 33 | Maryam Azani Mwinyi | CCM |
| 34 | Ummy Hamisi Nderiananga | CCM |
| 35 | Martha Nehemia Gwau | CCM |

| Na. | Jina Kamili | Chama |
|---|---|---|
| 36 | Mariam Ditopile Mzuzuri | CCM |
| 37 | Juliana Daniel Shonza | CCM |
| 38 | Mwantum Mzamilu Zodo | CCM |
| 39 | Zulfa Mmaka Omar | CCM |
| 40 | Khadija Hassan Aboud | CCM |
| 41 | Oliver Daniel Semuguruka | CCM |
| 42 | Latifa Khamis Juakali | CCM |
| 43 | Suma Ikenda Fyandomo | CCM |
| 44 | Ghati Zephania Chomete | CCM |
| 45 | Minza Simon Mjika | CCM |
| 46 | Aysharose Ndogholi Mattembe | CCM |
| 47 | Regina Ndege Qwaray | CCM |
| 48 | Kabula Enock Shitobela | CCM |
| 49 | Zaytun Seif Swai | CCM |
| 50 | Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge | CCM |
| 51 | Anastazia James Wambura | CCM |
| 52 | Zuena Athumani Bushiri | CCM |
| 53 | Aleksia Asia Kamguna | CCM |
| 54 | Asha Abdullah Juma | CCM |
| 55 | Santiel Eric Kirumba | CCM |
| 56 | Esther Lukago Midimu | CCM |
| 57 | Maida Hamad Abdallah | CCM |
| 58 | Munde Tambwe Abdallah | CCM |
| 59 | Rose Vicent Busiga | CCM |
| 60 | Mwantumu Dau Haji | CCM |
| 61 | Agnes Elia Hokororo | CCM |
| 62 | Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | CCM |
| 63 | Zainab Athman Katimba | CCM |
| 64 | Fakharia Shomar Khamis | CCM |
| 65 | Mariam Nassoro Kisangi | CCM |
| 66 | Neema Wiliam Mgaya | CCM |
| 67 | Amina Iddi Mabrouk | CCM |
| 68 | Catherine Valentine Magige | CCM |
| 69 | Marryprisca Winfried Mahundi | CCM |
| 70 | Angelina Adam Malembeka | CCM |
| 71 | Agnes Mathew Marwa | CCM |

| Na. | Jina Kamili | Chama |
|---|---|---|
| 72 | Marry Francis Masanja | CCM |
| 73 | Lucy Thomas Mayenga | CCM |
| 74 | Taska Restuta Mbogo | CCM |
| 75 | Subira Khamisi Mgalu | CCM |
| 76 | Asia Abdulkarim Halmga | CCM |
| 77 | Amina Bakari Yusufu | CCM |
| 78 | Janejelly James Mtate | CCM |
| 79 | Thea Medadi Ntara | CCM |
| 80 | Bahati Keneth Ndingo | CCM |
| 81 | Martha Festo Bariki | CCM |
| 82 | Wanu Hafidhi Ameir | CCM |
| 83 | Ng'wasi Damas Kamani | CCM |
| 84 | Judith Salvio Kapinga | CCM |
| 85 | Amina Ali Mzee | CCM |
| 86 | Pindi Hazara Chana | CCM |
| 87 | Josephina Tabitha Chagulla | CCM |
| 88 | Tauhida Cassian Gallos | CCM |
| 89 | Nancy Hassan Nyalusi | CCM |
| 90 | Furaha Ntengo Matondo | CCM |
| 91 | Amina Daudi Hassan | CCM |
| 92 | Christina Christopher Mzava | CCM |
| 93 | Janeth Elias Mahawanga | CCM |
| 94 | Husna Juma Sekiboko | CCM |
| 95 | Halima James Mdee | CHADEMA |
| 96 | Grace Victor Tendega | CHADEMA |
| 97 | Esther Nicholous Matiko | CHADEMA |
| 98 | Cecilia Deniel Paresso | CHADEMA |
| 99 | Ester Amos Bulaya | CHADEMA |
| 100 | Agnester Lambert Kaiza | CHADEMA |
| 101 | Nusrat Shaaban Hanje | CHADEMA |
| 102 | Jesca David Kishoa | CHADEMA |
| 103 | Hawa Subira Mwaifunga | CHADEMA |
| 104 | Tunza Issa Malapo | CHADEMA |
| 105 | Asya Mwadini Mohamed | CHADEMA |
| 106 | Felista Deogratius Njau | CHADEMA |
| 107 | Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | CHADEMA |

| Na. | Jina Kamili | Chama |
|---|---|---|
| 108 | Sophia Hebron Mwakagenda | CHADEMA |
| 109 | Kunti Yusuph Majalla | CHADEMA |
| 110 | Stella Simon Fiyao | CHADEMA |
| 111 | Anatropia Theonest Rwehikila | CHADEMA |
| 112 | Salome Wycliff Makamba | CHADEMA |
| 113 | Conchesta Leonce Rwamlaza | CHADEMA |